# ATHARI ZA SAYANSI NA TEKNOLOJIA KATIKA HADITHI ZA WATOTO: MIFANO YA NGANO KUTOKA WILAYA YA MICHEWENI PEMBA.

Na

Mbarouk Juma Mbarouk

Tasnifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii Katika Fasihi ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Dodoma

Octoba, 2015

## ITHIBATI

Aliyesaini hapa chini amethibitisha kwamba ameisoma na amependekeza tasnifu hii inayoitwa '***Athari za Sayansi na Teknolojia katika Hadithi za Watoto: Mifano ya Ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Pemba'*** na anapendekeza ikubalike na itumiwe kwa minajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi za Jamii katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

……………………………………

Prof. J. S. Madumulla

(**Msimamizi**)

Tarehe………………………….

**IKIRARI**

**NA**

**HAKIMILIKI**

Mimi, **Mbarouk Juma Mbarouk,** nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada nyingine yoyote.

Sahihi…………………………………………..

Kazi hii ni mali yangu na Chuo Kikuu cha Dodoma hairuhusiwi kuchukuliwa au kutolewa kopi, isipokuwa kwa idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

**SHUKURANI**

Kazi hii ni matokeo ya michango kutoka kwa watu mbalimbali. Ninalazimika kuwataja wachache kwa sababu ya uwingi wao. Kwanza kabisa natoa shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya na uwezo wa kukamilisha kazi hii. Pili, namshukuru sana msimamizi wangu, Prof. J.S. Madumulla, kwa mwongozo mkubwa wa kitaaluma alionipa katika kipindi chote cha utafiti. Alitumia muda wake kwa kuisoma kazi yangu, kuirekebisha, kunipa maelekezo na kunishauru kila ilipobidi bila kuchoka licha ya kuwa na majukumu mengi. Sina budi ila ni kumuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kumpa maisha yenye kila aina ya baraka ndani yake.

Tatu, nawashukuru walimu wangu wote walionifundisha kozi mbalimbali za masomo ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili. Nao ni Prof. J. S. Madumulla, Dkt. E. M. Songoyi, Dkt. M. S. Khatib, Dkt. R. Sebonde pamoja na Dkt. A. Ponera.

Nne, nawashukuru wanafunzi wenzangu niliosoma nao programu ya masomo ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili kwa mwaka wa masomo 2013/2015 kwa ushirikiano na ushauri wao wa kitaaluma walionipa katika kipindi chote tulichokaa pamoja kwenye maisha mapya.

Tano, nawashuru wanafamilia kwa ushirikiano mkubwa walionipa hadi kufikia hatua hii. Shukurani mahasusi zaidi nazipeleka kwa mke wangu, Maryam Hemed Said, kwa kunitia moyo katika kipindi chote nilichokuwa masomoni. Pia, nawashukuru wanangu Abdul-hamid Mbarouk Juma na Rahma Mbarouk Juma. Zaidi, ni wazazi wangu ninaowashukuru kwa kunizaa, kunilea na kunisomesha. Kwenu nyote niliowataja na ambao sikuwataja kwa majina nasema. “Ahsanteni sana’’

## TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa watoto wangu wapendwa, Abdul-hamid Mbarouk Juma na Rahma Mbarouk Juma, kwa kukosa malezi yenye mapenzi kutoka kwa baba yao, kwa wakati wote ambao nilikuwa mbali nao. Pia natabaruku kazi hii kwa marehemu baba yangu, Juma Mbarouk Juma, kwa msaada wake mkubwa kwangu wakati wa uhai wake. Kwa hakika, yeye ndiye aliyenionesha mwanga katika maisha yangu, hususan katika harakati za kutafuta elimu. Mungu amlaze mahala pema peponi. Amin.

Mwisho natabaruku kazi hii kwa mama yangu mpendwa, Salama Abdalla Omar, kwa moyo wake wa kutokata tamaa katika mchakato wangu wa kutafuta elimu, huku akiamini kwamba elimu ni ufunguo wa maisha.

## IKISIRI

Utafiti huu ulikuwa na lengo la kuchunguza hadithi za watoto, kwa kuangalia jinsi hadithi hizo zilivyoathiriwa na maendeleo ya sasa ya sayansi na teknolojia. Hususan, kwa kuchunguza mifano ya hadithi za ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Zanzibar. Utafiti ulibaini kwamba, sifa nyingi za Fasihi Simulizi zimebadilika au zimo katika mabadiliko makubwa. Hasa hasa katika kipindi hiki cha kukua na kuimarika kwa sayansi na teknolojia. Ikiwa hivyo ndivyo, basi ni dhahiri kwamba Fasihi Simulizi na vipera vyake inafaa vizidi kuchunguzwa zaidi, ili kujua ni kwa namna gani vipera hivyo vimeathiriwa na maendeleo hayo ya sayansi na teknolojia.

Utafiti huu umeongozwa na malengo matatu, ambayo ni kuchunguza madhara yanayotokana na sayansi na teknolojia jinsi yanavyoathiri usimuliaji na uhifadhi wa hadithi za watoto, hususan hadithi za ngano, kutathmini mchango wa sayansi na teknolojia katika maendeleo ya utanzu wa hadithi za watoto, kwa kuangalia mifano ya ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Zanzibar na lengo la tatu ni kuchunguza mwamko wa wanajamii wa Wilaya ya Micheweni walioupata kuhusiana na athari ya sayansi na teknolojia katika utanzu wa hadithi za watoto, kwenye mifano ya hadithi za ngano. Katika malengo matatu hayo kila lengo lilipewa nafasi kutegemea na matokeo ya utafiti wenyewe.

Katika tasnifu hii, mkabala uliotumika ni wa nadharia ya Uhalisia**.** Nadharia hii imekuwa na umuhimu mkubwa sana katika kupata matokeo bora ya utafiti huu. Kwani nadharia hii ya uhalisia imetusaidia katika kujiridhisha kwamba, kila lengo tulilolijadili linasawiri uhalisi uliopo katika jamii ambayo ililengwa kufanyiwa utafiti.

Matokeo ya utafiti huu ni kwamba, utatoa mchango mkubwa katika uga huu wa Fasihi Simulizi kwani ni sehemu muhimu ya chanzo cha taarifa za kifasihi. Utafiti huu unategemewa pia kuwa na faida kubwa kwa taifa, kwani utasaidia kufafanua hadithi za watoto, kwa kuangalia mifano ya ngano ambazo, kwa kiasi fulani, zinaelekea kupotea kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Pia utasaidia kuzifanya hadithi hizo zisambae na kufahamika na watu wengi ndani na nje ya nchi yetu.

## YALIYOMO

**ITHIBATI** ........ i
**IKIRARI NA HAKIMILIKI** ........ ii
**SHUKURANI** ........ iii
**TABARUKU** ........ iv
**IKISIRI** ........ v
**YALIYOMO** ........ vi
**ORODHA YA VIAMBATANISHO** ........ x
**ORODHA YA VIFUPISHO** ........ xi

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ........ 1
1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........ 1
1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti ........ 4
1.3 Malengo ya Utafiti ........ 5
1.3.1 Lengo la Jumla ........ 5
1.3.2 Malengo Mahususi ........ 5
1.4 Maswali ya Utafiti ........ 6
1.5 Manufaa ya Utafiti ........ 6
1.6 Sababu za Kuchagua Mada ........ 8
1.7 Nadharia ya Uchanganuzi wa Data ........ 9
1.8 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisia ........ 12
1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza ........ 12

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO** ........ 14
2.1 Utangulizi ........ 14
2.2.1 Vipengele Muhimu vya Fasihi Simulizi. ........ 17
2.3 Machapisho Kuhusiana na Fasihi ya Watoto ........ 18
2.4 Machapisho Kuhusu Hadithi za Watoto ........ 20
2.4.1 Ngano (vigano; hurafa) ........ 20
2.4.1.1 Istiara ........ 20
2.4.1.2 Mbazi ........ 21
2.4.1.3 Kisa ........ 21
2.4.2.1 Visakale ........ 21

2.4.2.2 Mapisi ........................................................................................ 21
2.4.2.3 Tarihi ......................................................................................... 21
2.4.2.4 Kumbukumbu ............................................................................. 22
2.4.2.5 Visasili ....................................................................................... 22
2.5 Sifa Bainifu za Hadithi za Watoto .................................................. 24
2.6 Mapitio Kuhusiana na Hadithi za Watoto kama Kipera cha Fasihi Simulizi ...... 28
2.7 Machapisho Kuhusiana na Sayansi na Teknolojia ........................... 30
2.8 Mapengo Yanayojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko ........... 34
2.9 Muhtasari wa Sura ya Pili ............................................................... 36

**SURA YA TATU: USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI** ................................ 38
3.1 Utangulizi ....................................................................................... 38
3.2 Mpango wa Utafiti ........................................................................... 38
3.3 Eneo la Utafiti .................................................................................. 38
3.4 Walengwa wa Utafiti ........................................................................ 39
3.4.1 Jamii ya Watafitiwa ....................................................................... 39
3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa ................................................................... 40
3.5 Ukusanyaji wa Data ......................................................................... 42
3.5.1 Mbinu na Zana za Ukusanyaji wa Data .......................................... 42
3.5.2 Mbinu ya Maktaba ........................................................................ 43
3.5.3 Mbinu ya Usaili ............................................................................. 43
3.5.4 Mbinu ya Dodoso ......................................................................... 43
3.5.5 Mbinu ya Ushuhudiaji .................................................................... 44
3.6 Njia za Kukusanyia Data .................................................................. 45
3.6.1 Zana za Kukusanyia Data ............................................................... 45
3.6.1.1 Kalamu na Karatasi ...................................................................... 45
3.6.1.2 Kinasasauti .................................................................................. 46
3.6.1.3 Kamera ya Dijitali ......................................................................... 46
3 .7 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data .................................................. 46
3.7.1 Udhibiti, Uchambuzi na Uunganishaji wa Data ................................ 47
3.7.2 Uchanganuzi wa Data .................................................................... 48
3.8 Vikwazo vya Utafiti (Changamoto) ................................................... 48
3.9 Mipaka ya Utafiti .............................................................................. 48

3.10 Muhtasari wa Sura ya Tatu ........ 49

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI** ........ 50
4.1 Utangulizi ........ 50
4.2 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Usimuliaji wa Hadithi za Watoto ........ 51
4.2.1 Kupungua kwa Uhai wa Hadithi za Watoto Wakati wa Utendaji ........ 52
4.2.2 Msimulizi Kutoichangamsha Vyema Hadhira yake Wakati wa Usimulizi ........ 53
4.2.3 Msimulizi Kuchanganya Mambo Mengi kwa Wakati Mmoja ........ 53
4.2.4..Msimulizi Kukosa Muda wa Kuipumzisha Hadhira yake Wakati wa Usimuliaji ........ 55
4.3 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Kuhifadhi Hadithi za Watoto ........ 56
4.3.1 Njia mbalimbali Zinzotumika Kuhifadhi Hadithi Za Watoto ........ 56
4.3.1.1 Njia ya Maandishi ........ 56
4.3.1.1.1 Athari ya Uhifadhi wa Hadithi za Watoto kwa kutumia Njia ya Maandishi ........ 57
4.3.1.2 Njia ya Vinasasauti ........ 58
4.3.1.2.1 Athari za Uhifadhi wa Hadithi za Watoto katika Njia ya Vinasasauti ........ 59
4.3.1.3 Njia ya Kompyuta ........ 60
4.3.1.3.1 Athari ya Uhifadhi wa Hadithi za Watoto kwa Kutumia Njia ya Kompyuta ........ 60
4.3.1.4 Njia ya Kanda za Video ........ 61
4.3.2.4.1 Athari ya Uhifadhi wa Hadithi kwa Kutumia Kanda za Video ........ 62
4.4 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Fani na Maudhui ya Hadithi za Watoto 63
4.4.1 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Fani Kwenye Hadithi za Watoto ........ 63
4.4.1.1 Uteuzi wa Maneno katika Hadithi za Watoto ........ 65
4.4.1.2 Matumizi ya Lugha ya Matusi katika Hadithi za Watoto ........ 67
4.4.1.3 Uchanganyaji wa Lugha katika Hadithi za Watoto ........ 68
4.4.1.4 Matumizi ya Mbinu ya Ucheshi katika Hadithi za Watoto ........ 68
4.4.1.5 Utungaji Katika Hadithi za Watoto ........ 69
4.4.2 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Maudhui ya Hadithi za Watoto ........ 70
4.4.2.1 Kuwaburudisha Watoto ........ 70
4.4.2.2. Kuelimisha Jamii ........ 72

4.5 Mchango wa Sayansi na Teknolojia katika Maendeleo ya Hadithi za Watoto.... 73
4.5.1 Mchango wa Sayansi na Teknolojia Kupitia Vyombo vya Habari.................. 74
4.5.2 Mchango wa Sayansi na Teknolojia katika Uwasilishaji wa Hadithi za Watoto ........................................................................................................................ 75
4.5.3 Mchango wa Sayansi na Teknolojia Katika Uhifadhi wa Hadithi za Watoto .. 75
4.5.4 Mchango wa Sayansi na Teknolojia katika Uchangiaji wa Mada .................... 77
4.5.5 Mchango wa Sayansi na Teknolojia katika Kuikosoa Jamii ............................ 78
4.6.. Mwamko wa Jamii ya Wilaya ya Micheweni Kuhusiana na Athari za Sayansi na Teknolojia Juu ya Hadithi za Watoto......................................................................... 81
4.6.1 Mwamko wa Jamii katika Ununuzi wa Vifaa vya Sayansi na Teknolojia........ 81
4.6.2 Mwamko wa Jamii katika Matumizi ya Vifaa vya Kisasa vya Sayansi na Teknolojia ........................................................................................................... 82
4.6.3 Urahisi na Upatikanaji wa Vifaa vya Sayansi na Teknolojia............................ 82
4.6.4 Mwamko Kutokana na Uwekezaji wa Vifaa vya Habari na Mawasiliano ....... 83
4.6.5 Mwamko katika Uimarikaji wa Biashara ya Vifaa vya Sayansi na Teknolojia 84
4.6.6 Muhtasari wa Sura ya Nne .................................................................... 85

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** .......... 86
5.1 Utangulizi........................................................................................ 86
5.2 Muhtasari wa Tasnifu ..................................................................... 86
5.3 Utoshelevu wa Mkabala wa Uchambuzi wa Data .............................................. 88
5.4 Mchango Mpya wa Utafiti huu ......................................................... 89
5.5 Maoni Kuhusu Utafiti Huu ............................................................... 89
5.6 Mambo Yanayotakiwa Kuzingatiwa Ili Kuondokana na Changamoto Hizo....... 91
5.7 Ugunduzi katika Utafiti huu............................................................ 93
5.8 Mapendekezo ya Mtafiti kwa Serikali ................................................ 94
5.9 Mapendekezo Kuhusu Tafiti Zijazo.................................................... 94
**MAREJELEO** ..................................................................................... 96
**VIAMBATISHO** ................................................................................. 100

## ORODHA YA VIAMBATANISHO

Kiambatanisho 1: Hojaji na Madodoso Yaliyotumika Kukusanyia Data za Utafiti Huu Kutoka kwa Wazazi, walimu, wafanyakazi wa Idara ya Habari na Wafanyabiashara. ……………………………………………………………100
Kiambatanisho 2: Dodoso kwa Watoto Waishio Wilaya ya Micheweni Katika Mkoa wa Kaskazini Pemba ........................................................................................ 101
Kiambatanisho 3: Hojaji/ Usaili kwa wadau mbali mbali wa Fasihi Simulizi ........ 104
Kiambatanisho 4: Picha Mbalimbali za Utafiti....................................................... 106

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili la Zanzibar |
| CD | Compact Disc |
| DVD | Digital Versatile Disc |
| ICT | Information Communication Technology |
| ITV | Independent Television |
| PCF | Pestallozi Children's Foundation |
| RTD | Radio Tanzania Dar es Salaam |
| TBC | Tanzania Broadcasting Cooperation |
| TAKILUKI | Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni. |
| TCRL | Tanzania Communication Regularity Authority |
| VCD | Video Compact Disc |
| ZBC | Zanzibar Broadcasting Cooperation |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Hadithi za watoto ni miongoni mwa tanzu za Fasihi Simulizi. Utanzu huu wa hadithi za watoto, kwa mfano ngano, umekuwa na matumizi makubwa miongoni mwa jamii kama njia ya kuelimisha, kuadilisha, kuhifadhi mila na utamaduni wa jamii husika, pamoja na kujenga maadili ya watoto katika jamii waliyomo. Lakini kwa sasa maendeleo ya sayansi na teknolojia, yameathiri sana utanzu huu, ikiwa ni pamoja na hadithi za ngano. Kwa kawaida hadithi za watoto, kama vile ngano, zimekuwa zikisimuliwa kwa njia ya ana kwa ana baina ya fanani na hadhira nyakati za usiku. Hali hii inarahisisha kupitisha maadili mema kwa watoto kupitia utanzu huu wa hadithi. Kwa kuwa hadithi hizo za watoto zimekuwa zikitumika kama nyenzo mojawapo ya kuwachonga vijana kimaadili, ili wakue wakiwa na mila zinazoendana na maadili ya jamii zao

Suala la hadithi za watoto hapa Tanzania linaonekana kupita katika vipindi kadhaa vya mabadiliko. Mabadiliko hayo, kwa kiasi kikubwa, yanaonekana yakisababishwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia, ambayo kwa miaka ya hivi karibuni, maendeleo hayo yanaonekana yakishika kasi katika vipengele mbalimbali vya maisha katika jamii. Jinsi dunia inavyobadilika kimaendeleo na fani za Fasihi Simulizi kwa mfano hadithi za watoto zinaendelea kubadilika.

Kutokana na mabadiliko hayo ya binadamu tangu alipomudu kutumia lugha na uwapo wa maendeleo endelevu, kutokea mapinduzi ya viwanda mnamo karne ya kumi na nane hadi karne ya kumi na tisa na baadaye kuingia kwa sayansi na

teknolojia, haya yote yamesababisha mabadiliko hadi katika Fasihi Simulizi na vipera vyake. Kikiwamo kipera cha hadithi za watoto.

Mapinduzi na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani yamekuwa yakienda mbio kiasi cha kuwaathiri binadamu wote. Kama asemavyo Mbiti (1969: 216), hakuna watu au nchi ambayo inaweza kubaki nyuma au kutoathiriwa na mabadiliko mapya. Kwa msingi wa kauli hiyo ni dhahiri kwamba hadithi za watoto katika Wilaya ya Micheweni nazo hazikuweza kukwepa mabadiliko hayo ya sayansi na teknolojia. Mabadiliko hayo kuhusiana na hadithi za watoto yatachunguzwa katika vipengele vya usawiri na uhifadhi wa hadithi hizo, kwa kutumia vyombo vya kisasa vya kisayansi kama vile televisheni, kompyuta, vinasasauti, redio na hata magazeti.

Kabla ya maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyofikiwa sasa katika jamii, utanzu wa hadithi za watoto ulikuwa ukiwasilishwa kwa njia ya mdomo, tena papo kwa papo. Fanani na hadhira walikuwa pamoja wakati wa utambaji. Bakize (2004) anaeleza kuwa msimulizi anapokuwa anasimulia, hushuhudia pia mwitiko na umakini wa wasikilizaji kwa kuwatazama jinsi wanavyoipokea hadithi yake. Hali hii humfanya msimulizi kuboresha uwasilishaji wake kwa kutumia mbinu na mitindo kadhaa, ili kuiteka hadhira kikamilifu na kukamilisha malengo yake. Kwa mfano, fanani kuishirikisha hadhira yake kuimba wimbo, kama sehemu ya hadithi anayoitamba. Hivyo, ili kuweza kusikia hadithi yoyote ile, ilikuwa ni lazima mtambaji wa hadithi na hadhira yake wakutane mahali pamoja. Na ikiwa fanani wa hadithi husika amefariki dunia, basi hadithi hiyo, ilitoweka kutokana na kupotea kwa vionjo vya ufundi wa mtambaji ambaye alikuwa amezihifadhi hadithi hizo kichwani. Hadithi zote zilizokuwa zinatambwa zilikuwa zimehifadhiwa kichwani mwa fanani

(mtambaji) na zilikuwa zikisambazwa kwa hadhira kwa kutumia njia ya mdomo pekee.

Siku hizi kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, hususan katika sekta ya habari na mawasiliano, watoto wengi wamekuwa wakisikiliza au kuangalia utanzu wa hadithi za watoto kupitia televisheni, redio na video. Kwa wakati wa sasa ili uweze kushiriki Fasihi Simulizi lazima umiliki vyombo kama vile redio, televisheni, video, Intaneti, magazeti, majarida na vitabu, kompyuta, CD, DVD na Ipadi. Vyombo hivyo vimeathiri sana utanzu huu wa hadithi za watoto hususan katika uwasilishaji wake, utendaji wake, usambazaji wake, pamoja na matini ya hadithi hizo. Wakati wa sasa mtambaji wa hadithi hizo si lazima awepo katika mazingira ambayo hadhira ipo kutokana na hadithi hizo kuhifadhiwa na kusambazwa kupitia vyombo hivyo.

Hivyo, hadithi za watoto waishio maeneo ya vijijini, kabla ya maendeleo ya sayansi na teknolojia zilikuwa zikihusishwa zaidi na mazingira ya jamii husika. Hii ilitokana na kutokuwepo kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo yalirahisha muingiliano wa habari na mawasiliano baina ya jamii moja na nyingine.

Kwa hivyo, kutokana na kukua na kuenea kwa sayansi na teknolojia, hususan teknolojia ya habari na mawasiliano, hadithi nyingi za watoto waishio vijijini zimepokea mabadiliko makubwa katika fani na maudhui, uwasilishaji, uhifadhi, usambazaji na matini zake ikilinganishwa na hadithi ambazo zilikuwa zikitambwa kabla ya kukua kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kwa sasa uwasilishaji wa hadithi za watoto kwa kutumia vyombo vya kisasa, mtambaji au fanani wa hadithi si lazima awepo katika mazingira ambayo hadhira ipo. Hali hii inatokana na hadithi hizo za watoto kuhifadhiwa na kutolewa kupitia vyombo hivyo vya kisayansi. Kwa mfano msimuliaji anasimulia hadithi yake huku akiwa katika studio za redio ama

televisheni. Hali hii hutoa fursa kwa hadhira kuweza kumsikiliza ama kumuangalia mtambaji katika maeneo yao na kuweza kufaidika na hadithi inayosimuliwa kwa wakati huo.

Kutokana na maendeleo yaliyofikiwa kwa sasa, uhai wa hadithi za watoto umepungua. Kwa kuwa mtambaji haonani ana kwa ana na hadhira yake. Muktadha, tukio na mada vilimfanya abadilike badilike ili kukidhi mahitaji ya kijamii ya hadhira yake.

Lakini kutokana na kuhifadhiwa katika vyombo vya kisasa, mtambaji hawezi kubadili hadithi yake, hata kama mazingira yake yamebadilika kutokana na wakati na mahitaji ya jamii husika ambayo inasawiriwa hadithi hiyo. Pamoja na kuwa hadithi za watoto ni nyenzo kubwa katika ufinyanzi wa maadili ya watoto, ili waweze kukua kwa mujibu wa mila na desturi za jamii husika inayosawiriwa hadithi hiyo. Hali hii imemfanya mtafiti kutathmini hali hiyo na kuona kwamba, ipo haja ya kuliangalia suala hilo, ili kufahamu mapungufu na mchango wa sayansi na teknolojia katika hadithi hizo za watoto huku tukijikita katika hadithi za ngano.

## 1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti

Katika kipindi kirefu utafiti unaohusiana na athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto, katika kipengele cha hadithi za ngano, inaonekana bado uchunguzi wake ni mdogo. Kwa mfano, uchunguzi uliofanyika kuhusu hadithi za watoto haukugusia athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia, katika hadithi hizo. Aghalabu tafiti nyingi zilizofanyika zilijikita katika kuangalia athari za sayansi na teknolojia katika Fasihi Simulizi na katika tanzu nyingine. Kwa mfano Steven (2011) alifanya utafiti kuhusiana na athari za maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika nyimbo za watoto. Kitundu (2011) alifanya utafiti kuhusiana na

athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia kwenye Fasihi Simulizi kwa kuangalia nyimbo za ibada ya Kikristo Tanzania. Naye Kitabuge (2011) alifanya utafiti kuhusiana na athari chanya na hasi za maendeleo ya sayansi katika Fasihi Simulizi. Kutokana na umuhimu na michango ya tafiti zao kuhusu athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia katika Fasihi Simulizi, utanzu wa hadithi za watoto (hususani ngano) haukupewa nafasi ya kuchunguzwa, namna ulivyoathiriwa na mabadiliko hayo.

Kwa mantiki hiyo, mtafiti wa tasnifu hii ameona bado kuna umuhimu mkubwa wa kujadili athari za sayansi na teknolojia ili kuweza kujua athari zake katika hadithi za watoto. Hali hiyo ndiyo kwa kiasi kikubwa ilitusukuma kufanya utafiti huu.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

### 1.3.1 Lengo la Jumla

Kuchunguza athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto kwa kuangalia mifano ya hadithi za ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Zanzibar.

### 1.3.2 Malengo Mahususi

Utafiti huu uliongozwa na malengo mahususi yafuatayo:

a) Kuchunguza namna sayansi na teknolojia inavyoathiri usimuliaji na uhifadhi wa hadithi za watoto, hususan ngano.

b) Kutathmini mchango wa sayansi na teknolojia katika maendeleo ya utanzu wa hadithi za watoto kwa kuangalia mifano ya ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Pemba.

c) Kuchunguza mwamko wa wanajamii wa Wilaya ya Micheweni walioupata kuhusiana na athari za sayansi na teknolojia katika utanzu wa hadithi za watoto, kwenye mifano ya hadithi za ngano.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Katika kufanikisha utafiti huu maswali yafuatayo yaliongoza utafiti:

a) Ni kwa namna gani sayansi na teknolojia inaathiri usimuliaji na uhifadhi wa hadithi za watoto, hususani hadithi za ngano?

b) Kwa jinsi gani sayansi na teknolojia imechangia maendeleo ya hadithi za watoto, kwa mfano hadithi za ngano?

c) Kuna mwamko gani walioupata wanajamii wa Wilaya ya Micheweni Zanzibar kutokana na athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia katika utanzu wa hadithi za watoto, hususan hadithi za ngano?

## 1.5 Manufaa ya Utafiti

Inatarajiwa kwamba matokeo ya utafiti huu yatawasaidia Wazanzibari, hususan jamii ya Wilaya ya Micheweni, kukuza ufahamu wao kuhusiana na mchango wa sayansi na teknolojia katika maendeleo ya Fasihi Simulizi katika kipera cha hadithi za watoto.

Utafiti huu umetusaidia kukusanya data na kuzihifadhi katika njia za kielekroniki na maandishi, kwa kuwa mambo mengi ya Fasihi Simulizi bado yamehifadhiwa vichwani mwa watu kama sehemu ya kutunzia kumbukumbu. Utunzaji wa kumbukumbu wa namna hii siyo thabiti, kwa kuwa wakati wowote data huweza kupotea au kusahaulika kutokana na maradhi au kifo.

Vile vile utafiti huu utaweza kufafanua kwa uwazi dhana hasi zilizoenea miongoni mwa jamii; ambapo jamii inaichukulia sayansi na teknolojia kuwa ndiyo sababu tu iliyosababisha mporomoko wa maadili miongoni mwa vijana, bila kuangalia sababu nyingine, hasa kwa kupungua kwa usimuliaji na matumizi ya hadithi za watoto katika jamii kama sehemu muhimu ya kujenga maadili.

Pia utafiti huu utasaidia kwa kiasi kikubwa kuonesha umuhimu wa kuikuza na kuhifadhi Fasihi simulizi, hususan kipera cha hadithi za watoto kwenye kipengele cha hadithi za ngano kutoka jamii ya Wilaya ya Micheweni Zanzibar, na kwengineko.

Vile vile utafiti huu utatoa mchango mkubwa katika uga huu wa Fasihi Simulizi kwani ni sehemu muhimu ya chanzo cha taarifa za kifasihi.

Utafiti huu utakuwa na faida kubwa kwa taifa, kwani utasaidia kufafanua hadithi za watoto, kwa kuangalia mifano ya hadithi za ngano ambazo, kwa kiasi fulani, zinaelekea kupotea kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Pia utasaidia kuzifanya hadithi hizo zisambae na kufahamika na watu wengi ndani na nje ya nchi yetu.

Utafiti pia utakuwa ni chachu na dira kwa kutoa mwanga kwa jamii ya watu wa Wilaya ya Micheweni na Zanzibar kwa jumla, kwa kuonyesha umuhimu wa kukua kwa sayansi na teknolojia, na mchango wake katika jamii ya Wilaya ya Micheweni na Taifa kwa jumla.

Matarajio ya utafiti ni kwamba, utashajihisha na kuwahamasisha watafiti wengine kufanya tafiti zao, katika kuchambua na kuchunguza jinsi ambavyo sayansi na teknolojia huathiri vipera vingine vya Fasihi Simulizi kama vile nyimbo, methali na

vitendawili. Ipo haja ya kufanya utafiti huo ili kuelewa hadhi ya vipera hivyo na jinsi vinavyoathirika kutokana na maendeleo hayo. Hii itafanyika kwa kuhusianisha na athari zinazojitokeza katika kipera cha hadithi za watoto.

### 1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Baada ya kuangalia kwa kina Fasihi Simulizi katika utanzu wa hadithi za watoto, hususan kwa kuchunguza baadhi ya hadithi za ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Zanzibar; tumeona kwamba, utanzu huo wa hadithi za watoto kwa kiasi kikubwa, umepata mabadiliko makubwa. Mabadiliko hayo, kwa kiasi kikubwa yanaonekana yakichangiwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo yameshika kasi katika jamii husika. Hivyo kwa kuangalia maendeleo haya ya sayansi na teknolojia, tumeshawishika kuchunguza athari zake na ili kuweza kufahamu ni kwa kiasi gani maendeleo hayo yameathiari utanzu wa hadithi za watoto, kwa kuangalia mifano ya ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Pemba.

Pia tumeamua kuchagua kutafiti eneo hili, kwa sababu tumepitia tafiti mbalimbali zinazohusu athari za sayansi na teknolojia, katika Fasihi Simulizi kuhusiana na tanzu zake mbalimbali. Lakini katika tafiti hizo bado watafiti hao, hawajaeleza katika tafiti zao athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto kwa kuangalia mifano ya hadithi za ngano. Hivyo, tumeona kuna umuhimu mkubwa wa kuangalia eneo hili la utafiti kwa kuziba pengo hilo. Katika kuchunguza athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto kuhusiana na mifano ya ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Pemba, lengo likiwa ni kutambua kwa undani jinsi sayansi na teknolojia inavyoathiri utanzu wa Fasihi Simulizi katika hadithi za watoto hususan hadithi za ngano. Kwa kuangalia utanzu huo wa ngano kama umeimarika au umedumaa, hasa

kutokana na kuwepo kwa sayansi na teknolojia, hususan katika usimuliaji na uhifadhi wake katika jamii iliyolengwa kufanyiwa utafiti huu.

### 1.7 Nadharia ya Uchanganuzi wa Data

Kwa mujibu wa mada husika, utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisia. Hivyo, ukusanyaji wa data na uchambuzi wake ulifanywa kwa kuzingatia nguzo-msingi ya nadharia hii ya uhalisia.

Nadharia ya Uhalisia kwa upana wake, humaanisha uwakilishi wa uhalisia wa mambo katika kazi ya Fasihi. Nadharia hii ilizuka katika karne ya kumi na tisa na ikikinzana na mkondo wa ulimbwende uliokuwapo katika kipindi hicho.

Mhalisia huamini matokeo ya mambo na ukweli unaopatikana katika kuchunguzwa kazi fulani, ukweli huo ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajirba. Vile vile wahalisia huamini demokrasia kama hali ya maisha, na mali hafi wanayochagua kuelezea maisha. Hivyo, Uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahususi na matokeo yanayoweza kuthibitika.

Neno uhalisia lilianza kutumika kwa mara ya kwanza na kuzungumnziwa kama moja ya matawi mawili ya falsafa ya enzi ya kati katika historia ya Ulaya. Kipindi cha enzi za kati kilitokea kati ya mwaka 1100-1500 BK. Aina nyingine ilikuwa falsafa iliyojishughulisha na ukweli na dhahania wa hali na vitu vilivyodhahiri ambavyo vinathibitika na binadamu kwa kutumia milango yake ya fahamu ni kama vile macho (kuona), masikio (kusikiliza), pua (kunusa), ulimi (kuonja) na ngozi (kuhisi).
Wellek (1965: 20) anaeleza kuwa dhana ya uhalisia ilianza kutumika kwa maana hii kutokea mwaka wa 1790. Katika mwaka huo Emanuel Kant katika chapisho lake

linaloitwa *Critique of Judgement* (1961) alitumia istilahi ya udhahania kikamilifu kama kinyume cha uhalisia.

Kufikia mwaka wa 1798 wahakiki kama vile Schiller walikuwa wakitumia maneno haya, yaani udhanifu (idealism) na uhalisia kutumika kama kinyume chake.

Katika kazi ya Fasihi, uhalisia huwa unaathiri uwezo wa kusawiri au kuelezea hali ya kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Hii ndiyo maana iliyotumika hata huko Ufaransa na waandishi kama vile Gustav Flambert (1850) katika kuelezea kazi ya sanaa inayoonesha maisha ya binadamu jinsi yalivyo.

Uhalisia kuhusu uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Katika kitabu chake kinachoitwa *Aesthetics* ( 1958) mwanafalsafa Hegel alitumia neno Uhalisia kumaanisha kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikolojia iliyowazungumka.

Imani ya wahalisia ni kwamba kazi ya Fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli na halisi. Hivyo basi, hata picha za ulimwengu atakazoziumba msanii zapaswa kudhihirisha hali hiyo ya ukweli wa dunia yenyewe kama tulivyoitaja hapo juu. Uhalisia ulizuka ili kuupinga ulimbwende ambao ulizingatia mambo ya halisi na yasiyo halisi maishani.

Wahalisia wanaona kwamba kazi ya Fasihi yapaswa kuwa sahihi iliyowazi na inayozingatia masuala halisi ya moja kwa moja bila kupiga chuku. Masuala kama ya kimaadili msanii hana budi kuyazingatia kwa kiwango fulani katika utunzi wa kazi yake. Wahalisia wanashikilia kwamba msanii anapaswa kuteua na kuwa na nia ya kuendeleza masuala yake kama yanavyowahusu watu katika hali halisi ya maisha

yao. Mwelekeo huu wa uhalisia katika utunzi umemfanya mhalisia kumuona muhusika kama kiungo muhimu sana katika kazi ya Fasihi.

Katika mawanda ya Fasihi, Uhalisia ulitokana na matatizo yaliyokuwa yakiwakabili watu, ambayo yaliwafanya kuutuhumu ulimbwende, mategemeo ya kilimbwende yalikuwa niya kinjozi zaidi yakilinganishwa na tabu zilizokuwa zikiwakabili watu. Walimbwende walikuwa wakijitungia mambo yasiyoweza kutendeka au kutunzika katika maisha, yaani walionekana kana kwamba wanaishi maisha ambayo ni sawa na mtu kuwa ndotoni.

Kulingana na nadharia hii, uelewaji wa maana ya hadithi za watoto huhusisha mambo mbalimbali ambayo watoto wanasawiriwa katika hadithi zao. Kwa msikilizaji yeyote wa hadithi, yaweza kuwa vigumu au si rahisi sana kuelewa maana ya baadhi ya maneno yatumikayo katika hadithi husika ambayo inasawiriwa. Iwapo msikilizaji au mhakiki wa hadithi hizo hatahusisha mambo yasemwayo katika hadithi hizo na uhalisia wa jamii husika.

Nadharia hii pia inasaidia kuelewa dhamira asilia ya hadithi za watoto wakati wanaposawiriwa. Kwa kuhusisha hadithi hizo katika mifumo mbalimbali ya maendeleo katika jamii, katika kuchambua na kuhakiki hadithi hizo.

Mhalisia anayezingatia nadharia hii ya uhalisia hupembua namna kazi inavyodhihirisha uhalisia wa mambo kupitia maudhui aliyoyazingatia. Hivyo basi, mhakiki hutazama jinsi ukweli ulivyodhihirishwa katika kazi ya Fasihi anayoishughulikia kulingana na uhalisia. Ufahamu wa mazingira na maisha anayolenga msanii wa kazi ya Fasihi ni nguzo muhimu kwa mhakiki wa kihalisia.

## 1.8 Mihimili ya Nadharia ya Uhalisia

Kwanza msanii katika kuzingatia nadharia ya uhalisia huandika kuhusu maisha yalivyo pasipo kuathiriwa. Kazi katika misingi ya kihalisia inaangazia maisha katika ngazi zote, za kisiasa, kiuchumi, kitamaduni, kijamii na kadhalika.

Vile vile wahusika katika sanaa za kihalisia husawiriwa wakiwa wa kawaida na wakiwasilisha jamii zao. Ukweli unafaa uonekane katika kuwaumba wahusika wa kawaida katika mandhari ya kawaida. Msanii wa kihalisia anawapata wahusika wake katika jamii yake   iliyo ya kawaida na inayojulikana.

Mhimili wa tatu ni kwamba lugha katika kazi hizi za kihalisia huwa ni ya kawaida na wahusika wanaitumia lugha kama ilivyo katika hali halisi ya ulimwengu.

Mhimili wa nne unahusu mandhari na matukio. Mandhari na matukio yanafaa kuwa yale yanayoweza kuonekana, kujulikana au kuwezekana.

Maudhui na matukio kwa kiasi kikubwa katika kazi za kihalisia yanatakiwa kulingana na yale ya jamii inayorejelewa.

Msanii huangalia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake. Yeye huchunguza mabadiliko ambayo hutokea katika kipindi fulani cha historia na namna ambavyo mabadiliko hayo husababisha hali mbalimbali. Hivyo basi, mwandishi wa kihalisia hutilia maanani mabadiliko ambayo yanatokea ili aweze kuwasawiri wahusika wake ama kile ambacho amekikusudia kifike kwa jamii yake aliyoikusudia

## 1.9 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Katika sura hii, tumejadili vipengele vya utangulizi kwa jumla, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, manufaa ya

utafiti, sababu ya kuchagua mada, nadharia iliyotumika pamoja na kuangalia mihimili ya nadharia iliyotumika na kumalizia na hitimisho la sura ya kwanza. Sura inayofuata imejikita katika kufafanua mapitio ya maandiko yaliyotumika katika utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.1 Utangulizi

Katika kufikia malengo ya utafiti: mapitio ya maandiko yaligawanywa katika makundi makuu matano. Kwanza, ni mapitio yanayozungumzia dhana ya Fasihi Simulizi na vipengele vyake muhimu vya kuzingatia. Pili ni mapitio yanayozungumzia Fasihi ya watoto.Tatu machapisho yanayohusiana na dhana ya hadithi, hadithi za watoto, sifa bainifu za hadithi za watoto. Nne mapitio yanayozungumzia hadithi za watoto kama kipera cha Fasihi Simulizi. Mwisho mapitio yanayozungumzia masuala ya sayansi na teknolojia kwa kutumia mapitio ya wataalamu mbalimbali ambao katika maandiko yao wamepata kuyaeleza. Lengo ni kufahamu na kutathmini ni kwa kiasi gani waandishi hao wamejikita katika ufafanuzi wa masuala hayo, ambayo ndio msingi wa utafiti wenyewe. Hatimaye tunataka kufahamu jinsi pengo la utafiti lilivyoweza kujitokeza, yaani yale mambo ambayo waandishi na watafiti hawakuyaangalia kwa upana wake katika kazi zao.

## 2.2 Machapisho Yanayohusiana na Dhana ya Fasihi Simulizi

Fasihi Simulizi kama dhana, imeelezwa na wengi kwa kuegemea nadharia na mitazamo mbalimbali. Hata hivyo ni muhimu tufahamu kwamba maana inayopewa dhana au kitu fulani, huwa inachukuana na matumizi ya dhana yenyewe, watu wanaohusika, mahali dhana hiyo inamotokea, na hata kipindi cha wakati husika. Hii ndiyo sababu twapata maana mbalimbali zikitolewa na wataalamu kuhusu Fasihi Simulizi. Kwa mfano, Mlacha (1995:22), anaeleza kuwa:

*Fasihi Simulizi ni kuwa moja katika maisha ya jamii ambayo huchangia katika kuendeleza na kuelimisha historia ya jamii husika.*

Mlacha alipokuwa akifafanua zaidi juu ya Fasihi Simulizi, alisema kuwa Fasihi Simulizi huchangia katika kuelimisha jamii kuhusu asili yake, chanzo na maendeleo ya utamaduni wake na maisha ya jamii hiyo kuanzia zamani.

Kwa kuzingatia maelezo haya ya Mlacha tunapoiangalia Fasihi Simulizi kwa jumla tunapata kipengele kimoja cha hadithi ambacho dhima yake ni kuelimisha, kuelekeza na kuburudisha jamii. Kama hizo ni miongoni mwa dhima za hadithi za watoto; Je kwa sasa dhima hizo bado zinapatikana au zimepotea? Hali hii ndiyo miongoni mwa mambo yaliyomsukuma mtafiti kufanyia utafiti suala hili, ili kuelewa ni kwa kiasi gani hadithi za watoto, zimeathiriwa na sayansi na teknolojia kutokana na kukua kwa maendeleo yalioshika kasi katika jamii husika, hususani kutokana na kuwepo kwa vyombo mbalimbali vya habari na mawasiliano. Vyombo ambavyo kwa kiasi kikubwa huwawezesha watoto kupata fursa katika kusikiliza na kuangalia vipindi vya watoto, vikiwamo vipindi vya hadithi za watoto ambazo hurushwa hewani na kusikika pamoja kuangaliwa sehemu mbalimbali.

Waandishi wengine ambao wameandika kuhusiana na dhana ya Fasihi Simulizi katika kazi zao ni pamoja na Kirumbi (1975:15) katika maelezo yake anaona kuwa:

*Fasihi Simulizi ni masimulizi tunayopokea mdomo kwa mdomo, Fasihi hii kuna utumiaji wa ulumbi ufundi wa kusema.*

Msimamo wa Kirumbi ni kwamba chombo cha kutongolea Fasihi Simulizi ni mdomo na kwa hivyo, katika Fasihi Simulizi tuna masimulizi. Pia masimulizi hayo huambatana na ufundi mkubwa ambao hulazimika msimuliaji kuuonyesha wakati anaposimulia kazi yoyote ya Fasihi Simulizi, ikiwa ni pamoja na hadithi za watoto.

Aidha amebainisha kuwa Fasihi Simulizi ni ya kale na ambayo hurithishwa kwa mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Ndyanao Balisidya (1982) anafafanua kuwa Fasihi Simulizi ni aina ya Fasihi ambayo hutumia mdomo na kuimbwa, kusambazwa kwa wasikilizaji na watumiaji wake. Fasihi Simulizi ikiwa ni sanaa itumiayo maneno katika kutoa dhana fulani, hutegemea sana nyenzo mbalimbali za kuonekana na kusikika zitumiwazo na binaadamu kujieleza. Jambo la msingi ni kubaini Fasihi Simulizi katika uwasilishaji wake, ambapo katika kutolewa kwake fanani na hadhira wanakuwa pamoja, na huweza kusikilizana na kuelewana.

Bakize (2014) anafafanua kuwa Fasihi Simulizi kupitia mfumo wa kidijitali siku hizi, Fasihi hiyo imekuwa ikihifadhiwa kwa njia ya maandishi na mifumo mingine ya kisasa. Hali ambayo inaonyesha kwamba Fasihi Simulizi iliyohifadhiwa kwa njia ya teknolojia ya kisasa haiwezi kuwa hai na halisi.

Mugyabuso Mlinzi Mulokozi (1996) kwa upande wake anatoa maana ya dhana ya Fasihi Simulizi kama ifuatavyo:

> *Ni Fasihi inayotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo na vitendo bila ya kuwepo kwa maandilizi.*

Kwa jumla tunapoangalia maana hiyo tutaona kwamba Fasihi Simulizi ni Fasihi inayotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo na vitendo bila ya maandalizi yoyote kufanyika kabla ya kusimuliwa mbele ya hadhira iliyokusudiwa. Ni Fasihi ambayo huimfungi fanani katika kujiandaa pindi anapotamani kuiwasilisha kazi yake kwa hadhira.

Mulokozi pia anaeleza kuwa, Fasihi Simulizi ni Fasihi inayotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo bila ya kutumia maandishi. Hivyo Fasihi Simulizi ni tukio linalofungamana na muktadha (mazingira) fulani ya kijamii na kutawaliwa na mwingiliano. Mwingiliano huu unaweza kuhusisha jamii moja na nyingine, hasa kutokana na kuibuka kwa sayansi na teknolojia, ambapo kupitia vyombo vya kisasa huweza kuzikutanisha jamii mbalimbali ulimwenguni.

Vile vile, Mrikaria (2007) wakati akitoa hitimisho kuhusiana na maana mbalimbali za Fasihi Simulizi kama zilivyotolewa na wataalamu alisema:

> *Fasihi Simulizi ni sanaa inayotumia lugha ya mazungumzo ya ana kwa ana katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira husika. Hii ni sanaa ambayo ujumbe wake upo katika mfumo mzima wa pande mbili za mawasiliano kuwepo pamoja ana kwa ana, hii ikimaanisha fanani yaani mtu anayerithisha na hadhira yaani mtu anayerithishwa.*

Kwa njia hii, Fasihi Simulizi hushirikisha au huwafikia watu wengi na mawazo ambayo jamii imeyakubali na maendeleo ya tanzu hizo za Fasihi yatakuwepo kwa kuyapitisha au kuyakabidhi kwa kuendelezwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine kwa njia ya mdomo.

### 2.2.1 Vipengele Muhimu vya Fasihi Simulizi.

(a) Msimulizi (fanani). Huyu huwa ni mtu ambaye anaitamba hadithi, kuimba wimbo au hata kuitaka hadhira yake iweze kuimba pamoja na yeye ama kupiga makofi au kutoa kitendawili au methali.

(b) Wasikilizaji au watazamaji (hadhira). Hawa huwa ni washiriki katika kutazama au kusikiliza fani za Fasihi Simulizi na mara nyingine huwa wanatumiwa na

fanani kama wahusika wa fani yake. Kwa mfano kushiriki katika kuimba wimbo au kupiga makofi wakati wa usimuliaji.

(c) Pahali. Hapa ni jukwaa au pahali ambapo tukio la Fasihi simulizi linatendeka. Pahali hapa paweza kuwa nyumbani, uwanjani, shule, kuzunguka moto, baharini na kadhalika.

(d) Tukio. Hili huwa tendo linalotendeka katika jukwaa la Fasihi Simulizi. Tendo hilo lawezakuwa ni usimuliaji wa hadithi, kutega vitendawili, kuimba wimbo/nyimbo au kutoa methali.

## 2.3 Machapisho Kuhusiana na Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto ni dhana yenye utata katika kuieleza, kwani sio rahisi kuweka mpaka kati ya Fasihi ya watoto naya watu wazima. Sababu ni kwamba watoto husoma vitabu vya watu wazima nao watu wazima vile vile husoma vitabu vya watoto. Kwa mujibu wa Jan (1969), Davies (1973) na Hunt (1994) wanaeleza kwamba Fasihi ya watoto ni ile inayowalenga, inayowavutia na kuwapa watoto burudani katika kuisoma au kuisikiliza.

Naye Wamitila (2010) anasema kuwa suala la ufafanuzi wa Fasihi ya watoto linaweza kueleweka kwa kukitwa katika mitazamo mikuu miwili. Mosi, Fasihi ya watoto ni ile ambayo hadhira yake ni watoto. Pili, Fasihi ya watoto ni ile ambayo msingi wake wa kidhamira na kimaudhui huwarejelea watoto.

Kwa upande wa Wafula (2011) katika kusaidia kuielewa dhana hii, amewagawanya watu katika makundi makuu manne. Anadai kuwa rika la utoto ni miaka 0-17,rika la ujana miaka 18-34,rika la wazazi/utu uzima miaka 35-52 na rika la wazee ni miaka 53- na kuendelea. Hivyo kwa mujibu wa mgawanyo huo, Fasihi ya watoto ni ile

inayowahusu watoto waliochini ya umri wa miaka 18. Mtazamo huo pia unaungwa mkono na Kahigi (1995:21) wakati akifafanua kuhusu vitabu vya kundi la watoto.

Kwa jumla, Fasihi ya watoto bado ni ngeni katika ulimwengu wa Fasihi. Ugeni huo unatokana na kwamba, hapo awali hasa kabla ya karne ya kumi na nane watoto walikuwa wanajumuishwa katika kazi za Fasihi za watu wazima. Watunzi na wachambuzi wa kazi za Fasihi walikuwa wanamchulia mototo kama hadhira au msomaji mwingine tu. Baada ya watunzi na wachambuzi wa kazi za watoto walipoanza kuona hadhira ya watoto kama kundi maalum linalotakiwa kutazamwa kwa upekee wake, na hapo ndipo Fasihi ya watoto ilipoanza kujulikana.

Fasihi ya watoto kwa nchi za Afrika Mashariki. Kwa mfano Kenya na Tanzania bado ni changa. Ngugi (2011) anakiri kuwa; Fasihi ya watoto huko Kenya imekua na kushamiri katika miaka ya hivi karibuni. Hali kadhalika ni sawa na hapa Tanzania kwani Fasihi ya watoto imeshamiri zaidi baada ya miaka ya 1990. Baada ya kuwepo kwa juhudi za maksudi baada ya kuinua uandishi na usomajiwa wa vitabu vya watoto kupitia mashirika mbalimbali duniani, kama vile British Council na Agha Khan Foundation. Baadaye mashirika mengine yaliongeza nguvu. Kwa mfano Book Aid International na Pestallozi Children’s Foundation (PCF).

Vile vile kuwepo kwa mradi wa vitabu vya watoto nchini Tanzania uliozinduliwa mwaka 1991. Mradi mwingine uliosaidia katika kukuza Fasihi ya watoto ni ule wa TUSOME VITABU uliofadhiliwa na Care International kwa kusaidia baadhi ya shule hapa Tanzania kufungua maktaba za vitabu vya watoto.

Pamoja na juhudi hizo zilizochukuliwa, bado kipera cha hadithi za watoto kama utanzu wa Fasihi ya watoto unaonekana haujachunguzwa kwa kina hasa kwa

kuhusisha na maendeleo ya sasa ya sayansi na teknolojia. Hali hii ndiyo iliyotusukuma kuliangalia suala hili. Ili tuweze kufahamu ni kwa namna gani utanzu huu umeathirika kutokana na maendeleo hayo.

### 2.4 Machapisho Kuhusu Hadithi za Watoto

Dhana za hadithi, pamoja na hadithi za watoto ni pana ambazo zimepata kufafanuliwa na wataalamu mbalimbali wa Fasihi. Hadithi ni miongoni mwa kipera cha Fasihi Simulizi. Wataalamu wa Fasihi Simulizi wamekuwa wakitofautina katika ugawaji wa vipera vya Fasihi Simulizi. Kila mmoja amekuwa na mawazo tofauti juu ya kipera cha hadithi katika tanzu za Fasihi Simulizi. Kwa mfano Mulokozi (1989) ameziweka hadithi katika utanzu wa masimulizi. Akifafanua kuhusiana na masimulizi anasema kuwa; 'masimulizi ni utanzu ya Fasihi Simulizi wenye kusimulia habari fulani'. Pia ameyagawanya masimulizi katika tanzu kuu mbili ambazo ni tanzu za kihadithi (za kubuni) na tanzu za kisalua (kihisitoria). Tanzu za kihadithi zina kipera kimoja ambacho ni ngano.

#### 2.4.1 Ngano (vigano; hurafa)

Hizi ni hadithi za kimapokeo zitumiazo wahusika kama wanyama, miti na watu kuelezea na kuonya kuhusu maisha. Vigezo vilivyotumika katika kugawa ngano ni kigezo cha lugha ambayo ni lugha ya kinathari, kigezo cha dhima ambacho huelezea au kuonya kuhusu maisha na kufurahisha. Kigezo kingine kilichotumika ni kigezo cha wahusika ambao ni wanyama, miti na watu. Kipera hiki cha ngano kinajumuisha vijipera vifuatavyo ambavyo ni istiara, mbazi na kisa.

##### 2.4.1.1 Istiara

Hizi ni hadithi ambazo maana yake ya wazi inawakilisha maana nyingine iliyofichika. Vigezo vilivyotumika katika kugawa kipera hiki ni kigezo cha lugha ambayo ni lugha ya mafumbo.

#### 2.4.1.2 Mbazi

Hizi ni hadithi fupi zenye mafunzo yatolewayo kama kielelezo wakati wa maongezi au kumkanya mtu. Kigezo kilichotumika katika kugawa kipera hiki ni kigezo cha dhima.

#### 2.4.1.3 Kisa

Hii ni hadithi fupi ya kufurahisha kuhusu tukio la kweli. Kigezo kilichotumika ni kigezo cha kidhima.

Utanzu mwingine wa masimulizi ni utanzu wa kisalua. Utanzu huu umegawanyika katika vipera vifuatavyo ambavyo ni visakale, mapisi, tarihi, kumbukumbu na visasili.

#### 2.4.2.1 Visakale

Haya ni masimulizi ya mapokeo juu ya wahenga au mashujaa wa kabila au taifa yenye kuchanganya chuku na historia (kama hadithi ya Liyongo). Vigezo vilivyotumika hapa ni kigezo cha wahusika ambao wapo katika historia yaani mashujaa fulani. Kigezo kingine ni fani ya ubunifu.

#### 2.4.2.2 Mapisi

Haya ni maelezo ya kihistoria bila kutia mambo ya kubuni. Hapa pia kigezo kilichotumika ni kigezo cha dhima ambacho huelezea mambo ya kihistoria yaliyo ya kweli.

#### 2.4.2.3 Tarihi

Haya ni maelezo au jedwali la matukio muhimu na tarehe zake. Kigezo kilichotumika hapa ni kigezo cha kidhima ambacho ni kuelezea matukio muhimu na

tarehe zake. Pia kigezo kingine ni namna ya uwasilishaji ambapo huwasilishwa kwa kutumia jedwali na lugha yake huwa katika maandishi.

#### 2.4.2.4 Kumbukumbu

Haya ni maelezo ya matukio muhimu yanayomuhusu mtu binafsi au jamii ya watu. Hapa kimetumika kigezo cha fani, ambayo ni fani za wasifu na tawasifu. Pia kigezo kingine ni kigezo cha wahusika ambao ni watu.

#### 2.4.2.5 Visasili

Hizi ni aina ya hadithi zinazofungamana na imani za dini na mizungu ya kijamii. Pia hizi ni hadithi za kale zenye kuwakilisha imani na mtazamo wa jamii inayohusika kuhusu asili ya ulimwengu na maisha yao. Kigezo kilichotumika ni kigezo cha kidhima ambacho huelezea shabaha ya maisha. Anafafanua hadithi kama, Fasihi yenye kusimulia habari fulani. Hivyo, hii ni Fasihi ya ki-hadithi na fani zake huwa na sifa zifuatazo: hueleza matukio katika mpangilio mahususi, huwa na wahusika; yaani watendaji au watendwaji, katika matukio yanayosimuliwa, hutumia lugha ya kimaelezo, utoaji au utambaji wake huweza kuambatana na vitendo au ishara na huwa na maudhui ya kweli na ya kubuni, na yenye funzo fulani kwa jamii. Kumbo hii inazo tanzu nyingi. Aghalabu zinazofahamika zaidi hapa kwetu ni hadithi za kubuni, kama vile visakale, mapisi, ngano, tarihi, kumbukumbu na visasili.

Mtaalamu mwingine ambaye amefafanua maana ya hadithi ni Habwe. (2010) yeye anaeleza kuwa hadithi ni utanzu wa kubuni ambao husimuliwa kwa lugha ya kinathari kwa lengo la kuburudisha, kukuza utamaduni na hata kuhimiza umoja na ushirikiano.

Kwa upande wa hadithi za ngano ni miongoni mwa dhana za Fasihi Simulizi ambazo baadhi ya wataalamu wamejaribu kuzifafanua. Kwa mujibu wa Wamitila (2003),

anasema, ‘Ngano ni hadithi ya kale ambayo ni moja kati ya tanzu maarufu za Fasihi Simulizi. Mianzo ni moja kati ya vipera au vitanzu vya hadithi simulizi. Ngano nyingi huwa “Hapo zamani za kale.’’ Ngano huwa na kawaida ya kupokezana katika jamii kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Ingawa zinaweza kubadilika kidogo kutokana na ufaraguzi wa wasimuliaji au watambaji. Hadithi hizi hubakia na ukale fulani katika muundo wake. Kwa kawaida ngano huweza kuwa na wahusika kama vile wanyama au binadamu.

Kwa upande wa TAKILUKI (1992) wanaeleza kuwa, ngano ni aina ya hadithi zinazowahusu, wanadamu, wanyama, mazimwi, majini, viumbe wengine waliopewa sifa na uwezo wa mwanadamu. Hadithi hizi hubuniwa na kisha kusimuliwa bila kuandikwa. Katika ngano fanani husimulia visa na mikasa iliyowafika: wanadamu, wanyama, mazimwi, majini na viumbe wengine ambao huitwa wahusika, kwa lengo la kumfunza mwanadamu yanayotokea katika ulimwengu wake. TAKILUKI (1992) wamezigawanya hadithi za ngano katika makundi mawili ambayo ni hekaya na khurafa.

Hekaya ni aina ya hadithi za ngano ambazo wahusika wake ni wanadamu ambao mara nyingine hushirikiana na: wanyama, mazimwi, majini na viumbe wengine wenye uhai na wasio na uhai. Katika hekaya tunaona mambo anayoyatenda mwanadamu. Kwa mfano: maajabu, wema, uovu, ushujaa na hata woga. Visa vya hekaya kwa kawaida huwa ni matukio ya kila siku na hasa migogoro inayotokea katika jamii, Lakini, kwa sababu hekaya ni kazi ya Fasihi, fanani huyasimulia matokeo haya kwa njia ya kisanaa. Anapofanya hivyo, anaweza kuongeza usanii kwenye hekaya hiyo. Mathalan anaweza kuongeza mambo ya kustajabisha, kutisha, kuchekesha na kuhuzunisha. Kwa hali hii hekaya huwa inabadilika kila inaposimuliwa; ndipo watu husema, Hadithi ina ncha saba, Maana yake ni kuwa

kila fanani ana uhuru wa kusimulia hadithi kwa namna anavyohisi itawavutia wasikilizaji (hadhira).

Aina ya pili ya hadithi ya ngano ni khurafa, ambayo ni aina ya hadithi ya ngano ambayo hubuniwa, Kwa kawaida wahusika wa khurafa ni wanyama, ndege na viumbe wengine wenye uhai na wasio na uhai. Wahusika wa khurafa kama walivyo wahusika wa hekaya ni wawakilishi wa matendo ya wanyama. Kutokana na sababu hiyo baadhi ya wanyama hupewa vyeo wanavyopewa wanadamu, kwa mfano: badala ya kumwita simba, huitwa "Mzee Simba.''

Kwa upande wa hadithi za watoto, Bakize (2014) anafafanua kuwa, hadithi za watoto ni aina ya hadithi ambazo hutambwa kwa watoto walio chini ya miaka kumi na nane. Hadithi za watoto ni miongoni mwa vipera vya Fasihi Simulizi ya watoto. Ingawaje suala la Fasihi ya watoto limekuwa na mitazamo kadhaa kutoka kwa wataalamu wa nyanja ya Fasihi. Kwa mfano, Wamitila (2010) anasema kuwa suala la ufafanuzi wa Fasihi ya watoto linaweza kueleweka kwa kukitwa katika mitazamo mikuu miwili. Mosi, Fasihi ya watoto ni ile ambayo hadhira yake ni watoto. Pili, Fasihi ya watoto ni ile ambayo msingi wa kidhamira na kimaudhui hawarejelea watoto. Lakini pia, ieleweke kuwa, nje ya mitazamo hiyo mtazamo mwingine unaweza kuwa Fasihi ya watoto ni ile iliyoandikwa au kusimuliwa na watoto wenyewe.

### 2.5 Sifa Bainifu za Hadithi za Watoto

Fasihi ya watoto ni mpya kwa kiasi fulani katika masikio ya wanafasihi. Fasihi hii si mpya kwa maana ya watoto kutohusishwa katika Fasihi kwa ujumla bali ni kutokana na kutotazamwa kwa kundi hili kwa upekee wake katika utanzu na uchambuzi wa kazi za Fasihi. Ni waandishi wachache wa Fasihi ambao wamejishughulisha katika

kuiyandikia Fasihi ya watoto. Kwa mfano Bakize (2014) amefafanua sifa mbalimbali za Fasihi ya watoto ikiwa ni pamoja na hadithi za watoto.

Sifa ya kwanza ya hadithi za watoto ni kwamba mwega wake wa kidhamira hujikita kwa watoto wenyewe. Yaani hadithi hizi zinawalenga watoto, kwa maana kwamba kidhamira Fasihi hii huzungumzia ulimwengu wa mtoto mwenyewe. Yaani hadithi hizi huakisi yale mambo ambayo mtoto anayafanya na anayoyawaza, yale mambo yanayomkuta katika maisha yake. Kwani hadithi yoyote ile isiyokuwa na dhamira zinazomlenga mtoto basi moja kwa moja haiwezi kuitwa hadithi ya watoto. Aidha, ieleweke pia kuwa mtoto haishi peke yake bali huishi katika jamii. Kwa hiyo, jamii pia inaweza kumuathiri mtoto kwa kiasi kikubwa sana. Hii inamaanisha kuwa Fasihi ya watoto pia inakuwa na athari za jamii kwa mtoto na pia mafunzo mazuri ya namna gani mtoto anaweza kuiathiri jamii. Kwa mfano, katika hadithi za watoto kuna baadhi ya hadithi ambazo zimeangazia imani ya ushirikina katika jamii, matukio ya kikatili dhidi ya watoto wenye ulemavu wa ngozi, mila na desturi, hata matatizo yanayowapata yatima, uzalendo kupitia historia ya harakati za ukombozi, kujenga ujasiri kwa watoto na vijana, kutii wazazi au watu wakubwa na watu wazima kuwanyanyasa watoto kingono.

Vile vile hadithi za watoto huwa na lugha nyepesi. Katika kipengele cha fani, hadithi za watoto kwa kawaida huwa na lugha nyepesi. yaani huwa na lugha yenye kiwango sawa na walengwa. Mara zote lazima iwe ni lugha changa. Uchanga wake kwa kawaida huwa na hadhi ya tungo kama sentensi fupi, mara nyingi hujiepusha na sentensi changamani zinazoweza kuwatanza watoto wakati wanaposawiriwa hadithi hizo. Ijapokuwa kuna watoto wachache ambao wana uwezo wa kipekee, bado mtambaji wa hadithi hawezi kufikiria hao wachache bali atafikiria hadhira pana na

kwa hivyo huirahisisha lugha ili watoto wote waelewe kwa urahisi. Ngugi (2011) anabainisha kuwa watoto husoma ili waweze kupata uzoefu na kuelewa umbo la lugha. Watoto wanaweza kutambua matumizi mbalimbali ya lugha kupitia wahusika katika hadithi na baadaye kupata maarifa ya matumizi ya lugha ambayo yatawasaidia kujieleza vilivyo.

Pia, mara nyingi hadithi za watoto huwa fupi. Hali hii hujitokeza kwenye hadithi hizo ili kuepusha kuwachosha watoto wakati wanaposoma ama kusawiriwa hadithi hizo. Kwa mfano, mtoto ukimpa kitabu asome kwanza huangalia picha na baada ya hapo anaangalia ukubwa wa hadithi yenyewe. Kama hadithi ni fupi humuhamasisha kuisoma kwa sababu anajua ataimaliza mapema. Na kama hadithi hiyo ni ndefu, mtoto hushikwa na uvivu hata kabla hajaanza kuisoma.

Hadithi za watoto huwa zinasheheni vielelezo (kwa mfano picha na michoro). Mara nyingi hadithi zinazowalenga watoto lazima ziwe na vielelezo. Vielelezo hivi huweza kuwa michoro na picha. Hii humfanya mtoto avutiwe zaidi na kuwa makini na ile hadithi kwa kuona kile anachokisoma kupitia michoro ama picha ambazo zimechorwa kwa kuwasilisha tukio lililokusudiwa katika hadithi.

Pia ujenzi wa wahusika wake katika hadithi za watoto hukitwa kwa watoto wenyewe. Mara nyingi watunzi wa hadithi za watoto huzingatia uhusika wa watoto wenyewe. Hata kama kutakuwa na wahusika ambao ni watu wazima lazima wahusika wakuu au waathirika wa kazi ya Fasihi, lazima wawe watoto. Pengine kwa njia hii ya watoto kuwa wahusika wakuu wa kazi husika kwa mfano, hadithi kunawafanya waanze kufanyia kazi yale anayokusudia mtambaji au mwandishi katika kipera husika cha Fasihi Simulizi. Kwa mfano watoto waweze kuchukua

majukumu yao kwa ajili ya utu uzima wa baadaye, kuwa jasiri, wazalendo, waaminifu, wavumilivu na wawajibikaji.

Sifa nyingine ya hadithi za watoto huwa na mwingiliano wa tanzu nyingine za Fasihi Simulizi kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, katika hadithi za watoto hujitokeza pia nyimbo, jambo hili kwa kawaida huwa hilikwepeki. Kama anavyoeleza Herman (2011) akifafanua dhima ya mwingilianotanzu katika hadithi za Kiswahili kwa watoto, anaainisha kuwa kazi nyingi za watoto huchanganya matini ili kuleta uhai wakati wa utendaji, kuchangamsha hadhira, kudokeza maudhui ya hadhira husika, kuvuta usikivu wa hadhira/wasomaji, kuwezesha kupokea mambo mengi kwa wakati mmoja, kuwaaminisha watoto juu ya yale yanayosimuliwa, kuipumzisha hadhira, kuiliwaza hadhira na kutambulisha utamaduni wa jamii husika.

Hadithi nyingi za watoto huwa zimesheheni mambo ya kifantasia, matumizi ya fantasia katika Fasihi, hususan hadithi za watoto ni suala la kawaida kwa kuwa ni sifa mojawapo ya kundi la Fasihi. Wamitila (2003) anafasili fantasia kama dhana inayotumiwa kuelezea kazi za Fasihi ambayo ina sifa ambazo zinakiuka uhalisia. Anaendelea kufafanua kuwa kazi za kifantasia ni zile zenye sifa za kindotondoto au za kutaka kuaminisha hali isiyo ya kawaida. Fantasia hutumika zaidi katika maandishi yanayolenga hadhira ya watoto. Hutumiwa katika kazi za kinathari ambazo huwa na mandhari ya ajabu, matokeo magumu kukubalika katika hali ya kawaida na hata wahusika wasioweza kupatikana katika hali ya kawaida. Wahusika hao ni kama vile mazimwi, mashetani, majini na vitu vyingine ambavyo havidhaniwi kuwapo katika jamii, yaani haviwezi kupatikana katika uhalisia.

Sifa nyingine muhimu katika hadithi za watoto nikuwa na muundo sahili. Kwa mujibu wa Madumulla (2009) muundo katika kazi ya Fasihi huonesha mjengo au

umbo la kazi inayohusika. Kwa hivyo muundo wa hadithi za watoto hujengwa na mfululizo wa matukio. Mfululizo huu ni lazima uwe na mantiki na pia ufuate utaratibu ili iwe ni rahisi kwa watoto kuielewa hadithi husika inayosimuliwa. Muundo hauna budi katika hadithi za watoto kuwa wa moja kwa moja, yaani kuwa na mwanzo, kilele chake na mwisho. Kwa namna hii mtoto anayesikiliza au anayesoma hadithi anaweza kufuata hadithi yenye muwala bila kutatizika. Kulingana na Arbuthnot na Sutherland (1947) wanasema kuwa watoto huutazama ulimwengu kama unaofuata sharia fulani, hivyo basi, kitabu cha mtoto cha Fasihi hakina budi kuwa na mpangilio mzuri wa mawazo ili kuwavutia katika usomaji wao.

## 2.6 Mapitio Kuhusiana na Hadithi za Watoto kama Kipera cha Fasihi Simulizi

Fasihi imegawanyika katika aina kuu mbili, nazo ni Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. Fasihi Simulizi inao urithi mkubwa kwa jamii kutoka kizazi hadi kizazi. Kwa kawaida, jamii hufundwa katika malezi na makuzi kupitia Fasihi Simulizi. Hivyo, Fasihi Simulizi ina uhusiano mkubwa na utamaduni wa jamii husika. Hadithi za watoto ni kipengele muhimu cha utamaduni. Hivyo, utafiti huu unachunguza athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto kwa kuangalia mifano ya hadithi za ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Zanzibar. Kwani hadithi za watoto ni kipera cha Fasihi Simulizi. Akizungumzia tanzu za Fasihi Simulizi, Khatib (2003:1) anasema kwamba tanzu za Fasihi Simulizi ni pevu, hai na zinashirikisha umma mkubwa. Tanzu hizi huingiza nyimbo, mashairi, hadithi, jando na unyago, misemo na mafumbo. Fasihi Simulizi hutongolewa kwa mdomo au kudhihirishwa ana kwa ana kwa jamii inayohusika au iliyokusudiwa. Hivyo hadithi za watoto ni miongoni mwa vipera vya Fasihi Simulizi kwa sababu zina sifa ya kutongolewa. Kwa mfano hadithi za ngano hutongolewa ana kwa ana baina ya fanani na hadhira yake.

Masebo na Nyangwine (2007) wameainisha tanzu za Fasihi Simulizi katika makundi manne, yaani hadithi, semi, ushairi na sanaa za maonyesho. Uainishaji huu wa tanzu za Fasihi Simulizi umekuwa na utata kwa sababu wengine wameainisha makundi sita, wengine matatu na wengine manne. Lakini kwa kuwa lengo lilikuwa ni kuonyesha tu jinsi kipera hiki cha hadithi za watoto kinavyopatikana katika Fasihi Simulizi, na haihusiani na uainishaji wa tanzu za Fasihi Simulizi, basi tutaendelea na kipera cha hadithi za watoto.

Kwa upande wa muktadha, Mulokozi (1989) anaeleza kuwa uwasilishwaji wa Fasihi Simulizi inazingatia ukweli wa msingi wa Fasihi hiyo. Fasihi Simulizi ni sanaa inayopita, isiyofungwa katika umbo maalum. Hivyo Fasihi Simulizi si kitu bali tukio. Kama yalivyo matukio mengine, Fasihi Simulizi hutawaliwa na mwingiliano wa vitu vitatu, yaani watu, wakati na mahali. Hivyo, andiko hili lilimsaidia mtafiti wa kazi hii kuelewa kuwa hadithi za watoto zinabadilika kulingana na wakati na mazingira, kutoka kipindi cha jamii moja na jamii nyingine kutokana na maendeleo ya jamii husika.

Naye Shelemi (2006:95) anasema kwamba Fasihi Simulizi ni chombo ambacho kinaendelea kukua na kubadilika, yaani haijatuwama mahali pamoja. Mabadiliko ya mfumo na amali za jamii yamesababisha mabadiliko katika kudhihirika kwake. Kwa jinsi hii, Fasihi Simulizi imekuwa chombo cha kulinda na kuendeleza amali za jamii kadri inavyojidhihirisha katika tanzu zake mbalimbali. Tanzu hizi ni pamoja ngoma, nyimbo, hadithi, majigambo na methali mbalimbali.

Hali kadhalika, Wamitila (2004:104) anaeleza kuwa hadithi za watoto kama kipera cha Fasihi Simulizi huhusishwa pia na utendaji. Kwa sababu inawasilishwa kwa hadhira kwa kutegemea sauti, kuimbwa na kughanwa. Si ajabu basi hadithi za watoto

zikaambatanishwa na mapigo ya makofi pamoja na sifa nyingine zinazohusishwa na utendaji, kama kubadilishwa kwa sauti na ishara za uso. Huu ndio msingi unaojidhihirisha kuwa hadithi za watoto ni kipera cha Fasihi Simulizi.

**2.7 Machapisho Kuhusiana na Sayansi na Teknolojia**

Kwa upande wa sayansi na teknolojia ambazo ni dhana muhimu katika utafiti wetu, ni dhana ambazo zinahusiana sana. Hivyo, wakati tunapozungumzia teknolojia, huwa tunazungumzia maendeleo ya juu zaidi ya kisayansi. Hivyo sayansi na teknolojia ni vitu ambavyo vinakwenda sambamba bila ya kuachana.Teknolojia ni maendeleo ya kisayansi katika hatua ya mwisho kabisa ambayo inaonekana.

Sayansi kwa mujibu wa sw.wikipedia.org (wiki/sayansi). Wanafafanua kuwa;

> *'' Sayansi ni maarifa yanayopatikana kwa kufanya vitendo, kutazama na kujaribu kweli zilizobainishwa pasi kuthibitisha''*

Kwa mujibu wa *Oxford Advanced Learners Dictionary of Current English* (2000:1051)

Inatoa fasili ya sayansi (science) kama ifuatavyo:

> *Knowledge about structure and behaviours of the natural and physical World based on facts that you can prove for example by experiment.*
>
> *Maana au elimu ya maumbile na mwenendo asili wa ulimwengu unaojikita katika msingi wa ukweli unaoweza kuthibitika kwa njia ya majaribio.*
>
> (Tafsiri yetu)

Kutokana na fasili iliyotolewa hapo juu ni dhahiri kuwa, neno sayansi ni elimu inayotolewa kwa uchunguzi, majaribio, vipimo na kuthibitishwa kwa utafiti au uchunguzi. Kwa madhumuni ya utafiti wetu, sayansi inatumika katika suala zima la

Fasihi Simulizi na hata tanzu zake za Fasihi Simulizi katika jamii yetu ya Kitanzania. Kitendo cha fanani kutumia zana au mitambo kama vile televisheni katika usimuliaji wa hadithi, hususan hadithi za watoto na kuweza kipindi hicho kurushwa hewani ili kuifikia hadhira iliyopo mbali ni tendo la matumizi na zao la sayansi.

Sayansi ilianza kama udadisi wa mtu mmoja mmoja. Lakini kadri maarifa yanavyopanuka ilikuwa ni vigumu kwa mtu mmoja kufanya mchango wa kujitenda hivyo, jumuiya zimebeba kusudi ambalo hapo mwanzo ilionekana kama ni shauku la mtu mmoja mmoja kama awali.

Sayansi na jamii huenda pamoja katika kuleta mabadiliko kwa kuwa mabadiliko huletwa na watu wenyewe (Sw. Wikipedia).

Kwa mujibu ( http.// tafakari net / ? cat = 8 march 2011).

Neno sayansi linatokana na neno, Scio, la Kilatini lenye maana ya kujua au kufahamu. Hivyo basi, sayansi ni taaluma ambayo hutumika katika kutafuta ukweli wa mambo katika jamii. Kwa mfano katika taaluma kuna masomo yanayochukuliwa kuwa ni sayansi yanajihusisha na kutafiti ukweli wa mambo iwe ni kwa kufanya majaribio (ambapo inakuwa sayansi tendeshi) au kwa kukisia kanuni za ukweli na kuzithibitisha (ambapo inakuwa ni sayansi nadharia).

Kwa mujibu wa Kadeghe (2000), sayansi ni elimu ambayo mtu huipata kwa kufuata taratibu za kisayansi katika kufikiria jibu na kutoa hitimisho. Mara nyingi elimu hii hupatikana kwa kufanya uchunguzi na ugunduzi.

Mwanasayansi ni mtu yeyote anayejishughulisha na upatikanaji wa elimu na maarifa kwa kufuata taratibu zenye njia maalumu za kisayansi.

Maendeleo ya sayansi na teknolojia ndicho chanzo cha kukua na kusambaa kwa vyombo vingi vya teknolojia. Vyombo ambavyo kwa kiasi kikubwa vinasaidia sana katika kufanikisha mawasiliano kwa kutumia vifaa kama vile; redio, video, televisheni, Intaneti, whatsap, magazeti na hata simu. Kwa kiasi kikubwa vyombo hivyo, ndivyo vinavyoathiri maendeleo ya Fasihi Simulizi katika kipera cha hadithi za watoto, zikiwamo hadithi za ngano, hususan katika zama hizi za maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Kwa mujibu wa Wamitila. (2003), katika *Kamusi ya Fasihi na istilahi* anasema:

> *Utandawazi ni dhana inayotumiwa kuelezea mikabala ya kitamaduni, kiuchumi na hata kisiasa ambayo inasisitiza muungano, na mahusiano yanayokiuka mipaka ya taifa, na inatambuliwa na kupungua kwa uwezo wa mataifa, dola na kuyadhibiti matukio hata katika maneno au nchi zao wenyewe. Huhusisha pia kani za kimazingira au kiutamaduni. Kwa mfano kuenea na kusambaa kwa tamaduni za kila aina kutoka sehemu moja hadi nyingine na kuathiri suala la Ujitambuzi. Msukumo wa utandawazi unatazamwa kama unayaathiri mataifa ya kimaskini vibaya kwa kuwa yanalazimishwa kushindana na mataifa makubwa.*

Katika kuangalia mapitio hayo, tumegunduwa kwamba, waandishi wengi katika maandishi yao bado hawajashughulikia suala la athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto, hususan hadithi za ngano, jambo ambalo limemsukuma mtafiti kulifanyia utafiti suala hili: ili kuchunguza kwa kina athari hizo za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto, kwa vile athari hizo bado hazijashughulikiwa na kuwekwa wazi na kupewa nafasi na watafiti ambao wamepata kufanya tafiti zao.

Kukua na kuenea kwa sayansi na teknolojia katika nyanja ya mawasiliano katika visiwa vya Zanzibar ikiwemo Wilaya ya Micheweni, kumesababisha kuenea kwa vyombo mbalimbali vya habari na mawasiliano. Vyombo hivyo vinaonekana kuleta

athari katika kipera cha hadithi za watoto, kama vile hadithi za ngano. Hivyo, mara nyingi watoto wamekuwa wakisikiliza hadithi za watoto kupitia redio na televisheni, na hata kusoma hadithi hizo kwenye vitabu au magazeti. Hivyo, athari inayojitokeza kwa fanani ni kutokuwa pamoja na hadhira yake wakati wa utambaji. Hali hii huifanya hadhira kukosa fursa ya kuongeza au kupunguza au hata kuuliza maswali yanayohusu hadithi ya watoto inayosawiriwa kwa wakati huo kupitia chombo cha habari husika. Hivyo kupitia utafiti huu tumekusudia kuchunguza ni kwa namna gani athari hizo zimeathiri kipera cha hadithi za watoto katika usimuliaji na uhifadhi wa hadithi hizo, katika kufikia lengo lake kwa jamii.

Athari hizi za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto zinaonekana kuchochewa na nyanja ya habari na mawasiliano. Mawasiliano ambayo yameigeuza dunia kuwa ndogo kama kijiji na kufanya muingiliano wa jamii mbalimbali kuwa pamoja. Hali hii imesababisha kujitokeza athari nyingi katika Fasihi Simulizi kwenye kipera cha hadithi za watoto, kama vile hadithi za ngano katika jamii ya Wilaya ya Micheweni.

Kwa mfano Konde (1984:232) anaeleza kuwa katika uchunguzi wake alioufanya aliona kuwa, kiasi cha watu milioni sita walisikiliza redio katika miaka ya sitini. Hivyo, kwa sasa ni dhahiri kwamba idadi ya wasikilizaji imeongezeka kutokana na kuongezeka kwa vyombo hivyo vya habari. Kitu ambacho kwa hakika hakiepukiki kutokana na maendeleo hayo, hususan katika eneo la Wilaya ya Micheweni, pamoja na kwamba maendeleo hayo ya sayansi na teknolojia yana manufaa kwa binaadamu katika kurahisisha kazi zake. Lakini kwa upande mwingine maendeleo hayo kwa kiasi kikubwa yameathiri Fasihi Simulizi katika kipera cha hadithi za watoto, hususan katika kipengele cha hadithi za ngano.

Kwa kuwa hadithi za watoto ni miongoni mwa kipera cha Fasihi Simulizi kilichoathiriwa na maendeleo haya ya sayansi na teknolojia katika jamii, hivyo kupitia utafiti huu tunakusudia kuchunguza ni kwa kiasi gani maendeleo hayo yamewakosesha muda vijana wa kukaa pamoja na wazazi wao, na kutambiwa hadithi za ngano.

### 2.8 Mapengo Yanayojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko

Pamoja na wataalamu mbalimbali kuchambua juu ya hadithi, hususan hadithi za ngano, bado zinaonekana hazijachambuliwa kwa kina kwa kuziambatanisha na athari za sayansi na teknolojia. Bado kazi hizo zimeacha mapengo kadhaa kuhusu kipengele cha athari za sayansi na teknolojia katika kipera cha hadithi za watoto, kwa mfano hadithi za ngano. Mapengo hayo yanadhihirishwa kupitia hoja zifuatazo:- Kwanza waandishi au wataalamu wengi waliojishughulisha na uchunguzi wa hadithi za watoto, hawakujikita zaidi kuzichunguza jinsi zinavyoathiriwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Wataalamu hao wamechunguza zaidi umuhimu wa hadithi hizo za Watoto kwa kuangalia dhima zake katika kujenga maadili ya jamii. Lakini hawakuangalia ni kwa jinsi gani hadithi hizo hubadilika kutokana na athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia. Maendeleo ambayo huchukua sura mpya siku hadi siku. Hivyo, utafiti huu unakusudia kuchunguza kwa kina, jinsi sayansi na teknolojia inavyoathiri kipera cha hadithi za watoto, na kuonyesha jinsi hadithi hizo zinavyobadilika.

Vile vile waandishi tuliowaangalia wameeleza jinsi sayansi na teknolojia inavyotumika kuhifadhi na kusawiri hadithi hizo, lakini hawakuweka wazi kuwa: uhifadhi na usawiri huo unaweza kuleta athari gani katika hadithi hizo za watoto? Kwa mfano vitumiwapo vifaa kama redio, televisheni ama mitandao ya kijamii, vyombo ambavyo wakati wa usawiri wa hadithi hizo humtenga fanani na hadhira

yake. Pia hadithi zinapohifadhiwa kwenye mfumo wa kikompyuta, watu wengi hawana uwezo wa kumiliki vifaa hivyo vya kisasa. Hali hii inahusisha magazeti, ingawa hadithi hizo hukaa muda mrefu, lakini tatizo linalojitokeza ni kwamba watu wengi hawajui kusoma na kuandika.

Athari hizi kwa kiasi kikubwa zimetokana na ukuaji mkubwa ulioshika kasi wa sayansi na teknolojia katika jamii zetu. Baadhi ya waandishi wa Fasihi wamekuwa wakiandika kazi zao kuhusiana na athari za sayansi na teknolojia bila kuambatanisha athari hizo katika kipera cha hadithi, hususan hadithi za ngano. Kwa mujibu wa McGrew (2008) anaeleza kuwa, sayansi na teknolojia ni mchakato wa kihistoria ulioingia Tanzania kutoka nchi za nje. Nao BAKITA (1969/70) wanaeleza kuwa nchini Tanzania, sayansi na teknolojia ilianza kidogo kidogo kujipenyeza katika Fasihi Simulizi wakati wa kipindi cha utawala wa kikoloni. Hali hii kwa namna moja ama nyingine ilisababisha mabadiliko kadhaa katika Fasihi Simulizi ya Waswahili. Lakini kwa bahati mbaya BAKITA hawakueleza mabadiliko hayo kwa kuonesha athari zake katika hadithi za watoto, kama vile hadithi za ngano na kuonesha mabadiliko gani yametokana na athari hizo.

Kwa jumla, sababu zinazotokana na sayansi na teknolojia ambazo zinaonekana kuiathiri Fasihi Simulizi na vipera vyake kama vile hadithi za watoto, bado hazijawekwa wazi na watafiti wa nyanja hii ya Fasihi Simulizi katika tafiti zao. Hali hiyo imeisababisha jamii kuwa na uelewa mdogo kuhusiana na athari za sayansi na teknolojia katika hadithi hizo za watoto. Kupitia utafiti huu tumekusudia kulifanyia utafiti suala hilo na kuliweka wazi, ili kuweza kufahamu sababu zake, na kwa namna gani sayansi na teknolojia imeiathiri hadithi za watoto. Kwani awali watoto walijumuika pamoja katika jamii zao mbalimbali wakiwa pamoja na wazee kwa

lengo la kusimuliana hadithi au vitendawili nyakati za usiku. Kwa hivyo, utafiti huu una lengo la kuchunguza hali ya kukosekana kwa mjumuiko wa pamoja nyakati za usiku kati ya wazee na watoto. Hali kadhalika kuchunguza namna ambavyo jamii imeathirika kwa jambo hilo.

Kwa upande wa Wamitila (2003) anasema kwamba ‘Mtambaji au mwasilishaji wa Fasihi Simulizi ana uhuru mpana sana kwa kuweza kubadilisha mbinu na hata muundo wa kazi anayoiwasilisha papo kwa papo.’ Kwa kuangalia hali hiyo twaweza kujiuliza kuwa, Je uhuru huu upo pia katika simulizi ambazo hutambwa redioni au kwenye televisheni? Kama uhuru huo haupo simulizi hizo zinapungua sifa za kuwa Fasihi Simulizi kwa sababu hiyo? Suala la uhuru wa msanii linaendana sana na lile la uthabiti na hata uhifadhi wa Fasihi Simulizi. Tunapoangalia hasa kuwapo kwa Fasihi hii katika vyombo vya kisasa vya habari, na namna vinavyotumika katika kuihifadhi na kuisambaza miongoni mwa jamii mbalimbali. Hapa tunapata fursa ya kuliangalia suala hilo kwa kuchunguza changamoto mbalimbali kwa upana ili tuweze kufahamu athari hizo.

Hivyo, utafiti huu utabainisha dhahiri athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto, kwa kuangalia mifano ya hadithi za ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Zanzibar. Hili ni eneo liloliteuliwa kufanyia utafiti huu. Ili kuweza kufahamu kiundani athari za sayansi na teknolojia, katika utanzu wa hadithi za watoto kwenye kipengele cha hadithi za ngano katika Wilaya hiyo.

**2.9 Muhtasari wa Sura ya Pili**

Katika sura hii, tumefanya mapitio ya maandiko ili kuona nini watafiti wengine wamefanya katika eneo hili au eneo linalokaribiana na mada yetu. Mapitio ambayo tuliyapata yamekuwa na umuhimu mkubwa sana katika kupanua mawanda ya

welewa wetu juu ya mada hii. Pia, tumefanikiwa kuyafahamu mapengo yaliyopo katika tafiti zilizofanyika. Baada ya kufahamu mapengo hayo, ni jukumu la utafiti huu kuziba baadhi ya mapengo yaliyojitokeza, hususan yale mapengo yanayohusiana moja kwa moja na malengo ya utafiti huu. Mapitio ya maandiko yamegawanywa katika makundi sita ambayo yanaonekana kuwa na uwazi mkubwa sana. Makundi hayo ni: Maandiko yanayohusiana na dhana ya Fasihi Simulizi, Maandiko kuhusiana na Fasihi ya watoto, vipengele muhimu vya Fasihi Simulizi, maandiko ya hadithi za watoto, sifa bainifu za hadithi za watoto, mapitio yanayozungumzia kipengele cha hadithi za watoto kama kipera cha Fasihi Simulizi.   Vile vile mapitio yanayohusiana na sayansi na teknolojia. Pia, katika sura hii ya pili tumeangalia mapengo yaliyojitokeza katika maandiko ya tafiti zilizokwishafanyika. Na kuifunga sura hii kwa kufanya hitimisho la sura hii ya pili. Sura inayofuata imejikita katika kuangalia usanifu na mbinu za utafiti.

## SURA YA TATU

## USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Sehemu hii inazungumzia mpango mzima wa utafiti, mkabala wa uchanganuzi wa data, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti ikihusisha jamii ya watafitiwa na sampuli ya watafitiwa na upatikanaji wake, ukusanyaji wa data, mbinu na zana zilizotumika katika ukusanyaji wa data kwenye utafiti huu. Pia inaelezea mchakato wa ukusanyaji data, udhibiti, uchambuzi na kumalizia na hitimisho la sura ya tatu.

### 3.2 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani na uwandani. Data mbalimbali zilikusanywa kutoka uwandani ambazo zinahusu hadithi za watoto, na jinsi hadithi hizo zinavyoathiriwa katika vipengele vya usimuliaji na uhifadhi kutokana na ukuaji wa sayansi na teknolojia.

Mbinu ya ufafanuzi na uelezaji wa mambo kwa undani zaidi, ndiyo iliyotamalaki katika utoaji wa matokeo ya utafiti huu. Data zilizokusanywa zilichambuliwa na kuhakikiwa. Hali kadhalika tulikwenda katika shule za msingi za Wilaya ya Micheweni Zanzibar. Lengo likiwa ni kuona ni kwa namna gani sayansi na teknolojia imeathiri hadithi hizo za watoto kwa watoto wanaoishi Wilaya hiyo.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika Wilaya ya Micheweni. Hii ni Wilaya moja kati ya Wilaya mbili za Mkoa wa Kaskazini Pemba. Eneo lake la Kaskazini la Wilaya hii limezungukwa na bahari ya Hindi. Kwa upande wa Magharibi wa Wilaya hii eneo lake kubwa limechukuliwa na msitu wa Ngezi. Upande wa Kusini mwa Wilaya kuna vijiji kadhaa vya Wilaya ya Wete kama vile vijiji vya Mzambarau Takao, Pandani,

Machengwe na Taifu. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka (2012) idadi ya wakaazi wa Wilaya ya Micheweni kwa mujibu Tanzania Communication Regularity Authority (TCRL) inakadiriwa kuwa na wakaazi laki moja thelathini na nane elfu na kumi na sita .

Mtafiti amechaguwa eneo hili kwa sababu ni eneo ambalo kwa kiasi kikubwa, kipera cha hadithi za watoto, yaani hadithi za ngano zilikuwa zikisawiriwa kwa njia ya ana kwa ana kati ya mtambaji na wasikilizaji nyakati za usiku. Hivyo mtafiti katika utafiti huu anataka kufahamu; namna jamii ya Wilaya ya Micheweni wanavyoona kutokana na uwepo wa sayansi na teknolojia katika Wilaya hiyo na jinsi inavyoathiri hadithi za watoto, hasa kutokana na kupungua kwa kiasi kikubwa mfumo huo wa usimuliaji wa hadithi hizo.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti (Kothari, (2004), Bryman (2004), Kombo na Tromp (2006). Walengwa wa utafiti huu ni makundi mawili, ambayo ni jamii ya watafitiwa kwa jumla wake na sampuli ya watafitiwa.

#### 3.4.1 Jamii ya Watafitiwa

Data za utafiti huu zilitarajiwa kupatikana kutoka katika makundi yafuatayo:-

a) Wanafunzi kutoka shule za msingi za Wilaya ya Micheweni Zanzibar, hususan kuanzia darasa la la nne hadi la saba. Kwa kawaida wanafunzi wa madarasa haya hupenda kusikiliza hadithi za watoto, kutoka kwa wazee wao au wakati mwingine kupitia vyombo vya habari.

b) Wafanyakazi kutoka Idara ya ya habari na mawasiliano na wengine kutoka katika redio jamii Micheweni.

c) Wakaazi kutoka katika jamii ya Wilaya ya Micheweni ambao wanajishughulisha na malezi ya watoto, hususan watoto wanaosoma shule za msingi za Wilaya hiyo.

Kuchagua watoa taarifa wachache ni bora zaidi kwa ajili ya kujibu maswali ya mdomo ili kumwezesha mtafiti kuandika muhtasari wa kile kizungumzwacho (Kothari, 1990). Kwa kuzingatia pendekezo la Kothari lakini kwa tahadhari kubwa ya kuchagua sampuli iliyobora ambayo itatuwezesha kupata data sahihi.

### 3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa

Uteuzi wa sampuli, kama unavyoelezwa na Bryman (2004) ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kutumika katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa kwani siyo rahisi kutafiti kundi zima. Utafiti huu ulitumia mbinu ya sampuli lengwa. Mbinu hii imejikita zaidi katika kuchagua taarifa zinazohusu athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto, kwa ajili wa kuzifanyia uchambuzi wa kina athari hizo. Ili tuweze kufahamu ni kwa namna gani athari hizo zimeathiri kipera hicho cha Fasihi Simulizi. Kama mtaalamu Mugenda (2003:50) anavyosema kuwa, katika kuitumia njia ya sampuli lengwa, mtafiti huchukua data ambazo zinahusu taarifa na malengo ya utafiti wake. Kwa ajili ya kufikia na kupata taarifa faafu. Sampuli ya utafiti itakuwa hivi:

a) Watu kumi (wanawake na wanaume, wenye umri kuanzia miaka 45 na kuendelea), wanaotoka katika jamii ya Wilaya ya Micheweni Zanzibar ambao wanaonekana kuwa na mwamko kiasi fulani kuhusiana na uwepo wa sayansi na teknolojia.

b) Wafanyakazi sita kutoka idara ya habari na mawasiliano pamoja na walimu watano kutoka shule tatu za msingi za Wilaya ya Micheweni.

c) Wafanyabiashara wa vifaa vya habari na mawasiliano ambao ndio hasa wanaowezesha kupatikana kwa vifaa hivyo vya kielektroniki. Vifaa ambavyo huwawezesha watoto kupata fursa ya kusikiliza na kuangalia hadithi za watoto kupitia vifaa hivyo kwa nyakati mbalimbali. Vile vile vifaa hivi hutumika katika kuhifadhia hadithi hizo.

d) Watoto kumi na tano kutoka shule tatu za msingi za Wilaya ya Micheweni wakiendelea na mchakato wa kutambiwa na kutambiana hadithi hizo za watoto.

e) Baadhi ya wafanyakazi wa maktaba kuu Pemba na maktaba ya Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA). Pia kupitia maktaba hizo kupata fursa ya kuangalia mapitio mbalimbali yanayohusiana na athari za sayansi na teknolojia katika hadithi hizo za watoto.

Kothari (2004:174) amekubaliana na ugawaji huu pale alipoeleza kwamba, ugawaji wa sampuli utaamuliwa na mtafiti kwa kuangalia mgawanyo wa makundi anayotegemea kuyatafiti, aina ya utafiti, aina ya sampuli na mengineyo. Sampuli hii imechaguliwa kulingana na aina ya utafiti ambao hasa hasa umejikita kwa wale ambao wanaonekana kuwa na mwamko kuhusiana na hadithi za watoto, pamoja na uelewa katika nyanja ya sayansi na teknolojia, hasa kwa kulinganisha na jamii ya Wilaya ya Micheweni Zanzibar. Kwa hivyo kupitia sampuli lengwa hizo, data zitakazopatikana kutoka kila kundi zitaongeza upeo wa kuelewa hadithi za watoto, na athari zake katika zama hizi za sayansi na teknolojia.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

#### 3.5.1 Mbinu na Zana za Ukusanyaji wa Data

Kwa mujibu wa Kothari (2004), mbinu za ukusanyaji data ni shughuli ya kukusanya data kutoka uwandani kwa kuwahoji wasailiwa. Ziko mbinu mbalimbali za kukusanya data, na kila mbinu ina ubora na manufaa katika kukusanya data za utafiti. Lakini ufaavu wa mbinu za kukusanyia data hutegemea na malengo ya utafiti, muda na tatizo la utafiti. Hivyo basi, kutokana na malengo ya utafiti huu. Mbinu zilizotumika kukusanya data za utafiti huu ni nne ambazo kwa ujumla wake zinakamilishana na kujalizana, nazo ni:-

i) Mbinu ya maktaba

ii) Mbinu ya usaili

iii) Mbinu ya dodoso

iv) Mbinu ya ushuhudiaji

Zipo sababu mbalimbali ambazo humfanya mtafiti kuamua kutumia mbinu zaidi ya moja katika kukusanya data. Kwa mujibu wa Kothari (2004) anasema kuwa mtafiti huamua kutumia mbinu za utafiti zaidi ya moja. Hivyo basi, katika utafiti huu sababu ya kutumia mbinu ya ukusanyaji data zaidi ya moja ni kwamba: zitasaidia kupata data ambazo zisingelipatikana kwa njia moja peke yake. Kama anavyosema Alderson (1992) hakuna mbinu iliyobora katika utafiti ikitumika peke yake. Ni vyema kukusanya data kutoka katika vyanzo na mbinu mbalimbali ili mtafiti aweze kuhakiki matokeo kupitia mbinu hizo. Katika utafiti huu mbinu hizo zilitumika kwa kukamilishana na kujalizana kama ifuatavyo:-

### 3.5.2 Mbinu ya Maktaba

Kothari (2004) anaieleza mbinu hii kuwa ni mbinu inayohusisha uchambuzi wa maudhui yaliyomo katika nyaraka kama vile vitabu, magazeti na maudhui ya maneno ambayo yanaweza kuwa ya maandishi au mazungumzo. Sababu ya kuchagua kutumia mbinu hii ni kwamba; kwa vile maktaba huhifadhi kumbukumbu mbalimbali, itarahisisha kupata data muhimu zinazohusu utafiti huu.

### 3.5.3 Mbinu ya Usaili

Babbie (992) anasema kuwa usaili unahusisha mawasiliano ya moja kwa moja baina ya mtafiti na wahojiwa na mtafiti hupata maelezo zaidi kuhusu baadhi ya mambo ambayo yasingeweza kuwekwa bayana kupitia mbinu nyingine ya utafiti. Sababu ya kuchagua kutumia mbinu hii ni kwamba ni mbinu inayoruhusu unyumbukaji katika mchakato wa kuuliza maswali, kuweka bayana istilahi ambazo zinaonekana hazieleweki kwa watu na kupata taarifa za ziada na za kina zaidi, hususan pale ambapo majibu ya watu wanaosailiwa hayaeleweki (Kothari 1990 na 2004) Hivyo, mbinu hii itafaa sana na kutusaidia kukusanya data za kutosha na zinazofaa.

### 3.5.4 Mbinu ya Dodoso

Kwa mujibu wa Kothari (2004), mbinu hii huhusisha uandaaji wa dodoso ambalo hutumwa kwa mhusika na ombi la kutaka kujibu maswali yaliyomo katika dodoso hilo na hatimaye kulirudisha kwa mtafiti. Dodoso huhusisha orodha ya maswali ambayo huwekwa katika mpangilio na utaratibu maalumu. Kothari (1990) anasema kuwa katika kiwango cha mahojiano ya msingi ya utafiti usiokuwa wa kitakwimu, undani wa taarifa za ziada kuhusu hisia, uzoefu na maarifa ya wahojiwa hujionesha vyema kupitia maswali funge. Hivyo katika utafiti huu mtafiti aliandaa maswali mengi ili kuwapa nafasi wahojiwa kujibu kwa uhuru na kuelezea hisia, uzoefu na

maarifa waliyonayo juu ya mada husika. Powell na Cannaway (2004) wanatoa sababu ya kupata data kwa njia ya maswali yaliyowazi kuwa humwezesha mtu kuelewa na kufahamu mtazamo wa mtu bila kushawishi mtazamo huo kabla hawajaonesha uelewa wao kuhusu suala hilo. Akishadidia mawazo hayo Patton (2002) anaeleza kuwa ili kuleta unaizi ama utambuzi wa washiriki unapaswa kuwapa nafasi kubwa ya kuelezea hisia zao, mawazo, uchunguzi na uzoefu wao. Hivyo, kazi ya mtafiti hapa ni kutoa muongozo ambao utawawezesha watu kujibu maswali kwa uwazi na kwa mtazamo wao kuhusu ulimwengu unaochunguzwa mawazo yao kwa kile kinachoendelea, uzoefu wao na msingi wa utambuzi wao. Sababu ya kuamua kutumia mbinu hii ya dodoso ni kwamba mhojiwa huwa huru kuelezea hisia, mawazo na maoni yake juu ya jambo fulani kwa uwazi zaidi. Hivyo, mbinu hii itasaidia sana kupata data za kutosha na kwa uwazi zaidi kwa kuwapa wahojiwa nafasi ya kuelezea mawazo, hisia, mtazamo na uzoefu wao (Patton, 2002).

### 3.5.5 Mbinu ya Ushuhudiaji

Kwa mujibu wa Ndunguru (2001:95), ushuhudiaji ni mbinu ya kukusanya data ambapo mtafiti hushiriki na kurekodi kile anachokiona, kukisikia na kuwa na uzoefu nacho. Katika mbinu hii mtafiti huwa na desturi ya kijichanganya na wahusika. Kwa hivyo, mtafiti wa kazi hii alipokwenda uwandani Wilaya ya Micheweni Pemba Zanzibar, alilazimika kwenda kushuhudia sehemu ambazo watoto hujumuika pamoja kusikiliza ama kuangalia hadithi za ngano katika vyombo vya habari, kama vile redio na televisheni. Mbinu hii ilitusaidia kupata data kwa kushuhudia na kuona, jinsi watoto wanavyoweka makini katika kusikiliza au kuangalia hadithi za watoto zinaposawiriwa kupitia vyombo hivyo vya sayansi na teknolojia.

### 3.6 Njia za Kukusanyia Data

Njia ambazo ziliweza kutumika na kusaidia katika kukusanya data na kuweza kukamilisha utafiti huu ni madodosi, hojaji kwa wanafunzi, walezi, walimu na baadhi ya wafanyakazi wa idara ya habari pamoja na watoto wakiwa katika sehemu za kuangalia televisheni ama kusikiliza redio wakati hadithi zinapotambwa kupitia vyombo hivyo.

Mwongozo wa mahojiano ulifanywa kwa kuwahoji wazee pamoja na watoto wa Wilaya ya Micheweni, kwa lengo la kufahamu mwamko wao kuhusiana na masuala ya sayansi na teknolojia katika utanzu wa hadithi za watoto, kwa mfano hadithi za ngano. Njia hii ya mahojiano ilirahisisha upatikanaji wa data za utafiti kwa urahisi, kwani ilishirikisha mahojiano ya wazee waishio maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Micheweni. Pia njia hii ya mahojiano ilirahisisha kupata data za ndani kutokana na kwamba, ilimruhusu mtafiti kusaili vipengele vya nyongeza kutoka kwa watafitiwa

Utafiti huu ulitumia njia hizo kwa sababu ndizo zilizoonekana kusaidia kupata data kwa kila sampuli iliyotumika katika kukamilisha utafiti huu.

#### 3.6.1 Zana za Kukusanyia Data

##### 3.6.1.1 Kalamu na Karatasi

Kwa mujibu wa Mulokozi (2003:5), matumizi ya vifaa vya utafiti kama vile, kalamu na karatasi ni bora, kwani ni vifaa vya jadi vya utafiti, na hapana shaka vitaendelea kutumika miaka mingi ijayo kwa vile ni vifaa rahisi kupatikana na vyepesi kutumika. Aidha ni vyepesi kubeba na havihitaji utaalamu wa pekee kuvitumia. Hivyo, kalamu na karatasi vilimsaidia mtafiti kuandika kumbukumbu ambazo alizipata kutoka maktabani na sehemu nyengine ambazo alikwenda kukusanya data .Hii ni pamoja na kuandika mawazo mbalimbali kutoka kwa watoto, walimu, wafanyakazi wa idara ya

habari, wazazi na walezi wa watoto pamoja na kuandaa madodoso mbalimbali ambayo yalitumika katika utafiti.

#### 3.6.1.2 Kinasasauti

Katika kupata taarifa mbalimbali kuhusiana na athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za ngano za watoto.Tulitumia kinasasauti kurekodi mifano ya hadithi za ngano mbalimbali kutoka Wilaya ya Micheweni, ambazo watoto wa Wilaya hiyo walikuwa wanazitamba katika maeneo yao. Hadithi hizo ziliweza kusaidia katika uchanganuzi wa data.

#### 3.6.1.3 Kamera ya Dijitali

Kamera ya dijitali ilitumika kuchukua picha mbalimbali za uwandani za matukio mbalimbali yaliyoshuhudiwa katika eneo la utafiti. Picha hizo zilitumika katika kuweka kumbukumbu mbalimbali za utafiti.

## 3 .7 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010:63) "data ni mkusanyiko wa taarifa za kiuchunguzi wa kitaalamu unaopelekea kupatikana ushahidi wa jambo''. Katika ukusanyaji wa data, utafiti huu ulifuata taratibu na miiko ya utafiti, Utafiti huu ulizingatia maadili na miiko yanayoongoza mchakato wa utafiti. Maswala kama vile uombaji wa ridhaa ya watafitiwa, utunzaji wa siri za taarifa, vyote hivyo ni vitu muhimu katika mchakato wa ukusanyaji wa data za utafiti. Mtafiti aliomba ridhaa ya utawala wa shule za msingi ambazo ziliteuliwa na baadhi ya ofisi za serikali ambazo zilihusika katika utafiti huu na watoto wenyewe ili watafitiwe. Data zote za uwandani zilikusanywa kwa njia ya mahojiano, ushuhudiaji pamoja na udodosaji. Kwa upande wa shule, walimu na watoto waligawiwa madodoso yanayohusu kuwapo kwa athari

za sayansi na teknolojia katika hadithi za ngano za watoto, kutoka Wilaya ya Micheweni Zanzibar.

Kitabu cha kumbukumbu za kila siku na kalamu vilitumika kunukuu data zilizopatikana katika mahojiano. Pia kamera ilitumika kupiga picha za watoto ambao walikuwa wanasimuliana hadithi wanapokuwa madarasani. Pia hata wale wanaosikiliza hadithi kupitia njia ya redio. Hali kadhalika tuliangalia jinsi hadithi hizo zinavyotambwa kupitia njia ya televisheni. Vile vile tulipiga picha vifaa mbalimbali vya sayansi na teknolojia ambavyo hutumika katika kurusha habari na mawasiliano pamoja na kuzihifadhi hadithi hizo za watoto kwa kumbukumbu za baadaye. Kinasasauti kilitumika kuwarekodi wahojiwa.

Utafiti huu pia uliweza kukusanya data za maktabani kwa kufuata mwongozo wa usomaji na kupitia tasnifu za tafiti, vitabu mbalimbali, majarida na vielelezo vingine. kwa lengo la kupata yale ambayo yamekwishafanywa na waandishi wengine kuhusu sayansi na teknolojia katika Fasihi Simulizi, hususan katika kipera cha hadithi za ngano za watoto. Aidha kutafuta habari kupitia katika mitandao kulitumiwa ipasavyo.

### 3.7.1 Udhibiti, Uchambuzi na Uunganishaji wa Data

Data zilizopatikana katika utafiti huu zilidhibitiwa kwa kutumia kinyonyeo, madaftari, kalamu na kinasasauti kwa wakati wa usaili. Taarifa zilizohojiwa kupitia hojaji zilihifadhiwa na kufupishwa katika daftari maalum. Pia data za maktabani nazo zilinukuliwa katika madaftari kwa lengo la kufanyiwa uchambuzi. Data zote hizi zilichambuliwa kwa mbinu ya ufafanuzi kwani utafiti huu siyo wa kitakwimu na kuunganishwa kwa utaratibu maalum.

### 3.7.2 Uchanganuzi wa Data

Data za utafiti huu zilichanganuliwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingangatia nadharia ya Uhalisia. Data zilizopatikana katika durusu za maandiko zilichujwa kwa kiwango kikubwa kwa sababu data hizo zilitumika iwapo tu zilikuwa za uhakika, zinakidhi na zinafaa kwa kazi yenyewe (Kothari 2004:111-112) Data zilizopatikana katika dodoso na usaili zilijumuishwa na zile za ushuhudiaji katika uchanganuzi na kuwasilishwa katika mfumo wa malengo ya utafiti. Hivyo, uwasilishaji wa uchanganuzi wa data ulikuwa katika mtiririko sawa na malengo ya utafiti.

## 3.8 Vikwazo vya Utafiti (Changamoto)

Kuna vikwazo mbalimbali vilivyoweza kujitokeza katika zoezi zima la utafiti huu ikiwa ni pamoja na kukosa ushirikiano wa moja kwa moja na baadhi ya wazazi na walezi. Tatizo hili lilitokana na sababu kuwa wengi wa wazazi na walezi hawakuwa na uelewa juu ya umuhimu wa kufanya utafiti. Hivyo mtafiti aliweza kujitahidi kuwaelimisha baadhi ya wazazi na walezi umuhimu wa utafiti huu, baadhi yao waliweza kuelewa na kutoa msaada pale walipoweza na kusaidia kufanikisha kupata data hizo.

Pia tatizo jingine ambalo lilijitokeza katika zoezi zima la ukusanyaji data zilipokuwa zinakusanywa na mtafiti, wakati mwingine kulikuwa na mvua ambayo ilisababisha kubadilka kwa ratiba ya ukusanyaji wa data zilizotumika katika kuukamilisha utafiti huu.

## 3.9 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu uliangalia na kuchunguza athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto; kwa kuangalia mifano ya hadithi za ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Zanzibar. Mifano mbalimbali ya hadithi za ngano kutoka jamii ya Wilaya ya

Micheweni Pemba zilitumika kama sampuli ya kuthibitisha nadharia yake. Kwamba, maendeleo ya sayansi na teknolojia yameathiri kwa kiasi gani utanzu wa hadithi za watoto, katika vipengele vya usimuliaji na uhifadhi hususani kwa kuangalia mifano ya ngano.

### 3.10 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Katika sura hii, tumeangalia mbinu na vifaa vilivyotumika katika utafiti huu.Vipengele ambavyo vimejitokeza katika sehemu hii ni pamoja na mpango wa utafiti,eneo la utafiti, jamii ya watafitiwa, sampuli ya watafitiwa, zana na njia za kukusanyia data, mpango wa ukusanyaji data na udhibiti wake, uchambuzi wa data na eneo la utafiti. Sura hii inaweka msingi wa namna ambavyo data zilizohusika na utafiti jinsi zilivyokusanywa. Uchaguzi makini wa mbinu na vifaa vya utafiti huu ulitusaidia kupata data zilizokuwa zinahitajika ili kukamilisha malengo ya utafiti huu. Sura ijayo imejikita katika uwasilishaji wa mjadala na matokeo ya utafiti

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia data mbalimbali zilizokusanywa wakati wa utafiti kutoka katika maeneo yaliyoteuliwa, ikiwa ni pamoja na data zile za maktabani. Mjadala juu ya uchambuzi wa utafiti ulifanywa kwa kuzingatia athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto kwa kuangalia mifano ya hadithi za ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Zanzibar.

Mtafiti aliongozwa na Nadharia ya Uhalisia iliyoasisiwa na Hegel (1958) Nadharia hii inasisitiza kwamba, kazi ya Fasihi yapaswa kuwa sahihi, iliyowazi na inayozingatia masuala halisi nayamoja kwa moja, bila kupiga chuku. Pia nadharia hii ya uhalisia husisitiza usawiri wa uhalisia katika ukamilifu wake, kama mtazamo wa uhalisia au masuala yanayoshughulikiwa hayana budi kuthibitika katika ulimwengu halisi.

Mjadala huu umegawanywa katika sehemu kuu tatu zinazoakisi maswali yaliyouongoza utafiti huu, na ndiyo yaliyosaidia katika kuukamilisha utafiti huu. Uchanganuzi wa data za utafiti huu ni muhimu katika kuangalia athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto, kwa kuangalia hadithi za watoto waishio Wilaya ya Micheweni Zanzibar. Vile vile sura hii imeonyesha mjadala, uchanganuzi na mapendekezo ya utafiti huu kuhusiana na athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto wa Wilaya ya Micheweni Zanzibar.

Kila wazo lililopatikana ambalo lilihusiana na utafiti huu tuliweza kulichukua, kama changamoto ya kuweza kuchunguza zaidi hadithi za watoto kwa kuangalia athari zake kwa kuhusisha na maendeleo hayo ya sayansi na teknolojia kwa watoto hao.

Sehemu ya kwanza inajadili namna sayansi na teknolojia, na hasa teknolojia ya habari na mawasiliano jinsi ilivyoathiri hadithi za watoto katika kipengele cha usimuliaji na uhifadhi wa hadithi hizo. Pia sehemu hii imeangalia jinsi ambavyo sayansi na teknolojia ilivyoweza kuiathiri fani na maudhui ya hadithi za watoto.

Sehemu ya pili inajadili kwa kina namna mchango wa sayansi na teknolojia ulivyosaidia katika kuchangia maendeleo ya hadithi za watoto, hususan katika uwasilishaji, uhifadhi, uchangiaji mada na pia kuangalia mchango wa sayansi na teknolojia katika kuirekebisha na kuikosoa jamii kutokana na kuanganishwa kwa kutumia vyombo hivyo vya kisasa. Pia kuangalia hadithi hizo zinavyoweza kufika katika jamii mbalimbali ikiwamo jamii ya watoto wa Wilaya ya Micheweni Zanzibar. Sura hii pia ilijikita katika kuchunguza mwamko wa jamii ya Wilaya ya Micheweni walioupata kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, hususan kwa kuhusisha mwamko huo na kipera cha hadithi za watoto. Hatimaye tutatazama mustakabali wa hadithi za watoto katika muktadha wa sayansi na teknolojia.

Mwisho wa sura hii tunatoa muhtasari kwa kudondoa mambo yote yaliyojadiliwa katika sura hii ambayo ndiyo matokeo ya utafiti wenyewe. Utafiti ambao umefanywa kwa watoto waishio Wilaya ya Micheweni Zanzibar.

## 4.2 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Usimuliaji wa Hadithi za Watoto

Katika sehemu hii mtafiti amebaini jinsi sayansi na teknolojia ilivyoweza kuiathiri Fasihi Simulizi, hususan kipera cha hadithi za watoto. Tutajikita kwa kuangalia hadithi za watoto kwa kuchunguza athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia katika usimuliaji na uhifadhi wa hadithi hizo.

### 4.2.1 Kupungua kwa Uhai wa Hadithi za Watoto Wakati wa Utendaji

Katika uwasilishaji wa Fasihi Simulizi, hususan kipera cha hadithi za watoto ni lazima pawepo na fanani na hadhira kwa wakati mmoja. Hali hii humfanya msimulizi anaposimulia, kushuhudia mwitiko wa wasikilizaji kwa kuwatazama jinsi wanavyoipokea hadithi yake. Hali hii humfanya msimulizi kuboresha usimulizi wake, kwa kutumia mbinu na mitindo kadhaa ili kuiteka hadhira na kukamilisha malengo yake. Lakini kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, Fasihi Simulizi, na hasa kipera cha hadithi za watoto kupitia vyombo vya kisasa ambavyo ni zao la sayansi na teknolojia; kwa mfano redio ama televisheni msimulizi wakati wa usimuliaji huwa yuko mbali na hadhira yake. Hali hii inadhihirisha ukweli kwamba Fasihi Simulizi hupungua uhai wake kwa kiasi kikubwa. Kwa kuwa fanani anakosa udhibiti wa hadhira yake wakati anaposimulia hadithi husika.

Kwa mfano, wakati tukiwa uwandani katika harakati za kukusanya data, tuliweza kuwashuhudia watoto jinsi wanavyokipokea kipindi cha hadithi za watoto kinachorushwa hewani kila siku ya Jumamosi kupitia kituo cha televisheni cha ITV. Katika uchunguzi tulishuhudia kuwa, badala ya watoto kuwa makini kusikiliza hadithi kupitia kituo hicho cha televisheni cha ITV “Hadithi Club’’Mtafiti baadhi yao walifanya vitu Fulani tofauti tofauti. Kwa mfano mtoto Rahma Said Mwinyi mwanafunzi wa darasa la Sita, mwenye umri wa miaka kumi na nne alikuwa na mazungumzo na watoto wenzake. Jambo hili linapotokea huwa linamnyima fursa fanani aliyeko kwenye chombo cha habari husika kushuhudia yale yanayotendwa na hadhira yake. Hii ni kwa sababu hayuko pamoja ana kwa ana na hadhira yake anayoisimulia hadithi kwa wakati huo.

### 4.2.2 Msimulizi Kutoichangamsha Vyema Hadhira yake Wakati wa Usimulizi

Kwa kawaida, katika usimuliaji wa hadithi, msimulizi ndiye mwanzilishi wa mazungumzo kati yake na hadhira. Baada ya hapo huanzisha mazungumzo ya kiusimulizi, huku wasikilizaji wakiwa kimya kumsikiliza. Wakati fulani baadhi ya wasikilizaji huanza kusinzia au kuhisi uchovu. Hali hii humfanya msimulizi achanganye tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi ili kuifanya hadhira ichangamke. Kwa mfano, msimulizi wakati anapotamba hadithi basi anaweza kuimbisha nyimbo au hata kutumia semi za kuchekesha. Kufanya hivyo husababisha hadhira iwe imechangamka na kumfuatilia kikamilifu msimulizi na kwa umakini zaidi.

Lakini kwa sasa maendeleo ya sayansi na teknolojia yanamfanya fanani awe mbali na hadhira yake. Mtafiti amebaini kwamba, hali hiyo inamfanya fanani ashindwe kupambanua hali ya watazamaji ama wasikilizaji wake, wakati anaposimulia hadithi yake. Hivyo, wakati fanani huyo anapokuwa anasimulia katika chombo cha habari, na huhisi kwamba wasikilizaji wake wanamsikiliza kwa makini. Aghalabu hali huwa ni tofauti na fikra zake. Kwa mfano, wakati tukiwa uwandani, tuliwashuhudia baadhi ya mwanafunzi wanaosoma darasa la Saba hawakuwa makini katika kusikiliza hadithi zilizokuwa zinatambwa na watoto wenziwao, wakati kipindi cha watoto kinarushwa na ZBC. Muda mwingi watoto hao, walionekana kusinzia wakati hadithi zikiwa zinasimuliwa, Mtafiti alibaini kwamba, suala hili lilitokana na hadhira kuwa mbali na fanani wakati wa usimuliaji. Hivyo, watoto hao walikosa kuhamasishwa na fanani huyo kiasi cha kutokuwa makini katika kusikiliza.

### 4.2.3 Msimulizi Kuchanganya Mambo Mengi kwa Wakati Mmoja

Kwa kawaida msimuliaji katika Fasihi Simulizi huwa hafungwi na kipengele cha wakati, pindi anapowasilisha kazi yake ya kifasihi. Hali hii kwa kiasi kikubwa

inaisadia hadhira husika kufahamu kwa urahisi kipera cha hadithi kinachosimuliwa kwa wakati huo.

Dhima mojawapo ya hadithi za watoto kwa jumla ni kuifunza jamii ili iweze kupata elimu kwa ajili ya maendeleo. Katika Fasihi ya watoto dhima ya kumfundisha mtoto kwa kutumia hadithi ni nyenzo muhimu sana. Msimuliaji anapokuwa anasimulia, wakati huo huo huwa anaifundisha hadhira yake. Hivyo, msimulizi mara nyingi hutumia ubunifu wake wa hali ya juu ili kuhakikisha kuwa msikilizaji anaelewa vizuri. Utafiti umebaini kuwa hali hii huwa ni tofauti wakati usimuliaji unapofanywa katika vyombo vya habari vya kisasa. Mara nyingi msimuliaji wa hadithi anapokaribishwa kwenda kurusha kipindi chake katika studio hufungwa na wakati. Kwa mfano, mambo mengi aliyojiandaa kuyafikisha hulazimika kuutumia muda huo mchache aliopangiwa na uongozi wa chombo cha habari husika kukamilisha masimulizi yake. Hali hii ya kuwasilisha mambo mengi kwa muda mfupi, utafiti umegundua kwamba, huwafanya watoto wasifahamu vya kutosha kile ambacho msimulizi ameazimia kukiwasilisha kwa hadhira yake. Hivyo kama msimuliaji alipanga kuelimisha jamii yake kuhusu jambo fulani, inakuwa ni nadra kufahamika kama alivyokusudia. Uthibitsho wa haya umepatikana wakati wa ukusanyaji wa data ambapo tuliweza kuwakuta watoto wamekaa wanasikiliza hadithi kupitia kwenye redio. Lakini baada ya kipindi kumalizika tulipowataka watoto hao watueleze lengo la hadithi iliyosimuliwa walisema kuwa hawakufahamu chochote wakati wa hadithi hiyo ilipokuwa inasimuliwa. Said Abdalla Kombo, mtoto wa darasa la tano wa Skuli ya Msingi Tumbe alisema “Wakati wa usimuliaji, msimuliaji alikuwa anasimulia hadithi haraka haraka sana, kiasi kwamba pamoja na kusikiliza kwa makini sikuambulia kitu chochote,’’

Katika usimulizi wa hadithi kwa watoto, sawa na mfano wa mwalimu darasani, fanani anapaswa kuyapangilia anayotaka kuyasimulia katika utaratibu utakaoepusha mkanganyiko miongoni mwa watoto au hadhira iliyolengwa kusimuliwa. Hali hii huisaidia hadhira yake kuwa na uwezo wa kujifunza kile alichokipangilia katika kipindi chake. Kwa kuwa hadhira iko mbali inakosa fursa ya kuuliza pale panapojitokeza utata. Hivyo inakuwa ni vigumu elimu iliyokusudiwa kufikishwa, kwa kiwango kilekile kama wakutanapo fanani na hadhira ana kwa ana.

### 4.2.4 Msimulizi Kukosa Muda wa Kuipumzisha Hadhira yake Wakati wa Usimuliaji

Msimulizi wa hadithi za watoto mara nyingi husimulia hadithi yake huku akifuatilia mwitiko wa wasikilizaji wake. Kama ni hadithi iliyoandikwa, mwandishi anakuwa msimulizi lakini wakati huo huo akijifanya msikilizaji kwa kuhisi kuwa mahala fulani panahitajika kuipumzisha hadhira yake. Hufanya hivyo ili kuwahamasisha watoke kidogo kwenye simulizi. Kwa mfano, msimulizi wa hadithi anaweza kutumia mbinu za sanaa ya maonyesho, kama vile uigizaji, mabadiliko ya sauti, ishara, mikunjo ya uso na mbinu kadhaa nyinginezo. Utafiti huu amegundua kuwa, mbinu hizi za kuipumzisha hadhira hukosekana wakati masimulizi yanapofanywa kupitia vyombo vya habari vya kisasa. Hali hii humkosesha fanani fursa ya kuipumzisha hadhira yake wakati wa usimuliaji. Vyombo hivyo, yaani redio na televisheni huinyima hadhira mapumziko hadi kuisha kwa kipindi kinachorushwa hewani. Kwa hali ya kawaida, watoto wadogo wanaposimuliwa hadithi huhitaji muda wa kupumzishwa. Hii inatokana na kwamba, watoto wadogo bado akili zao hazijakomaa kubeba mambo mengi kwa muda mfupi.

### 4.3 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Kuhifadhi Hadithi za Watoto

Kukua na kuimarika kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia katika nyanja mbalimbali katika jamii, ikiwa ni  pamoja na mfumo mzima wa uhifadhi wa hadithi za watoto kubadilika, kumeifanya jamii kubuni njia mbalimbali za uhifadhi wa kazi za kifasihi.

#### 4.3.1 Njia mbalimbali Zinzotumika Kuhifadhi Hadithi Za Watoto

Kukua kwa sayansi na teknolojia katika jamii, kumesababisha kubuniwa kwa njia mbalimbali za kisayansi, ambazo kwa namna moja ama nyingine zinasaidia kuhifadhiwa kwa vipera mbalimbali vya Fasihi Simulizi. Vipera hivyo ni kama vile vitendawili, nahau, methali na hata hadithi za watoto kwa kutumia vyombo vya kisayansi kama vile kompyuta, kanda za kunasia sauti, maandishi, flashi, CD, VCD na hata DVD. Licha ya vyombo hivi vya kisasa kuwa na mchango mkubwa katika kuhifadhi kumbukumbu za hadithi za watoto kwa muda mrefu, kwa upande mwingine vyombo hivyo vimekuwa na madhara mbalimbali kwa kipera hiki cha hadithi.

##### 4.3.1.1 Njia ya Maandishi

Maandishi ni njia mojawapo inayotumika kuhifadhia kazi za Fasihi. Njia hii imeanza kutumika baada ya watu kujua kusoma na kuandika. Uhifadhi wa kazi za Fasihi kwa njia hii hupitia njia mbili kubwa. Hatua ya kwanza ni kubuni kisa au wazo; na hatua ya pili ni kuliweka wazo hilo katika maandishi.  Kwa kutumia njia hii ya maandishi kazi mbalimbali za Fasihi Simulizi zinaweza kuhifadhiwa. Kama vile hadithi, nyimbo, mashairi, ngonjera, majigambo, na hata vitendawili.

#### 4.3.1.1.1 Athari ya Uhifadhi wa Hadithi za Watoto kwa kutumia Njia ya Maandishi

Kazi yoyote ile ya Fasihi Simulizi, kikiwemo kipera cha hadithi za watoto, inapohifadhiwa kwa njia ya maandishi inaweza kudumu kwa muda mrefu. Hii inasaidia kwa vizazi vijavyo kupata fursa ya kuishuhudia kazi iliyohifadhiwa. Kwa mfano, hadithi hizo za watoto zinapohifadhiwa zinaweza kudumu kwa miaka mingi bila kuharibika. Hivyo, kutoa fursa kwa vizazi vijavyo kusoma hadithi mbalimbali za watoto ambazo zilikuwa zikisimuliwa na vizazi vilivyotangulia. Hii huvisaidia vizazi hivyo kupata fursa ya kuvuna hekima mbalimbali zilizokuwa zikitumika kipindi kilichotangulia.

Kazi iliyohifadhiwa inaweza kuifikia hadhira hata ile iliyoko mbali na msanii. Kwa kawaida hadithi za watoto huwasilishwa kwa njia ya masimulizi ya papo kwa papo baina na fanani na hadhira yake. Lakini hadithi hizo zinapohifadhiwa kwa njia ya maandishi huvuka mipaka na kuweza kufika sehemu mbalimbali. Kwa mfano hadithi za watoto wa Kenya zilizohifadhiwa kwa njia ya maandishi, zinaweza kusomwa hapa Tanzania na sehemu mbalimbali ulimwenguni.

Hadithi za watoto zilizohifadhiwa katika maandishi hazipotezi fani yake na maudhui yake, bali huendelea kuwa katika asili yake ya awali hadi msanii atakapoamua kuibadilisha. Iwapo itatokea msanii wa hadithi hizo kufariki basi fani na maudhui yaliyoandikwa hayabadiliki bali hubakia kama yalivyoandikwa.

Pamoja na faida mbalimbali ambazo hupatikana kwa kuzihifadhi hadithi za watoto, kupitia njia ya maandishi lakini njia hii mtafiti amebaini kwamba; inaweza kuleta hasara mbalimbali. Kwa mfano, mtafiti amebaini kwamba; kuzihifadhi hadithi za watoto katika njia ya maadhishi, husababisha njia hii itumike kwa ajili ya watu

wachache tu wanaojua kusoma na kuandika. Yaani kwa wale ambao hawajui kusoma na kuandika wanakosa fursa ya kuitumia njia hii katika kuzihifadhi hadithi zao. Hata kama hadithi hizo zina mafunzo mbalimbali ambayo yanaweza kuisaidia jamii kimaendeleo. Kwa hivyo, njia hii huitenga jamii ya wale wasiojua kusoma na kuandika, wakati ambapo Fasihi Simulizi ni mali ya jamii yote.

Hadithi za watoto zinapohifadhiwa katika maandishi huwa ni ghali sana. Ughali huo unatokana na msanii wa hadithi hizo kulazimika kununua vifaa vinavyohitajika katika maandishi ambavyo ni kalamu, karatasi, meza. Kwa hiyo, vifaa hivyo vya maandishi vinahitaji kugharamia jambo ambalo wengi hawana uwezo huo.

Hadithi za watoto zinapohifadhiwa katika maandishi uwasilishaji wake si hai. Hii inatokana na sababu kwamba, hakuna kuonana ana kwa ana kati ya hadhira na fanani. Hivyo, msomaji hawezi kupata vionjo vya msanii, na badala yake itambidi ajibunie yeye mwenyewe. Hali hii inaondosha ile ladha inayotarajiwa katika Fasihi Simulizi katika uwasilishaji wa vipera vyake kama vile hadithi za watoto. Inatarajiwa kwamba msanii anapotamba hadithi yake mbele ya hadhira yake, hutumia viungo mbalimbali vya mwili wake kama vile macho, kukunja uso kuashiria woga. Viungo hivyo vya mwili vinapotumika hurahisisha ufahamu kwa hadhira. Lakini hadithi hizo zinapohifadhiwa katika njia ya maandishi, vionjo mbalimbali ambavyo hurahisisha ufahamu kwa hadhira, huwa vinakosekana.

#### 4.3.1.2 Njia ya Vinasasauti

Vinasasauti ni miongoni mwa vifaa ambavyo hutumika katika kuhifadhi hadithi za watoto na vipera vyingine vya Fasihi Simulizi. Vifaa hivi vimeibuka kutokana na kuibuka na kukua kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia.  Miongoni mwa vyombo hivyo vya kisasa vinavyotumika kuhifadhi kazi za Fasihi Simulizi.ni kama vile CD,

DVD na hata vinasasauti. Vinasasauti ni njia mojawapo ya kuhifadhi hadithi za watoto iliyoendelea zaidi kuliko ile ya maandishi. Hii ni kwasababu kwa kutumia njia hii, walau unaweza kupata fursa ya kusikia sauti ya msanii na vionjo vyake.

#### 4.3.1.2.1 Athari za Uhifadhi wa Hadithi za Watoto katika Njia ya Vinasasauti

Kwa kutumia njia ya vinasasauti kazi ya msanii huweza kuwafikia watu hata walio mbali na alipo mtunzi wa kazi ya Fasihi husika. Baada ya msanii wa kazi ya Fasihi Simulizi kuwasilisha kazi yake na kurekodiwa, inaweza ikazagaa maeneo mbalimbali ya mijini na hata vijijini. Kwa mfano kupitia njia hii ya vinasasauti, utanzu wa hadithi za watoto umeweza kuhifadhiwa na kuweza kusikilizwa na watoto mbalimbali walioko maeneo tofauti ya hapa nchini na hata nje ya nchi yetu.

Hadithi za watoto zinapohifadhiwa katika vinasasauti kama vile tepurekoda au CD ubora wake huwa haupotei wala kuharibika endapo vifaa hivyo vitatunzwa vizuri .Kwa mfano, nyimbo za msanii maarufu wa nyimbo za taarabu Zanzibar Siti Bint Saad pamoja na kufariki kwake tarehe 08/07/1950, bado nyimbo hizo zimehifadhiwa kwa njia ya vinasasauti.Kwa mfano hadithi mbalimbali za watoto zilizokuwa zikirushwa hewani na Redio Tanzania Dar es Saalam (RTD) katika kipindi cha *Chechei Shangazi* bado zinaendelea kuwepo kutokana na kuhifadhiwa kwake kwenye vinasasauti.

Vile vile hadithi za watoto zinapohifadhiwa kwa kutumia vinasasauti, huwawezesha wasikilizaji kusikia sauti ya msimuliaji moja kwa moja. Kwa mfano, kwa kutumia tepurekoda unaweza kumsikia msimulizi wa hadithi jinsi anavyoitamba hadithi yake kwa watoto. Kupitia vinasasauti walau unaweza kusikia vionjo vya msanii ambavyo kwa namna fulani wakati anatamba hadithi kwa hadhira.

Kwa upande mwingine pamoja na kuwapo kwa faida mbalimbali zinazotokana na njia hii,njia hii huhusisha gharama. Hii ni kwasababu kuna kununua vinasasauti. Kwa kuwa watu wengi uchumi wao ni mdogo, inakuwa ni vigumu kumiliki vifaa hivyo. Hali inayosababisha wengi wao kukosa fursa ya kuhifadhi hadithi za watoto na vipera vingine vya Fasihi Simulizi.

Hadithi za watoto zilizohifadhiwa kwa njia ya vinasasauti uwasilishaji wake si hai. Hata kama unaweza ukasikia sauti ya fanani au wasikilizaji wanapopiga makofi wakati wa usimuliaji hawataweza kuonekana.

Madhara mengine ya kutumia vinasasauti katika kuhifadhia hadithi za watoto ni kwamba, kazi yoyote ya kifasihi inapohifadhiwa katika vinasasauti huwa ni mali ya fanani husika.Mtu mwingine haruhusiwi kuitumia bila kuruhusiwa na msanii ambaye aliiwasilisha kazi hiyo ya kifasihi.

#### 4.3.1.3 Njia ya Kompyuta

Kompyuta ni miongoni mwa vifaa kisasa vya sayansi na teknolojia. Vifaa hivi vina uwezo mkubwa wa kuhifadhi mambo mengi. Njia hii ya kuhifadhi hadithi za watoto katika nchi zetu za ulimwengu wa tatu, imeanza kutumika katika miaka ya hivi karibuni, baada ya watu kuanza kupata maendeleo ya sayansi na teknolojia na kujua namna ya kutumia kompyuta katika shughuli zao mbalimbali za kimaisha.

##### 4.3.1.3.1 Athari ya Uhifadhi wa Hadithi za Watoto kwa Kutumia Njia ya Kompyuta

Kuhifadhi hadithi za watoto katika kompyuta ni njia ya uhakika zaidi, kwa kuwa hadithi zilizohifadhiwa kwa kutumia njia hii huishi kwa muda mrefu na kuweza kusikilizwa wakati wowote zinapohitajika.

Vile vile kompyuta zinauwezo wa hali juu wa kuhifadhi hadithi nyingi. Kuhifadhi huku kunaweza kuwa msaada mkubwa katika kupata kumbukumbu ya aina za hadithi za watoto ambazo zilikuwa zinatambwa na vizazi vilivyotangulia.

Pamoja na ubora mkubwa wa kuhifadhi hadithi za watoto kwa kutumia njia hii. Lakini utafiti alibaini kwamba, zipo na kasoro pia. Hii ni kwa sababu katika kompyuta wasimuliaji au wasanii wanaohusika hawawasiliani na hadhira papo kwa papo. Hivyo hadhira hukosa kuuliza maswali katika vipengele vinavyotatiza wakati wa utambaji wa hadithi hizo.

Tatizo jingine ambalo hujitokeza kutokana na kuhifadhi hadithi za watoto katika kompyuta ni kwamba, ili kuhifadhi kazi ya Fasihi kwa kutumia njia hii ni sharti msanii awe anajua kutumia kompyuta. Hili linakuwa ni tatizo kubwa kwa kuwa ni watu wachache miongoni mwa jamii wenye uwezo wa kutumia kompyuta. Watu wengi hawana ujuzi wa kompyuta. Hivyo, kutumika kwa njia hii hasababisha hadithi nyingi kutohifadhiwa kutokana na kukosa ujuzi wa kutumia kifaa hicho.

Pia kompyuta ni miongoni mwa vifaa vya sayansi na teknolojia ambavyo gharama yake ni kubwa ili kuipata. Pia ni kifaa ambacho kinahitaji umeme wakati wa utumiaji. Hivyo katika maeneo ya vijijini, kwa mfano Wilaya ya Micheweni Zanzibar maeneo mengi hayajafikiwa na umeme. Hivyo kuhifadhi hadithi za watoto kwa kutumia njia hii inaweza kuwa na usumbufu mkubwa miongoni mwa watumiaji.

#### 4.3.1.4 Njia ya Kanda za Video

Kanda za video ni miongoni mwa njia za kisasa ambazo hutumika kuhifadhi hadithi za watoto. Uhifadhi wa hadithi za watoto kwa kutumia njia hii, utafiti umebaini kwamba ni ghali, Matumizi ya njia hii msanii atahitajika kununua, kanda ya video,

kumlipa mpiga picha na mzalishaji pia. Ndipo msimuliaji huyo aweze kuiwasilisha hadithi yake kwa hadhira iliyokusudiwa.Pia inahitajika hadhira husika imiliki vifaa vya kisasa vitavyowawezesha kuonesha kanda hizo za video ambazo ndani yake kuna hizo hadithi ambazo zimehifadhiwa. Mchakato huu unahitaji muda na gharama kubwa katika maandalizi yake.

#### 4.3.2.4.1 Athari ya Uhifadhi wa Hadithi kwa Kutumia Kanda za Video

Kwa kutumia njia hii, msimuliaji wa hadithi wakati anapotamba hadithi yake huonekana, hata vifaa anavyovitumia wakati wa utambaji. Pia navyo huonekana.
Njia hii husababisha sauti ya mtambaji na mwitikio wa hadhira wakati wa usimuliaji kusikika na pia kuonwa na hadhira. Kwa kiasi fulani huipa uhai kazi ya msanii mbele ya hadhira.

Kanda za video huweza kudumu kwa muda mrefu endapo itatunzwa katika njia nzuri. Njia hii hii inaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuchunguza aina ya hadithi na muundo wake ambao ulikuwa unatumiwa katika zama zilizotangulia.
Pamoja na faida mbalimbali zinazoweza kupatikana kutokana na uhifadhi wa hadithi za watoto kwa kwa kutumia njia hii, kwa upande mwingine kuna baadhi ya kasoro zinazoweza kujitokeza. Mathalani, watu wanaoweza kunufaika na njia hii wakati hadithi za watoto zinapohifadhiwa ni wachache, na wengi wao ni wale wenye uwezo wa kumiliki televisheni, ambao kimsingi hupatikana maeneo ya mijini na wachache tu wanapatikana vijijini.

Hadithi za watoto zinapohifadhiwa katika kanda za video, hadhira wanaweza kumwona msanii akisimulia hadithi yake, lakini hawawezi kuwasiliana naye ana kwa ana, hivyo hukosa fursa ya kuuliza maswali pindi wanapohitaji kufanya hivyo. Vile vile hadhira kukosa kushiriki katika matendo fulani wakati wa usimuliaji, pamoja na

kwamba, hii ni moja ya sifa ya Fasihi Simulizi kuishirikisha hadhira yake ipasavyo katika matendo.

## 4.4 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Fani na Maudhui ya Hadithi za Watoto

### 4.4.1 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Fani Kwenye Hadithi za Watoto

Fani ni mojawapo mwa kipengele muhimu katika kazi yoyote ile ya Fasihi Simulizi au Fasihi Andishi. Kwa mujibu wa Senkoro (2011) fani katika Fasihi ni ule ufundi wa kisanaa anaoutumia msanii katika kazi yake. Katika fani mambo mbalimbali huweza kuunda ama kubomoa kazi ya Fasihi hutegemea na vile ambavyo msanii anayatumia

Utafiti huu amebaini kwamba,hadithi nyingi wazitambazo watoto wa Wilaya ya Micheweni zimeathiriwa na uwapo maendeleo ya sayansi na teknolojia.Maendeleo makubwa yaliyofikiwa katika katika uwanja wa habari na mawasiliano,yametekeleza athari hizo kwa kiwango kikubwa. Wakati tukiwa uwandani katika harakati za kukusanya data juu ya athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto, yalifanyika mahojiano na Suleiman ambaye alisema kwamba:

> *Sayansi na teknolojia hususan teknolojia ya habari na mawasiliano kwa kupitia vyombo vyake kama vile, redio na televisheni vimebadilisha mfumo mzima wa utambwaji wa hadithi za watoto. Kupitia vyombo hivyo utambwaji wa hadithi umekuwa tofauti na ulivyozoeleka kabla.*[1]

Katika kusawiri hadithi za watoto, kwa kiasi kikubwa watoto wanaonekana wakiiga miundo ya hadithi zinazotambwa na kutolewa katika redio na televisheni. Watoto

[1] Mahojiano yaliyofanyika kati ya Suleiman Hamad Said na mtafiti January 24/2015 hapo skuli ya Tumbe Msingi.

huiga muundo wa hadithi, majina na wahusika kama wafanyavyo wasanii wanaoalikwa kwenye vyombo hivyo vya habari.

Kwa mfano hadithi ya ngano iliyosimuliwa na mwanafunzi wa Skuli ya Msingi Tumbe anayeitwa Bahati Kombo Massoud inaonesha hali hiyo kama ifuatavyo.

MFALME NDAMANGA NA BAHATI

| | |
|---|---|
| *Msimulizi* | *Wasikilizaji* |
| *Paukwa* | *Pakawa* |

*Hapo zamani za kale paliondokea Mfalme mmoja aliyekuwa akijulikana kwa jina la Ndamanga. Mfalme huyu alikuwa na watumishi wake ambao walikuwa wapo kwa ajili ya kusikiliza amri ya Mfalme wao. Siku moja Mfalme na watumishi wake walikwenda msituni kuwinda. Kwa bahati mbaya pete ya Mfalme ilimvuka bila mwenyewe kujua. Mfalme aligundua kwamba pete yake imempotea mara tu baada ya kufika kwake.*

*Baada ya kugundua kuwa pete imempotea, akaamrisha watumishi wake waende msituni wakaitafute, kwa bahati mbaya pamoja na kuitafuta kwa muda wa siku tatu lakini hawakuiona. Hivyo ikamlazimu Mfalme atoe amri kwa wananchi wake waingie msituni wakaitafute hiyo pete ya kifalme. Lakini pamoja na bidii kubwa waliyoifanya wananchi hao, lakini hawakujaaliwa kuikuta.*

*Bahati kijana mwenye umri wa miaka kumi na tatu. Siku ya tano tangu kupotea kwa pete, siku hiyo akaamua kwenda kuwinda ndege msituni. Punde tu mara baada ya kuingia msituni alikiona kitu kinang'ara kwa mbali kufika ilikuwa ni pete. Bahati akasema bila shaka hii ni ile pete ya Mfalme. Akaichukua kwa ajili ya kumpelekea Mfalme.*

*Kufika tu kwenye nyumba ya Mfalme alikutana na walinzi wake wakamwambia unasemaje? Bahati akasema nina pete ya Mfalme naomba muniruhusu kuingia ndani. Wakamwambia tupe tukamkabidhi, lakini Bahati akakataa kuwapa. Kwa hivyo wakamwambia kama atakwenda yeye mwenyewe, atakachopata wagawe pamoja. Bahati akakubali na akaingia ndani, ambako nako pia alikutana na walinzi wengine, nao pia wakawa na masharti kama wale wa mwanzo lakini Bahati akawakubalia wagawanye atakachokabidhiwa.*

*Kabla ya kumfika Mfalme alikutana na walinzi wa mwisho ambao nao pia walikuwa na masharti yale yale lakini bahati akakubali. Mwisho akaingia kwenye chumba cha Mfalme ambako alimkuta Mfalme akiwa na furaha sana, labda aliamini kwamba yule kijana atakuwa ameiokota hiyo pete. Na ikawa ni kweli na Mfalme akamuahidi kwamba atamkabidhi zawadi mbele ya wananchi wa nchi hiyo.*

*Siku ya pili harakati za sherehe zikaanza mapema, watu wakaanza kukusanyika kushuhudia tukio lenyewe la kijana Bahati kupewa zawadi maalum kutoka kwa Mfalme. Bahati akaambiwa na Mfalme*

*nataka tukagawanye mali yangu nusu kwa nusu. Kama nina ng'ombe elfu moja basi wewe nikupe mia tano. Au unasemaje Bahati? Bahati akasema nataka unipige bakora elfu mbili.Kusema hivyo watu wote waliohudhuria kwenye sherehe hiyo wakashangaa kwa aina ya zawadi aliyoitaka Bahati apatiwe.*

*Mfalme alimuuliza Bahati kwani umenikosea nini hata ukanambia nikupe aina hiyo ya zawadi?. Bahati akasema hujanikosea lolote ila siko peke yangu; nilitamani zawadi hiyo ya bakora tugawanye pamoja na wenzangu. Mfalme akauliza ni nani hao? Bahati akampa orodha yenye majina ya wale walinzi waliotaka wagawanye atakachopewa na Mfalme. Baada ya kuona majina ya walinzi wake kwenye orodha hiyo, alishangaa sana kwa kuona walinzi wake wanataka kuchukua rushwa pamoja na huduma wanazopatiwa. Hivyo Mfalme akatoa idhini kwamba Bahati hana makosa ila walinzi ndio ambao wamefanya makosa na wanastahiki kupata adhabu kama aliyoisema Bahati, ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia kama hiyo.*

*Baada ya hapo Bahati akapewa Ufalme kutokana na uaminifu wake alioufanya kwa kuwa mkweli dhidi matatizo yote yaliyomkumba, kwa kile kitendo cha kuwafichua wale waliodai rushwa.*

Hivyo katika hadithi hii kunaonekana kuwepo kwa majina kama vile Ndamanga na Bahati. Majina haya si aghalabu kupatikana katika hadithi ambazo zilikuwa zinatambwa Wilaya ya Micheweni. Jina zaidi ambalo lilikuwa likitumika katika masimulizi ya hadithi ni kama vile Makame wa Makame na majina mengine ambayo yaliambatana na majina ambayo yanapatikana katika Wilaya hii. Vile vile kujitokeza kwa majina kama vile rushwa huonyesha ni kwa namna gani athari hizi za sayansi na teknolojia zipo waziwazi katika hadithi za sasa za watoto. Hali kadhalika rushwa ni msamiati ambao umeibuka miaka ya hivi karibuni.

#### 4.4.1.1 Uteuzi wa Maneno katika Hadithi za Watoto

Katika hadithi nyingi za watoto uteuzi wa maneno ni ufundi anaoutumia mtambaji katika kuchagua maneno yanayotumiwa ndani ya hadithi yake. Hadithi nyingi wanazozitamba watoto zimeathiriwa na uteuzi wa maneno wayatumiayo wasanii mbalimbali ambao husawiri hadithi hizo kupitia vyombo vya habari na mawasiliano vilivyopo mijini na vijijini.

Katika Skuli ya Msingi ya Tumbe tuliwakuta watoto wakiwa katika kundi la watoto sita. Watoto hao walikuwa wanafunzi wa darasa la saba. Walikuwa wakitambiana hadithi, wanafunzi wengine walionekana wakishangilia kwa kuburudika kwa vionjo vinavyopatikana katika hadithi hizo. Kwa mfano hadithi iliyotambwa na Said Ismail Amour mwanafunzi wa darasala saba. Msimulizi wa hadithi alianza kwa kusema:

**KWANINI TEMBO ANA MKONGE MREFU?**

| *Msimuliaji* | *Wasikilizaji* |
|---|---|
| *Paukwa* | *Pakawa* |

*Hapo zamani za kale tembo hakuwa na mkonge mrefu kama anavyoonekana hivi sasa. Alikuwa na pua ya kawaida kama walivyo wanyama wengine. Lakini siku moja katika tembea tembea zake alipita karibu na ziwa kwa mbali akasikia sauti ya nyoka akihaha kwa maumivu makali, kwani alikuwa anateswa na mamba. Baada ya tembo kushuhudia hali ile, kutokana na urafiki waliokuwa nao tangu zamani alikata shauri akaona bora kujitoa muhanga ili aweze kumsaidia rafiki yake nyoka.*

*Muda si muda akaingia ndani ya ziwa kwa ajili ya kwenda kutoa msaada wake, ili aweze kumuokoa nyoka. Ghafla akajiona pua yake imeng'watwa na mamba. Katika harakati za kujinasua akaanza kujivuta kwa nyuma. Kwa hivyo kadri alivyotumia nguvu kujivuta kwa nyuma ndivyo pua yake ilivyozidi kurefuka, hadi ikawa inagusa mchanga kwenye ardhi. Baada ya kuona hivyo tembo alisikitika sana kwa aina ya umbo alilolipata bila ya kutegemea.*

*Baada ya muda mfupi akaijaribu pua yake ndefu kukamatia vitu akagunduwa kwamba, inafanyakazi vizuri sana. Kwani aliweza kuitumia kwa kujipatia chakula chake kwa urahisi. Kwa mfano kuangushia mipapai na hata baadhi ya miti. Ndipo alipogunduwa kwamba pua yake imekuwa na manufaa makubwa maishani mwake.*

Katika hadithi hii kuanzia mwanzo hadi mwisho, wanafunzi walionekana wakiwa na furaha sana. Hali hii ilitokana na uteuzi wa maneno uliofanyika ambao uliibua shauku na hamu ya kuipenda hadithi hiyo. Kwa hivyo, hali hii inadhihirisha kwamba kuwepo kwa vyombo vya sayansi na teknolojia, hususan katika sekta ya mawasiliano kumeleta mvuto kwa kiasi fulani katika kuzifanya hadithi hizo ziwe na mvuto wa kipekee. Hali hii kwa kiasi kikubwa imechangiwa kutokana na kuwepo kwa vifaa

vya mawasiliano kama vile redio na televisheni. Kutokana na kuwepo kwa wataalamu ambao hupata nafasi ya kutamba hadithi zao kupitia vyombo hivyo. Kunatoa fursa kwa watoto wa Wilaya hii ya Micheweni kuigiza mbinu hizo ikiwa ni pamoja na uteuzi wa maneno.

#### 4.4.1.2 Matumizi ya Lugha ya Matusi katika Hadithi za Watoto

Maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyoshika kasi katika nchi yetu, ambayo ndiyo yamesababisha kukua na kuenea kwa utandawazi yameathiri hadithi za watoto wa Wilaya ya Micheweni. Kutokana na uchunguzi uliofanywa katika utafiti huu, imebainika kwamba, sayansi na teknolojia imeathiri kwa kiasi kikubwa hadithi za watoto na watoto wenyewe. Katika kuchunguza tumeweza kubaini kwamba hadithi za watoto zimekuwa zikitumia lugha isiyo ya heshima, yaani lugha yenye matusi.
Hii imetokana na sayansi na teknolojia iliyoenea kutokana na kusikiliza hadithi za watoto kupitia vyombo vya habari  katika kila kona ya nchi yetu. Hivyo, watoto wanaposikia hadithi zilizoambatana na lugha yay a matusi zikitambwa katika redio ama kwenye televisheni, basi nao huona jambo la kawaida.Hatimaye nao huzitamba bila kujali matusi hayo.

Hadithi mbalimbali ambazo hurushwa hewani, aghalabu huwa na matusi ambayo kutokana na sayansi na teknolojia huonekana maneno ya kawaida katika jamiii. Lakini kwa hakika kutokana na uchunguzi katika utafiti huu tulioufanya, maneno hayo ya matusi yanaposikika kupitia vyombo vya habari huwaathiri watoto katika mienendo ya tabia zao. Ikiwa ni pamoja na kuigiza mila na desturi zisizoendana na utamaduni wa jamii zao.

#### 4.4.1.3 Uchanganyaji wa Lugha katika Hadithi za Watoto

Kutokana na mfumo wa kisasa katika utambaji wa hadithi za watoto, mara nyingi hadithi za watoto hurushwa hewani kupitia vyombo vya habari. Utafiti amegundua kuwa hadithi hizo huwa na mchanganyiko wa lugha tofauti. Kwa mfano, mtafiti amebaini kwamba, ndani ya hadithi moja ambayo husawiriwa kwa lugha ya Kiswahili huweza kujitokeza pia lugha ya Kiingereza. Mchangiko huu unapotumika katika hadithi hizo huipoteza ladha na uasili wa hadithi katika jamii ya Waswahili, Ikiwamo jamii ya watu wa Wilaya ya Micheweni. Hivyo, lengo na makusudio katika hadithi hizo za watoto hupotea.Mathalani iwapo zilikusudiwa kuelimisha na kujenga maadili miongoni mwa jamii husika. Kwa mfano, wakati tunaendelea na ukusanyaji wa data za utafifi huu. Katika nyumba ya Bwana Khamis Dawa Khatib, tulimshuhudia mtoto wake Bijuma Khamis Dawa wa darasa la Saba, akiwa amechanganyikiwa wakati akisikiliza na kuangalia hadithi katika kituo cha televisheni cha ITV katika kipindi cha watoto cha " Hadithi Club''. Kipindi hicho kilioneshwa tarehe 07/03/2015 siku ya Jumamosi asubuhi. Hii ilitokana na mtambaji wa hadithi kupitia kipindi hicho kuchanganya lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

#### 4.4.1.4 Matumizi ya Mbinu ya Ucheshi katika Hadithi za Watoto

Ucheshi ni mbinu wanazozitumia watambaji wa hadithi katika kuchagua maneno ambayo yanawachekesha wasikilizaji na watazamaji wa video na televisheni. Hadithi mbalimbali hutumia mbinu hii kwa lengo la kuvuta makini kwa hadhira pindi zinapotambwa.

#### 4.4.1.5 Utungaji Katika Hadithi za Watoto

Tabia na mwenendo wa watoto katika kutunga na kuwasilisha hadithi zao za kitoto, kwa kiwango kikubwa umeathiriwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Katika uchunguzi wetu tulioufanya, utafiti umebaini kwamba, kuwepo kwa vyombo vingi vya habari,kupitia matangazo na vipindi mbalimbali umeathiri utungaji wa hadithi za watoto. Katika eneo tulilofanyia utafiti tuliweza kupata idadi kubwa ya vituo vya redio na televisheni, wakazi wengi wamefunga ving'amuzi katika majumba yao, hususan ving'amuzi vya Azam TV. Hivyo, kupitia king'amuzi hicho, watazamaji hupata fursa ya kuangalia televisheni mbalimbali kama vile TBC 1, ITV, Channel Ten, Clouds TV, ZBC na hata East African Television.

Vituo hivyo vya habari ingawaje havipo maeneo haya ya Micheweni, lakini vinasikilizwa na kuangaliwa kwa kiasi kikubwa na wakaazi wa maeneo hayo. Pamoja na vituo hivyo vya televisheni vipo pia vituo vya redio ambavyo husikika vyema na baadhi vipo katika maeneo haya ya Micheweni. Kwa mfano, Redio Jamii kutoka Micheweni. Pamoja na upya wa redio hii lakini imejizolea wasikilizaji wengi wa Wilaya ya Micheweni na viunga vyake. Wakati mtafiti alipofanya mahojiano na mkuu wa redio hiyo Ndugu Ali Massoud Kombo alisema kwamba:

> *"Uanzishwaji wa redio jamii katika Wilaya ya Micheweni kumetoa ari na hamasa kwa jamii ya Wilaya hiyo. Kwani ni muda mfupi tangu kuanzishwa kwake lakini vipindi vyake vimejizolea umaarufu mkubwa, hususan vipindi vya watoto, kama vile vipindi vya masimulizi ya hadithi za watoto[2]''.*

Redio nyingine zinazosikika katika maeneo haya ni pamoja na ZBC Redio, Zenj FM, Chuchu FM. TBC Redio, Redio One Sterio na nyingi nyinginezo. Kupitia

[2] Mahojiano yaliyofanyika kati ya mtafiti na mkurugenzi wa Redio Jamii Micheweni Pemba February 05/2015

vyombo hivyo vya habari watoto hupata fursa ya kusikiliza na kuangalia jinsi hadithi za watoto zinavyotambwa na watoto wenziwao walio maeneo mengine ya Tanzania. Hivyo, hali hii imeathiri mfumo mzima wa utungaji wa hadithi za watoto wa Wilaya ya Micheweni. Kwani watoto hujaribu kufuata mfumo mpya wa usawiri unaofanywa na watambaji wa hadithi katika vituo hivyo vya habari.

### 4.4.2 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Maudhui ya Hadithi za Watoto

Utafiti huu umebaini kwamba, sayansi na teknolojia imeathiri maudhui katika hadithi za watoto, hususan maendeleo makubwa ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

Katika kuzichunguza hadithi hizo, tumeweza kubaini dhamira mbalimbali ambazo zimejitokeza katika hadithi hizo.

#### 4.4.2.1 Kuwaburudisha Watoto

Hadithi nyingi wazisimuliazo masuala ya watoto, utafiti umegundua kwamba zinabeba dhima ya kuwaburudisha watoto hao. Kwa mfano katika hadithi ifuatayo:

**BINADAMU HANA WEMA**

***Hadithi, Hadithi...........Hadithi njoooo utamu kolea***

*Hapo zamani za kale palikuwa na kijana mmoja aliyekuwa akijulikana kwa jina la Sande na alikuwa anaishi pamoja na mama yake.*

*Siku moja Sande akamwambia mama yake kuwa anataka kwenda kuishi mbali akiwa peke yake. Lakini mama yake akamwambia kwa nini mwanangu unataka kuishi mbali, na kuniacha mimi nibaki peke yangu? Sande akamwambia mama yake kuwa anataka akakae mbali na watu. Sande akaamua kuondoka akamwacha mama yake, mkononi akiwa amebeba panga na kamba.*

*Akatembea umbali mrefu mpaka akafika kwenye msitu mkubwa sana. Kwenye huo msitu akaona shimo kubwa sana. Alipoangalia ndani ya lile shimo akamuona binadamu, simba, nyoka na nyani.*

*Wale viumbe wakamlilia sana Sande awatoe mle shimoni na hatimaye Sande akapatwa na huruma akachukua kamba akarusha shimoni na kuanza kuwaokoa.*

*Aliporusha kamba mara ya kwanza, nyani akaidaka akamvuta akatoka. Nyani alipofika juu akamwambia Sande," Nakushukuru sana kwa kuniokoa umeyanusuru maisha yangu ila nakuomba umuokoe simba, usimuokoe binadamu kwa sababu binadamu hana*

*wema. Akarusha kamba kwa mara ya pili akadaka simba akamvuta akatoka, alipofika juu akamwambia Sande "Nakushukuru sana kwa kuniokoa umeyanusuru maisha yangu ila nakuomba umuokoe nyoka, binadamu muache kwa kuwa binadamu hana wema."*

*Aliporusha mara ya tatu akadaka nyoka, akamvuta mpaka juu akatoka, alipofika juu akamwambia Sande "Nakushukuru sana kwa kuniokoa, umeyanusuru maisha yangu lakini nakuomba ondoka zako, usimtoe binadamu kwa sababu binadamu hana wema."*

*Sande akamwambia sawa nimekusikia, yule binadamu kule chini kwenye shimo alilia sana kwa kumuomba msaada Sande tena kwa maneno mengi. Yaani wewe umeamua kuwaokoa wanyama unaniacha mimi binadamu mwenzako na maneno mengine kadhaa.*

*Sande kwa huruma akarusha kamba kwenye shimo, binadamu akashika kamba akavutwa mpaka juu. Akamshukuru sana siku ile kwa kuokoa maisha yake.*

*Sande akaamua kujenga nyumba yake kwenye msitu ule, huku akiishi peke yake. Mara nyingi nyani alikuwa akienda kumtembelea Sande pale nyumbani kwake huku akiwa amebeba mihogo, mahindi, ndizi na vyakula vingi ambavyo aliweza kuiba kwenye mashamba ya watu, aliyafanya haya ili rafiki yake asipate njaa.Simba naye alikuwa akienda kumtembelea mara kwa mara na tena kumuwekea ulinzi ili asiweze kudhuriwa na wanyama wengine. Simba alikuwa anamuonea huruma sana rafiki yake huyo kwa kuishi kwa upweke pale msituni. Siku moja akapita kwenye mitaa akamkuta binti wa mfalme akamdaka akampeleka mpaka kwa rafiki yake.*

*Sande akamwambia; "rafiki yangu nimekuona upo mpweke sana hapa nyumbani kwako hakuna mtu wa kukusaidia kazi kama vile kupika, sasa nimekuletea huyu msichana uishi naye." Sande akamshukuru sana simba kwa kumjali.*

*Huko nyuma lamgambo likalia kwa Mfalme, wakatangaza kwamba binti wa mfalme amepotea hivyo anatakiwa atafutwe haraka iwezekanavyo.*

Katika kuchunguza hadithi hii, wakati wa utambaji watoto walionekana kuburudika na hadithi hiyo, huku wakipokea kile ambacho mtambaji alikikusudia kifike katika jamii yake. Kwa vile msimuliaji alikuwa pamoja na wasikilizaji, basi dhamira za hadithi hiyo zilifika haraka sana. Hali hii ilijidhihirisha pale baada ya kumaliza kusimuliwa hadithi, mtafiti akajaribu kuwauliza wanafunzi maswali kama kuna mtu ameifahamu hadithi vizuri. Kila mmoja alitaka apate fursa ya kusema chochote pamoja na kwamba hadithi ilikuwa haijafika mwisho.

#### 4.4.2.2. Kuelimisha Jamii

Kuelimisha ni mojawapo ya dhamira katika hadithi za watoto. Siyo kwamba watoto wanasawiriwa hadithi kwa ajili ya kuelimisha peke yake. Baada ya kusawiri hadithi hiyo hapo chini tuliweza kuwauliza watoto wa Skuli ya Msingi Michewenini kuwa kwanini wameamuwa kuisawiri hadithi hii? Wakadai kwamba wameitamba kama sehemu ya kuwaelimisha na kuwaonya watoto juu ya suala la umuhimu wa kuthamini wakati. Hadithi ni hii ifuatayo.

KILICHOMPONZA NYOKA AKAKOSA MIGUU

*Paukwa* *Pakawa*

*Hapo zamani za kale walipanga wanyama wote wakusanyike kwa ajili ya kufanya mgawanyo wa miguu. Ili waweze kutembea hata kwa masafa ya mbali pasi na usumbufu wowote. Kwa hivyo viongozi wa wanyama wakapanga wakusanyike baada ya siku tatu. Muda wa wanyama wote kuhudhuria ni saa mbili kamili asubuhi.*

*Kufika saa mbili kamili asubuhi wanyama wote walikuwa wameshafika, kwa ajili ya kuanza kuchukua miguu yao isipokuwa nyoka alikuwa bado hajawasili. Nyoka kwa uvivu wake alichelewa kuamka, mara baada ya kuamka akajishughulisha huku na huku, hata alipofika kwenye mgawanyo wa miguu walikuwa wanyama wote wameshatawanyika.*

*Jongoo ambaye alikuwa ndiye aliyekuwa akigawanya miguu, Kwa hivyo jongoo baada ya kuona hadi saa nne hakuna mnyama aliyetokea akaamuwa miguu yote iliyobakia ajibandike yeye. Hata alipowasili nyoka wanyama wote wameshatawanyika na kila mmoja ameshapata mgawanyo wake. Nyoka kuona hali hii alisiktika sana lakini masikitiko yake yangesaidia kitu gani? Kwa hivyo hadi leo nyoka amekosa miguu.*

Baada ya mwanafunzi kusimulia hadithi hii, wanafunzi wenzao ambao walikuwa wakisikiliza waliweza kutoa michango mbalimbali. Pia walikiri kwamba, hadithi hiyo imeweza kuwaelimisha kuhusiana na umuhimu wa kuchunga wakati. Huku wakitoa mifano ya wanafunzi wenye tabia ya kuchelewa skuli, walisema kwamba, aghalabu watoto wenye tabia hiyo ya kuchelewa skuli huwakuta kama yaliyomkuta nyoka baada ya kuchelewa na hatimaye kukosa miguu.

### 4.5 Mchango wa Sayansi na Teknolojia katika Maendeleo ya Hadithi za Watoto

Tunapozungumza juu ya maendeleo ya sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto, tunamaanisha mchango ambao umechangiwa na hiyo sayansi na teknolojia katika kukuza na kuimarisha kipera cha hadithi za watoto. Sayansi na teknolojia ni vitu viwili vinavyokwenda sambamba pasipo kuachana.Teknolojia ni maendeleo ya kisayansi katika hatua ya mwisho ambayo inaonekana. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa, sayansi na teknolojia vyote kwa pamoja vimekuwa ni muhimili mkubwa katika maendeleo ya hadithi za watoto. Wakati tunapoijadili sayansi hali inaonesha kwamba nchi zote ambazo zimepata maendeleo, maendeleo hayo yalitokana na sayansi na teknolojia. Hali hii inatokana na kwamba, sayansi na teknolojia inatumika katika maisha yetu ya kila siku. Kwa mfano sayansi katika ujenzi, mawasiliano, nishati ya umeme na vile vile tunaitumia teknolojia katika maisha yetu ya kila siku. Kama vile kuwasiliana, kutembeleana na mambo mengi yanayofanana na hayo.

Tunapozungumzia juu ya maendeleo ya hadithi za watoto kutokana na sayansi na teknolojia, tunamaanisha jinsi ambavyo sayansi na teknolojia ilivyoweza kutoa mchango katika hadithi za watoto. Hususan katika suala zima la kuzihifadhi, kuziwasilisha, kuikosoa jamii na kutoa fursa kwa hadhira inayoangalia ama kusikiliza ambayo iko mbali kuweza kupata fursa ya kuchangia mada. Mambo yote haya hufanyika wakati masimulizi ya hadithi katika vipindi vya hadithi za watoto vinavyoendelea kufanyika katika vyombo vya habari husika.

Mambo yote hayo yanawezekana kupitia vyombo ya kisayansi na teknolojia, kama vile televisheni, kompyuta, mikanda ya video, mikanda ya CD, DVD, VCD, barua

pepe, simu za mkononi na hata maandishi. Vifaa hivi vya sayansi na teknolojia kwa pamoja vimechangia maendeleo makubwa ya hadithi za watoto.

### 4.5.1 Mchango wa Sayansi na Teknolojia Kupitia Vyombo vya Habari

Kutokana na maendeleo makubwa yaliyojikita katika nyanja mbalimbali za sayansi na teknolojia, hususan katika nyombo vya habari. Utafiti umebaini kwamba, maendeleo hay kwa kiasi kikubwa yamechochea mabadiliko mbalimbali vipera mbalimbali vya Fasihi Simulizi, kikiwemo kipera cha hadithi za watoto. Hadithi za watoto kwa sasa kwa kiasi kikubwa zinasimuliwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari.Hivyo, kwa sasa si jambo la ajabu kuona watoto wamejipanga kwenye chombo kimojawapo cha habari kama vile redio ama televisheni wamekaa wanasikiliza au kuangalia hadithi zinavyosimuliwa. Vyombo vya habari kwa muda huu vimekuwa chumio la watoto kujipatia tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi kikiwamo kipera cha hadithi za ngano. Kupitwa kwa mfumo wa utambaji wa hadithi unaomshirikisha babu au bibi na wajukuu, kumetoa fursa kubwa kwa vyombo hivyo kuhusika katika usimuliaji wa hadithi za watoto.

Mlacha (2004) anasema kwamba, vyombo vya habari vina uhusiano mkubwa sana na Fasihi, hasa kwa kuwa vyote vimetawaliwa na lugha ambayo ndiyo njia muhimu ya mawasiliano baina ya binadamu. Kwa maneno mengine, mtu anaweza kusema kuwa vyombo vya habari na Fasihi ni vyombo vinavyotumiwa na binadamu kwa mawasiliano. Pia, vyombo vya habari hutumiwa kama vyombo vya kuwasilisha Fasihi kwa binadamu. Uchunguzi uliofanyika kutokana na utafiti huu tumebani kuwa, kuna vipindi mbalimbali vya watoto vinavyohusu hadithi za watoto, vitendawili na hata mafumbo. Vipindi hivi hurushwa hewani kwa kutumia vyombo vya habari kama vile redio ama televisheni. Naye Parry (1967: 29) anasisitiza kuwa

ni ndani ya mfumo mzima wa mawasiliano ambamo kuelimishana kunajitokeza na ndilo jambo linalotawala. Hapa mwandishi huyu anaona kwamba, kutumika kwa vyombo vya habari katika kuwasilisha tanzu za Fasihi Simulizi kama vile hadithi za watoto ni sehemu mojawapo ya kuifikishia elimu jamii inayohusika, kama vile kujenga maadili.

### 4.5.2 Mchango wa Sayansi na Teknolojia katika Uwasilishaji wa Hadithi za Watoto

Vile vile mtafiti ameonesha kuwa, sayansi na teknolojia imetoa mchango mkubwa katika kuziwasilisha hadithi za watoto kwa watu wengi walio mbali na fanani. Matumizi ya njia za kisasa wakati wa uwasilishaji wa hadithi za watoto, hayahitajiki uwapo wa ana kwa ana fanani na hadhira. Hadhira inaweza ikawapo, lakini fanani asiwepo na nafasi yake ikachukuliwa na utaalamu wa kisasa unaotokana na sayansi na teknolojia. Hili hufanyika kupitia mikanda ya video, CD, kompyuta, barua pepe, simu za mkononi, redio, televisheni na njia nyingine kadhaa. Kwa kutumia njia hizi sayansi na teknolojia inatumika sana katika uwasilishaji wa hadithi za watoto na ushirikishwaji wa hadhira.

### 4.5.3 Mchango wa Sayansi na Teknolojia Katika Uhifadhi wa Hadithi za Watoto

Sayansi na teknolojia imekuwa nyenzo muhimu katika kuzihifadhi tanzu za Fasihi Simulizi, kikiwamo kipera cha hadithi za watoto. Utafiti umebaini kwamba, kuhifadhiwa kwa hadithi hizi kumesaidia sana kuhifadhi kumbukumbu za hadithi hizo. Ili vizazi vingine viweze kurithi hadithi hizo. Katika kufanya hivi sayansi na teknolojia hutumia vyombo vyake vya kisasa kama vile mikanda ya video, CD, DVD, tepurekoda, vinyonyi, na hata kompyuta ambayo ina uwezo mkubwa wa

kuzihifadhi hadithi nyingi na kuweza kudumu kwa muda mrefu. Kwa mfano, tulibaini kwamba hadi leo hii bado hadithi nyingi za watoto, zilizokuwa zikisimuliwa katika kipindi kilichokuwa kikirushwa hewani na Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) cha Mama na Mwana. Mtangazaji wa kipindi hicho alikuwa anaitwa Mama Betty Mkwasa. Mama huyu alikuwa maarufu katika usimuliaji wa hadithi nzuri ambazo zilivuta masikio ya wasikilizaji wengi. Mojawapo ya hadithi hizo ni hii ifuatayo licha ya kupita miaka mingi lakini bado kumbukumbu zake zimo katika mtandao;

**MFALME KIGONGO**

*Paukwa Pakawa*

*Hapo zamani za kale kulikuwa na Mfalme ambaye alikuwa akiitwa Mfalme Kigongo. Mfalme huyu alikuwa na mtoto wake wa kike ambaye alikuwa akiitwa Tunda. Tunda alitokea kumpenda Kiyela na akamuahidi ya kwamba siku moja watafunga ndoa. Ile habari hiyo alikuwa hajapata kumueleza baba yake juu ya jambo hilo.*

*Mfalme Kigongo akaipata habari kwamba mwanawe ametokea kumpenda Kiyela ambaye alikuwa anatoka katika familia ya kimaskini. Jambo hilo lilimuhuzunisha Mfalme na akaamrisha askari wake wamtafute Kiyela popote alipo na wamlete mbele yake.*

*Habari hii ya kutafutwa na askari wa kifalme ikamfikia Kiyela, na hapo akaanza kujificha kwenye msitu mnene na kulala kwenye mapango yenye kiza sana. Baada ya kukaa katika msitu kwa muda mrefu akafikiria kuhusu hali ya mama yake. Hii ilitokana na kwamba hakukuwa na mtu mwengine wa kumshughulikia mama yake. Hali hii ikamfanya Kiyela akose utulivu katika msitu, na akaamua atoke kwenye msitu na aje kumuangalia mama yake.*

*Kiyela kabla ya kuingia mjini alikutana na askari wa Mfalme Kigongo na wakamtaka asimame. Lakini kwa hofu akaamua kukimbia, walinzi wa Mfalme Kigongo mmoja wao akaamuwa kumrushia mkuki. Kwa bahati mbaya mkuki huo ukamchoma mkongoni. Na kwa sababu ya sumu kali ya mkuki huo, Kiyela akaanguka chini na ghafla akapoteza maisha. Kuanguka na kufa kwa Kiyela liliwapa hofu walinzi wa Mfalme kwa vile walitakikana wampeleke mbele yake akiwa hai ili apate kumuhoji.*

*Baada muda walinzi wa Mfalme wakaingia ndani na kumueleza Mfalme juu ya mkasa huo, ya kwamba kwa bahati mbaya wakati wakiwa katika harakati za kumkamata Kiyela alikimbia na wakamlenga mkuki na kwa bahati mbaya akafariki dunia. Mfalme Kigongo akisema si tatizo kuuliwa na akasema kwamba asizikwe na*

*maiti yake iwekwe juani ili iliwe na ndege na wanyama wengine. Na yeyote atayehuzunika juu ya kifo chake basi akamatwe na auliwe.*
*Muda si muda walinzi wa mfalme karibu na maiti ya Kiyela, wakamuona mwanamke analia. Kukaribia wakamuona ni Tunda mtoto wa mfalme akawa analia huku akiirushia mchanga maiti ya Kiyela kama ishara ya kumzika. Hapo hapo wakamchukua Tunda na kumpeleka mbele ya mfalme. Mfalme Kigongo hakuamini macho yake kwa kumuona mwanawe analetwa mbele yake.*
*Walinzi wa mfalme wakaeleza mkasa mzima kama ulivyotokea.Mfalme Kigongo akamwambia mwanawe kweli umemlilia Kiyela? Tunda kwa huzuni akasema ndiyo baba kwa sababu Kiyela alikuwa ni rafiki yangu na matarajio yetu ilikuwa ni kufunga ndoa baadaye. Mfalme akasema ni aibu kwetu ndani ya familia ya kifalme mtoto wetu kuolewa na fukara. Tunda akesema baba! Kiyela alikuwa anafanya kazi kwa bidii.Mfalme akasema hata hivyo isingewezekana wewe kuolewa na mtoto huyo wa kimaskini na kuitia aibu familia ya kifalme.*
*Mfalme Kigongo akaamrisha mwanawe auliwe kwa kutumia shoka. Jambo hili lilimsikitisha sana malkia mke wa mfalme Kigongo, kwa na ukatili wa mume wake. Lakini hilo hata halikumfanya mfalme abatilishe maamuzi yake ya kuuliwa kwa Tunda. Na Tunda akapigwa shoka na kupoteza maisha hapo hapo.*

Hadithi hii ni miongoni mwa hadithi nyingi za mama na mwana ambazo zilikuwa zinasimuliwa kupitia Redio Tanzania Dar es Salaam. Kumbukumbu zote hizi zimekuwepo kutokana na kuimarika kwa vifaa vya habari na mawasiliano, bado hadithi hizi zinapatikana katika mtandao. Hivyo kutoa fursa kwa wasomaji wanapotaka kujikumbusha hadithi hizo kupata nafasi hiyo ya kusoma bila shida yoyote.

### 4.5.4 Mchango wa Sayansi na Teknolojia katika Uchangiaji wa Mada

Katika uchunguzi ulioufanyika utafiti umebaini kwamba, sayansi na teknolojia imekuwa na mchango mkubwa kwa hadhira katika kuchangia mada. Hapa sayansi na teknolojia hutumika kama kiunganishi kati ya fanani na hadhira yake kwa pamoja. Mfano mzuri kuhusiana na hili ni matumizi makubwa ya setilaiti. Aidha setilaiti yaweza kutumika kuziwasilisha kazi za Fasihi Simulizi kwa hadhira iliyombali na fanani. Kwa mfano, tunaona kupitia katika vyombo vya habari kama vile redio na

televisheni, hadhira inaweza kuchangia mada ikiwa ni pamoja na kupata fursa ya kutamba hadithi wakati wa kipindi cha usimuliaji wa hadithi za watoto kinapoendelea.

### 4.5.5 Mchango wa Sayansi na Teknolojia katika Kuikosoa Jamii

Sayansi na teknolojia imekuwa ni muhimili mkubwa katika kuikosoa jamii kupitia vyombo vyake mbalimbali vya kisasa. Kwa mfano kupitia redio na televisheni, kupitia hadithi mbalimbali za watoto husimuliwa na kwa kiasi kikubwa huikosoa jamii, pale ambapo jamii imekosea au kufanya mambo kinyume na maadili ya jamii husika. Hivyo, jamii inaposikiliza hadithi hizi kupitia vyombo hivi vya kisayansi hupata mafunzo mbalimbali. Kwa mfano, hadithi za watoto zinazorushwa hewani na vyombo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi yetu. Kwa kuwa hadithi hizi huonesha matatizo mbalimbali, yanayofanana basi hadithi hizo zinaweza zikatoa mafunzo muhimu kwa jamii mbalimbali ulimwenguni.

Kwa upande mwingine sayansi na teknolojia imeigeuza dunia kuwa ndogo na kuwa ndogo zaidi kila kukicha. Udogo huu wa dunia ni dhahiri kwamba, umetokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia hususan katika nyanja ya habari na mawasiliano ambapo mawasiliano yamekuwa ya kisasa zaidi.

Sayansi na teknolojia ndiyo iliyozaa dhana mpya ya Fasihi Simulizi ya leo iliyochukua nafasi ya dhana ya Fasihi Simulizi ya zamani. Kwa mtazamo wa juu juu unaotokana na baadhi ya watu, twaweza kusema kuwa ni Fasihi ambayo inaonekana kwenda na wakati zaidi.

Vile vile kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, wataalamu wengi wa Intaneti wamefungua tovuti mama kwa nia ya kuharakisha mawasiliano. Hali hii

imechochea watoto wengi kupata fursa ya kujifunza hadithi nyingine kutoka kwa watoto wengine, wa maeneo mengine. Hili linawezekana kwa kutumia vyombo vya kisasa kama vile redio, televisheni, mitandao ya Intaneti, mitambo ya setilaiti, ving'amuzi na vyombo vingine mbalimbali vya habari. Vyombo hivi vimesaidia sana kwa watoto kukusanya hadithi nyingi ambazo zinasaidia kuwachonga kimaadili, ili kuenda sambamba na matakwa ya jamii husika.

Pia, kwa kuzingatia maendeleo yanayotokana na sayansi na teknolojia, hususan katika nyanja ya habari na mawasiliano. Na kwa kuzingatia ukweli kwamba, dunia ni mahala pa ujirani. Kuna aina fulani ya kukaribina kwa watu kupitia njia hizo zinazotokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Hili limewezesha utanzu wa hadithi za watoto uweze kusikilizwa katika redio na kuoneshwa kwenye televisheni.

Sayansi na teknolojia imechangia sana maendeleo ya hadithi za watoto. Kwa mfano katika Tanzania ya leo tuna vituo vingi vya redio na televisheni ambavyo hurusha matangazo yake sehemu mbalimbali hapa nchini. Kwa kupitia vituo hivi hadithi za watoto zinazosimuliwa zimekuwa zikiwafikia watoto wengi hapa nchini. Katika vituo hivyo vya redio na televisheni vya hapa nchini vipindi mbalimbali vya watoto husikika kama vile hadithi, vitendawili, methali na hata mafumbo husimuliwa, Na huwahusisha washiriki waliopo hapo studio na watu wengine wanaoyapata matangazo hayo katika sehemu walizopo.

Kituo cha televisheni cha ITV kuna kipindi cha watoto kila siku ya Jumamosi saa tatu asubuhi, kipindi cha "Hadithi Club''. Katika kipindi hicho, watoto mbalimbali kutoka maeneo tofauti hualikwa kwenda kusikiliza hadithi zinazosimuliwa na Mama Terry ambaye pia ni muigizaji maarufu filamu hapa nchini. Kutokana na umaarufu alionao msimuliaji huyu, watu wengi wanapenda kukifuatilia kipindi hicho na

kukiangalia ili kujua ni aina gani ya hadithi ambazo amekusudia kuzisimulia kwa siku hiyo.

Vile vile katika televisheni hiyo hiyo ya ITV kila siku ya Jumapili saa tisa alasiri kuna kipindi cha mgongano wa mawazo ambapo Fasihi ya Kiswahili ya Mtanzania husimuliwa hasa Fasihi ya vitabu. Hapo huendeshwa mjadala kuhusu mada mbalimbali za Fasihi Simulizi na vipera vyake ikiwa ni pamoja na kipera cha hadithi za watoto. Vipindi hivyo huendeshwa na wanafunzi chini ya usimamizi wa walimu wao.

Kwa upande wa shirika la habari la Zanzibar kupitia vyombo vyake vya habari. Yaani televisheni Zanzibar (ZBC) kila siku jioni huwa wanaendesha kipindi cha watoto,ambapo watoto hujumuika pamoja katika studio kuimba, kutoa hadithi, chemsha bongo na vipindi vyingine vingi. Kipindi hiki hutoa fursa kwa watazamaji walio wengi wa mijini na vijijini, kwa vile katika maeneo hayo matangazo hufika, Wanajamii hupenda kukikiangalia kipindi hicho na kushuhudia aina mbalimbali za hudithi za watoto zinazosimuliwa kupitia kipindi hicho.

Kwa upande wa redio vipo vipindi kadhaa ambavyo hurushwa hewani kupitia redio hizo. Kwa mfano katika Redio One Stereo kuna vipindi mbalimbali vya watoto ambavyo hurushwa hewani kupitia redio hiyo.Vipindi hivyo hurushwa hewani kila siku ya Jumamosi asubuhi, na baadhi ya vipindi hivyo vimedumu kwa muda mrefu vikiwa vinaendeshwa na mtangazaji wa siku nyingi wa redio hapa nchini ajulikanaye kwa jina Julius Nyaisanga, ambaye katika kipindi cha watoto hujulikana kama, Babu Kimanzichana. Kimanzichana ni moja kati ya sehemu maarufu katika mkoa wa Pwani ambayo ipo kijijini. Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD), kwa sasa inaitwa TBC Taifa, ambapo redio hiyo inaonekana haiko nyuma kuhusu hilo nao pia

kama zilivyo redio na televisheni nyingine. TBC Taifa wana vipindi kama vile cheichei shangazi na mama na mwana ambapo hadithi za watoto mbalimbali zenye semi, mafumbo, methali na hata vitendawili husimuliwa

## 4.6 Mwamko wa Jamii ya Wilaya ya Micheweni Kuhusiana na Athari za Sayansi na Teknolojia Juu ya Hadithi za Watoto

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) mwamko ni tendo la mtu kulishughulikia kikamilifu jambo maalum. Pia tunaweza kusema kwamba mwamko ni ile hali ya ufahamu juu ya jambo fulani. Utafiti umebaini kuwa jamii ya watu wa Wilaya ya Micheweni kwa kiasi fulani, wanaonekana kuwa na mwamko mkubwa juu ya athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto.

### 4.6.1 Mwamko wa Jamii katika Ununuzi wa Vifaa vya Sayansi na Teknolojia

Suala la mwamko katika ununuzi wa vifaa vya habari na mawasiliano, ni jambo ambalo linaonekana kuimarika kwa kiasi kikubwa miongoni mwa jamii ya watu wa Wilaya ya Micheweni. Utafiti umegundua kwamba, watu wengi hupenda kununua vifaa hivyo ili wapate fursa ya kufuatilia habari zinazoendelea kila kipembe cha dunia, ndani na nje ya nchi yetu. Wakati watu wazima wakiwa na utashi wa habari kupitia vyombo hivyo.Utafiti umegundua kuwa, kwa upande wa watoto huitumia fursa hiyo kufuatilia vipindi vya watoto kupitia vyombo hivyo. Ikiwa ni pamoja na kusikiliza na kuangalia hadithi za watoto, ambazo hurushwa hewani na vyombo vya habari mbalimbali vya hapa Tanzania. Mtoto Omar Hamad Khalfan mwanafunzi wa Skuli ya Msingi Wingwi, anayesoma darasa la Sita mwenye umri wa miaka kumi na tatu alieleza kuwa.

> *"Wakati baba anapokuwa yuko kazini, hupata fursa ya kuangalia televisheni mbalimbali mimi na wadogo zangu ambazo huonesha katuni na baadhi yao huonesha michezo ya*

*watoto ikiwa ni pamoja na nyimbo, hadithi na hata vitendawili.''*

### 4.6.2 Mwamko wa Jamii katika Matumizi ya Vifaa vya Kisasa vya Sayansi na Teknolojia

Utafiti ulibaini kwamba, Wilaya ya Micheweni ni sehemu mojawapo ambayo kuna matumizi makubwa ya vifaa vya sayansi na tekolojia, hususan vifaa vya habari na mawasiliano. Kwa mfano, katika jamii ya watu wa Micheweni siyo jambo la ajabu kuona mtoto mdogo akitumia kompyuta au simu za kisasa ambazo zinauwezo mkubwa wa kuona mambo mbalimbali ulimwenguni. Hali hiyo, inakuwa ni rahisi kwa watoto kupata fursa ya kuangalia vipindi mbalimbali vya michezo ya watoto, ikiwa ni pamoja na hadithi mbalimbali. Mtafiti aliwashuhudia watoto chini miaka kumi wakiwa wanaangalia televisheni huku wakibadilisha chaneli mara kwa mara, tena kwa ustadi mkubwa.

### 4.6.3 Urahisi na Upatikanaji wa Vifaa vya Sayansi na Teknolojia

Kwa majibu ya maelezo yaliyopatikana kutokana na utafiti uliofanywa kutoka kwa watafitiwa mbalimbali waliohojiwa, mtafiti alibaini kwamba, wengi wa wahojiwa hao waliibuka na hoja kwamba, kwa sasa kumekuwa na urahisi na upatikanaji wa vifaa vya sayansi na teknolojia, hususan zana za habari na mawasiliano.Waliendelea kueleza kwamba kutokana na kuwepo kwa maduka mengi yanayojishughulisha na uuzaji wa vifaa hivyo, kumesababisha ushindani wa kibiashara miongoni mwao na kushuka kwa bei kwa bidhaa hizo. Kwa mfano, simu, redio, kompyuta na hata televisheni. Suala hili linaungwa mkono na Bwana Massoud Salim. Wakati alipofanyiwa mahojiano katika mchakato wa kukusanya data za utafiti alieleza kwamba:

> Siyo siri kwa sasa sayansi na teknolojia imerahisisha upatikanaji wa vifaa hivyo vya mawasiliano miongoni mwa jamii, na kwa hali hii imechochea upatikanaji wa habari kuhusu mambo mbalimbali yanayotokea ulimwenguni. Kwa mfano, kuingia kwa bidhaa zilizokwishatumika, yaani (used) kumetoa fursa kwa watu, hata wa kipato cha chini kumuliki vifaa hivyo vya kisayansi[3]

Mfanyabiashara huyu anathibitisha na kuweka wazi juu ya urahisi na upatikanaji wa vifaa hivyo vya habari na mawasiliano. Hasa kwa kuibuka kwa vifaa chakavu, ambavyo vimeshatumika kutoka nje ya nchi kama vile China, Dubai na nchi nyingine kadhaa za Ulaya. Vifaa hivyo vinaletwa nchini mwetu na kuuzwa kwa bei rahisi sana na kuwawezesha watu wengi kumiliki vifaa hivyo bila ya usumbufu

### 4.6.4 Mwamko Kutokana na Uwekezaji wa Vifaa vya Habari na Mawasiliano

Utafiti umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa uwekezaji katika vyombo vya habari katika nchi yetu umeongezeka. Kuongezeka huku kwa uwekezaji wa vyombo vya habari kumetoa mchango kubwa kwa jamii kupokea matangazo kwa urahisi. Kwa mfano, matangazo ya redio ama televisheni yameimarika kwa kiasi kikubwa sana na kuweza kuwafikia wananchi waliowengi katika maeneo yao. Kampuni za ving'amuzi kama vile Azam TV, Startimes zimekuwa zikifanya vizuri katika suala zima la habari na mawasiliano. Kwa mfano, katika Wilaya ya Micheweni kutokana na uchnguzi tulioufanya tumegundua kwamba, watu wengi wanamiliki ving'amuzi vya Azam TV. Hivyo hali hii imetoa fursa kwa jamii ya Wilaya hiyo kupata mwamko juu ya mambo mbalimbali. Kwa mfano, watoto kuweza kujionea watoto wenziwao wa maeneo mengine wanavyoweza kucheza michezo mbalimbali. Ikiwa

---

[3] Mahojiano kati ya mtafiti na mfanyabiasha wa vifaa vya elektroniki yaliyofanyika kijiji cha Tumbe Februari 20/2015

ni pamoja na kusimuliana hadithi. Kwa mujibu wa maoni ya mtafitiwa alieleza kwamba;

> *Kutoka katika mfumo wa analogi hadi digitali kumetoa fursa kwa makampuni kadhaa makubwa kuwekeza zaidi katika sekta ya habari na mawasiliano kama vile mitandao na vyombo vya habari, huku uwekezaji huo ukitumia vyombo vya kisasa na vya uhakika zaidi. Hivyo ubora wa matangazo unaorushwa na makampuni hayo kutokana na uwepo wa ving'amuzi umeimarisha mawasiliano* [4]

Kwa jumla maneno hayo ya mtafitiwa, yanatilia maanani uimarikaji wa suala zima la sayansi na teknolojia, hususan katika nyanja ya habari na mawasiliano, kwani siyo siri matangazo kupitia vyombo hivyo vya kisasa yanasikikika na kuonekana katika hali nzuri kabisa kwenye maeneo ambayo kabla ilikuwa ni vigumu kupatikana.

### 4.6.5 Mwamko katika Uimarikaji wa Biashara ya Vifaa vya Sayansi na Teknolojia

Biashara inayohusiana na vifaa vya Sayansi na teknolojia kwa sasa inaonekana kustawi kwa kiasi kikubwa ndani ya nchi yetu. Maduka ya vifaa vya habari na mawasiliano yameongezeka kila kona ya nchi yetu. Kutokana na mwamko mkubwa ambao wameupata watu juu ya vifaa vya kisasa vya mawiliano. Hali hiyo huwachochea watu katika kumiliki vifaa hivyo ili waweze kujiona wanakwenda na wakati. Kwa mfano, kuongezeka kwa maduka ya vifaavilivotumika, yaani (used). umeimarisha biashara. Maduka haya kwa kawaida huuza vifaa kama vile simu za aina mbalimbali, kompyuta, redio na hata Ipadi. Hivyo, kwa kutumia gharama nafuu watu wanauwezo wa kumiliki vifaa hivyo. Kuongezeka kwa watumiaji wa vifaa vya sayansi na teknolojia kumeimarisha sekta ya biashara miongoni mwa jamiii.

[4] Mahojiano kati ya mtafiti na Mkurugenzi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba katika kitengo cha ICT Pemba, yalifanyika Februari 05/2015 huko ofisini kwake Chake Chake Pemba.

### 4.6.6 Muhtasari wa Sura ya Nne

Katika Sura Nne tumewasilisha na kujadili namna sayansi na teknolojia ilivyoathiri hadithi za watoto wa Wilaya ya Micheweni, katika suala zima la usimuliaji na uhifadhi wa hadithi hizo na tumejaribu kuchunguza namna fani na maudhui, vyote kwa pamoja vilivyoweza kuathiriwa kwa ujumla wake. Pia katika sura hii mtafiti amejaribu kuangalia mchango wa sayansi na teknolojia katika maendeleo ya hadithi za watoto. Vile vile sura hii imejikita katika kufafanua mwamko wa jamii ya Wilaya ya Micheweni walioupata kutokana na sayansi na teknolojia. Lengo la kuchunguza na kuvibainisha vipengele vyote hivyo vilivyojadiliwa lilikuwa kutaka kuonesha jinsi sayansi na teknolojia ilivyoathiri kipera cha hadithi za watoto wa Wilaya ya Micheweni Zanzibar. Sura inayofuata imejadili hitimisho la utafiti huu.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ni muhtasari wa mchakato wa utafiti huu, ambao unahusu athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto, kwa watoto wa Wilaya ya Micheweni Zanzibar. Matokeo ya utafiti yamedhihirishwa na mapendekezo ya maeneo ya kufanyiwa utafiti yametolewa.

## 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ilijikita katika kuchunguza athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto, kwa kuangalia mifano ya hadithi za ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Zanzibar. Hadithi zilizohusika ni zile zilizotambwa na wanafunzi wenyewe, walezi na baadhi ya hadithi ambazo zimesikika kupitia vyombo vya habari, kama redio, televisheni na hata kwenye Intaneti.

Utafiti huu uliongozwa na malengo matatu, ambayo ni kuchunguza namna madhara ya sayansi na teknolojia yanavyoathiri usimuliaji na uhifadhi wa hadithi za watoto, hususan hadithi za ngano, kutathmini mchango wa sayansi na teknolojia katika maendeleo ya utanzu wa hadithi za watoto, kwa kuangalia mifano ya ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Zanzibar na lengo la tatu ni kuchunguza mwamko wa wanajamii wa Wilaya ya Micheweni walioupata kuhusiana na athari ya sayansi na teknolojia katika utanzu wa hadithi za watoto, kwenye mifano ya hadithi za ngano. Katika malengo matatu hayo kila lengo lilipewa nafasi kutegemea na matokeo ya utafiti wenyewe.

Tasnifu hii kama ilivyokwisha kudokezwa kuwa ina jumla ya sura tano. Sura ya Kwanza inaweka msingi wa tasnifu hii kwa kutoa mwelekeo wa utafiti huu. Katika

sura hii mtafiti amejikita katika kufafanua usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, lengo la jumla na malengo mahususi, maswali ya utafiti, manufaa ya utafiti,sababu za kuchagua mada,nadharia iliyotumika, mihimili ya nadharia iliyotumika,mapengo yaliyojitokeza na kumalizia katika sura hii kwa kungalia hitimisho la sura ya kwanza.

Sura ya Pili inahusu mapitio ya maandiko ambayo yamegawanywa katika makundi matano. Kundi la kwanza la maandiko hayo linahusu dhana nzima ya Fasihi Simulizi kama ilivyopata kujadiliwa kutoka kwa wataalamu mbalimbali wa Fasihii, maandiko mengine yanahusu vipengele muhimu vya Fasihi Simulizi, kundi jingine la maandiko linaangalia Fasihi ya watoto. Pia maandiko yanayohusina na ufafanuzi wa hadithi pamoja na kujadili hadithi za watoto, sifa bainifu za hadithi za watoto, mapitio yanayofafanua hadithi za watoto kama kipera cha Fasihi Simulizi, pia yanayozungumzia dhana ya sayansi na teknolojia. Hali kadhalika katika sura hii tumeeleza mapengo ya utafiti yaliyojitokeza kutokana na mapitio yaliyoangaliwa na kumalizia sura hii kwa kugusia hitimisho la sura ya pili.

Katika Sura ya Tatu utafiti unaeleza juu ya mbinu na vifaa vilivyotumika katika mchakato mzima wa utafiti huu. Vipengele vinavyohusishwa katika sura hii ni pamoja na mpango wa utafiti,eneo la utafiti, walengwa wa utafiti yaani jamii ya watafitiwa na sampuli ya watafitiwa, ukusanyaji wa data, kwa kuangalia mbinu na njia zilizotumika katika utafiti katika kukusanyia data pamoja na mchakato wa ukusanyaji wa data na udhibiti, uchambuzi na uunganishaji wa data, pia sura hii imeangalia hitimisho la sura ya tatu.

Sura ya Nne inahusu mjadala wa matokeo ya utafiti. Sura hii imeongozwa na maswali matatu ambayo yameigawanya sura hii katika sehemu kuu tatu, ambapo

sehemu ya kwanza inajibu madhara yanayotokana na sayansi na teknolojia katika usimuliaji na uhifadhi wa hadithi za watoto na kuangalia athari zake katika fani na maudhui ya hadithi za watoto. Sehemu ya pili inazungumzia mchango wa sayansi na teknolojia katika maendeleo ya hadithi za watoto, na sehemu ya tatu inajibu suali la mwamko wa jamii ya Wilaya ya Micheweni kuhusiana na suala zima la sayansi na teknolojia, hususan kwa kuhusisha na hadithi za watoto.

Katika Sura ya Tano tunapata hitimisho la tasnifu hii. Sura hii inabeba vipengele kama vile muhtasari wa tasnifu yote, matokeo ya utafiti na mapendekezo kadhaa yanayostahili kupewa kipaumbele katika tafiti zijazo, hususan zinazofanana na kuhusiana kwa namna fulani ya utafiti huu.

## 5.3 Utoshelevu wa Mkabala wa Uchambuzi wa Data

Katika tasnifu hii, mkabala uliotumika ni wa nadharia ya Uhalisia**.** Nadharia hii imekuwa na umuhimu mkubwa sana katika kupata matokeo bora ya utafiti huu. Kwani nadharia hii ya uhalisia imetusaidia katika kujiridhisha kwamba, kila lengo tulilolijadili linasawiri uhalisi uliopo katika jamii ambayo ililengwa kufanyiwa utafiti.

Kutokana na nadharia hii ya uhalisia tuliweza kuangalia maandiko mbalimbali na kuingia uwandani juu ya mambo yanayojadiliwa, na hatimaye tukapata uthibisho wa kutosha kwamba, hali inayojadiliwa inasawiri katika kipindi husika. Kwa kuwa ni kipindi ambacho kimeshuhudia kukua na kuimarika kwa maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia, ambayo kwa kiasi kikubwa maendeleo hayo yanonekana kukiathiri kipera cha hadithi za watoto katika kila nyanja mbalimbali ikiwamo usimuliaji na hata uhifadhi wake.

## 5.4 Mchango Mpya wa Utafiti huu

Mchango mpya tuliougundua katika utafiti huu ni kwamba, tumeona namna sayansi na teknolojia ilivyoweza kukiathiri kipera cha hadithi za watoto, hususan katika usimulizi na uhifadhi wa hadithi hizo. Kwa sasa kutokana na kuimarika kwa sayansi na teknolojia, hadithi za watoto zinahifadhiwa na kusimuliwa kwa kutumia njia hizo za kisasa.

Jambo jingine kama mchango wa utafiti huu, ni kuhusu mchango wa sayansi na teknolojia katika maendeleo ya hadithi za watoto. Hivyo imebainika kwamba, kumbe sayansi na teknolojia ina mchango mkubwa katika maendeleo ya hadithi za watoto.

Pia utafiti huu umebainisha kwamba, kuwepo kwa athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto katika eneo la Wilaya ya Micheweni Zanzibar, hasa kutokana na maendeleo makubwa ya vyombo vya habari kama vile redio, kompyuta na hata televisheni.

Vile vile kutokana na utafiti huu imebainika kuwa kama vyombo vya sayansi na teknolojia, iwapo vitatumiwa ipasavyo vinaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuzihaulisha tanzu za Fasihi Simulizi na kuziwezesha kutumiwa kwa miaka mingi ijayo na kwa vizazi vijavyo.

## 5.5 Maoni Kuhusu Utafiti Huu

Utafiti huu licha ya kukusudiwa kuchunguza athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto, umetusaidia kuyafahamu mambo kadhaa ambayo yanahusiana moja kwa moja na utafiti au yanahusiana kwa sehemu. Kuna mambo kadhaa yaliyojitokeza katika utafiti huu na inafaa tuyatolee maoni.

Jambo la kwanza linahusiana na uga wenyewe wa hadithi za watoto, ambapo hili tumeona kwamba limekabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na utanzu huo kuanza kupoteza umuhimu wake kama njia mojawapo ya kujenga maadili ya jamiii, hususan kwa vijana. Hii inatokana na kwamba baadhi ya watu kukosa mwamko juu ya umuhimu wa kipera hiki cha hadithi za watoto.

Jambo jingine ni katika uwasilishaji wa hadithi hizo. Hadithi za watoto zimekabiliwa na changamoto katika uwasilishaji wake. Hali hii inatokana na kuwa kwa kawaida hadithi za watoto huwasilishwa kwa njia ya mdomo, lakini kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia vijana kuathirika na utamaduni wa kigeni. Hadithi za watoto zinaonekana kudhoofika sana. Hii ni kwa sababu kundi kubwa la watu hususan vijana hawapendi kutambiwa hadithi na mabibi zao kwa kuhisi ni mfumo na utaratibu uliopitwa na wakati, na badala yake hupenda kusikiliza sana redio na kungalia televisheni. Hali hii huchangia kwa namna moja ama nyingine kipera cha hadithi za watoto kuanza kupoteza hadhi yake, kwani warithi wa hadithi hizo wanajishughulisha zaidi kusikiliza redio ama kuangalia televisheni

Pia kunaonekana kuwa na uhaba wa hadhira iliyo hai. Uzoefu unatuonesha kuwa hadithi za watoto hadhira yake huwa hai na hushiriki katika utendaji kwa kumuuliza fanani maswali pale ambapo hadhira hiyo haikuelewa, kupiga makofi, kufurahi na kucheka lakini kwa wakati huu hadhira ya hadithi za watoto iko mbali na fanani wake. Kwa hivyo, hadhira huishia katika kusikiliza na kuona baadhi ya matendo tu na kukosa baadhi ya fursa kama kuuliza maswali. Hali hii inasababishwa na kutengwa kwa fanani na hadhira yake.

Vile vile utafiti umebaini kwamba, kuna baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Micheweni ambayo yanaonekana kuwa na ugumu mkubwa kupokea teknolojia mpya. Baadhi tu

ya maeneo ya Wilaya hiyo yamefaidika na teknolojia hii kwa kumiliki televisheni na kununua kanda za video, CD, DVD kwa wingi. Lakini hali inaonesha kuwa kuna baadhi ya maeneo ambayo hata nishati ya umeme haijafika, hivyo sehemu hizo zimekosa fursa ya kufaidika na teknolojia mpya katika usimuliwaji wa hadithi hizo za watoto kama wanavyofaidika watu wa maeneo mengine ya Wilaya hiyo.

Jambo jingine lililogunduliwa katika utafiti ni kuwa hadithi wazitambazo watoto kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia zimebadilika kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na zile za zamani katika kipengele cha uhifadhi na hata usawiri wake. Kwa mfano, kwa sasa hadithi nyingi za watoto hurushwa hewani kupitia vituo mbalimbali vya redio na televisheni

Pia, utafiti huu umegundua kwamba, watoto wengi wanaoishi Wilaya ya Micheweni wanatumia muda wao mwingi katika matumizi ya vifaa vya kisayansi kama vile simu, kompyuta na hata kusikiliza na kuangalia vyombo mbalimbali vya habari, kama vile redio na televisheni.Vyombo hivyo vya kiteknolojia, kwa pamoja, vimechangia kwa kiasi kikubwa sana katika kuharibu tabia na mienendo ya watoto, kutokana na baadhi ya matangazo na baadhi ya vipindi vinavyorushwa hewani kuwapotosha watoto.

## 5.6 Mambo Yanayotakiwa Kuzingatiwa Ili Kuondokana na Changamoto Hizo

Baadhi ya njia mbadala ambazo zinaweza kusaidia kupunguza changamoto zinazotokana na athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto ni kama ifuatavyo:

Kwanza, watu waelimishwe juu ya ukuzwaji wa Fashi Simulizi ya kijadi na kuelezewa madhara yatakayopatikana ikiwa baadhi ya vipengele vya Fasihi Simulizi

vitaanza kutoweka. Majukumu haya wayabebe zaidi walimu wanaosomesha shule za msingi. Kwa mfano, wawahimize watoto wa shule za msingi kujenga tabia na desturi ya kukaa pamoja na wazazi wao wakati wa mapumnziko. Kama vile nyakati za jioni au usiku kuwa pamoja na wazazi na kuanza kupokea hadithi na vitendawili mbalimbali katika nyakati hizo.

Jambo jingine ambalo ni muhimu katika kupunguza changamoto hizo ni kwamba, wale wasimulizi wanaopata nafasi ya kusimulia hadithi za watoto kwenye vyombo vya habari, kama vile kwenye redio ama televisheni, basi wapangiwe muda wa kutosha utakaoweza kutosheleza usimuliaji wao. Hili litaweza kuwasaidia watoto wadogo ambao bado akili zao hazijakomaa kiufahamu, waweze kufuatilia vyema wakati wa usimuliaji wa hadithi hizo kwa urahisi. Na kwa upande mwingine itaepusha kuwachanganya watoto hao wakati wa usimuliaji pindi wanaposikiliza hadithi hizo.

Vile vile kwa sehemu ambazo zinaonekana bado ziko nyuma hususan katika nyanja ya habari na mawasiliano, kutokana na ukosefu wa miundo mbinu ya uhakika kama vile suala la nishati ya umeme. Ni vyema serikali iharakishe huduma hizo ili kuwawezesha watu wa sehemu hizo waweze kujinunulia televisheni, redio na hata kompyuta. Hali hii itawasaidia watu wa maeneo hayo kufaidika na tanzu za hadithi zinazorushwa kwenye vyombo vya habari mbalimbali.

Njia nyingine ya kupunguza changamoto ya athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto ni kwamba, kuandaliwe mkakati maalum wa kuwatafuta wale magwiji wa fani ya hadithi za watoto ili wazitambe hadithi hizo na zirekodiwe. Kumbukumbu hizo zitakuwa zimehifadhiwa katika mazingira ambayo zitaweza kudumu kwa muda mrefu. Ili zitumike kwa matumizi ya baadaye pale zinapohitajika.

Vile vile watu watakapofundishwa na wakaelewa vizuri dhana ya sayansi na teknolojia na matumizi yake. Basi hali hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kusongambele kwa haraka sana Fasihi Simulizi na vipera vyake, kama vile kipera cha hadithi za watoto. Mchakato huu utasaidia sana kuwa na idadi kubwa ya watumiaji wa mitandao, ambao wanaweza kusaidia kuweka makala mbalimbali za Fasihi Simulizi na kuiwezesha hadhira pana kufaidika na Fasihi hiyo.

**5.7 Ugunduzi katika Utafiti huu**

Matokeo ya utafiti huu yametuonesha kwamba mazingira, wanayoishi watoto wa Wilaya ya Micheweni kutokana na kuwepo kwa vyombo mbalimbali vya habari ambavyo huonekana na kusikika, ndivyo kwa kiasi kikubwa vimezua mfumo mpya katika usimuliaji, uhifadhi, uwasilishaji, utungaji hadithi, usambazaji, pamoja na matini zake.

Jambo jingine lililogunduliwa katika utafiti ni kuwa baadhi ya hadithi wazitambazo watoto kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, zimebadilika kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na zile za zamani katika kipengele cha uhifadhi na hata usawiri wake. Kwa mfano, kwa sasa hadithi nyingi za watoto hurushwa hewani kupitia vituo mbalimbali vya redio na televisheni.

Pia, utafiti huu amegundua kwamba, watoto wengi wanaoishi Wilaya ya Micheweni wanatumia muda wao mwingi katika matumizi ya vifaa vya kisasa kama vile simu, kompyuta hali kadhalika kusikiliza na kuangalia vyombo mbalimbali vya habari, kama vile redio na televisheni. Vyombo hivyo vya kiteknolojia, kwa pamoja, vimechangia kwa kiasi kikubwa sana katika kuharibu tabia na mienendo ya watoto, kutokana na baadhi ya matangazo na baadhi ya vipindi vinavyorushwa hewani kuwapotosha watoto. Kwa mfano, katika utafiti huu, tuliweza kugundua kuwa watoto wadogo wanafahamu mambo makubwa kama vile mambo yanayohusu

mapenzi kuliko mambo mengine muhimu ambayo yanaweza kutoa msaada mkubwa katika maendeleo ya maisha yao.

Vile vile jambo jingine jipya ambalo tumeligundua kutokana na utafiti huu ni kwamba, mbinu zinazoweza kutumika katika uwasilishaji na usambazaji wa hadithi za watoto, zinaonekana kuathirika kwa kiasi kikubwa na maendeleo ya sayansi teknolojia.

Kutokana na kukua na kuimarika kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia, kumejitokeza athari nyingi katika hadithi za watoto waliopo ndani ya Wilaya ya Micheweni Zanzibar.

Athari hizo zinajitokeza katika fani, maudhui, usawiri, uwasilishaji wake, uhifadhi, usambazaji wake pamoja na sayansi hiyo kusababisha mporomoko wa maadili miongoni mwa jamii husika.

### 5.8 Mapendekezo ya Mtafiti kwa Serikali

Kwa vile sayansi na teknolojia imeshika kasi katika kila kipengele cha maisha yetu. Hivyo ni jukumu la serikali kuharakisha kuifikisha huduma ya nishati ya umeme kwa zile sehemu ambazo hazijafikiwa na huduma hiyo. Hii itasaidia jamii kupata fursa ya kufaidika na tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi ambazo hurushwa hewani na vyombo vya habari na vile redio na televisheni na katika Intaneti.

### 5.9 Mapendekezo Kuhusu Tafiti Zijazo

Mpaka sasa kutokana na uchunguzi tulioufanya katika utafiti huu kuhusiana na athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto. Kutokana na uchunguzi huo tumebaini kuwa, maendeleo yaliyoshika kasi ya sayansi na teknolojia katika ulimwengu wa leo ni dhahiri yameathiri kila sekta na katika kila kipengele cha

maisha ya wanadamu. Hivyo, athari hizo hazikujikita katika kipera cha hadithi za watoto katika kipengele cha ngano peke yake, bali athari hizo zinapatikana kwenye vipera vingine vya Fasihi Simulizi. Kama vile methali, vitendawili na hata misemo.Ili vipera hivyo kuvihusisha na maendeleo ya sasa ya sayansi na teknolojia.

Hivyo, ni mapendekezo ya mtafiti kwa watafiti wengine ni kwamba ipo haja ya kuzamia kwenye vipera vingine vya Fasihi Simulizi ili kufahamu kiwango cha athari za sayansi na teknolojia katika vipera hivyo vya Fasihi Simulizi. Kwa kuwa kila kukicha ulimwengu huchukua sura mpya kutoka hali moja na nyingine. Fasihi Simulizi na vipera vyake kwa vile ni mali na zao la jamii nayo pia haina uwezo wa kukwepa mabadiliko hayo yanayoibuka siku hadi siku.

## MAREJELEO


Alderson, C. G &Beretta, A.(1992*), Evaluating, Second Edition: Applied Linguistic*, C.U.P, Cambridge.

Arbuthnot M. na Z. Sutherland. (1947), *Children's Literature.* Scott Forsman and Company, London.

Babbie. (1992), *The Practice of Social 6th Edition*, Wadsworth Publishing Company.

BAKITA. (1969/70), *Baraza la Taifa la Lugha ya Kiswahili Taarifa za Kila Mwaka*.BAKITA, Dar es Salaam.

BAKIZA. (2010), *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Oxford University Press,Dar es Salaam.

Balisidya, M. L. (1987),'*Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi*' Mulika 19: 2-10.

Bakize, L. H. (2004), *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*, Moccony Printing Press, Dar es Salaam.

Bukenya, A. and Nandwa, A. J (1977), African *Oral Literature*, Longmans, Nairobi.

Bryman, A. (2004), *Social Research Methods (2nd Edition)*, Oxford University Press, Oxford.

Dadi, K.S. (1995), *Dhima ya Vyombo vya Habari katika Matumizi ya Msamiati; ktk Mlac (mh) Kiswahili na vyombo vya Habar*i, TUKI, Dar es Salaam.

Davies, A. (1973), *Literature for Children*, Open University Press, Portstmouth.

Daymon, C. and Holloway, I. (2002) *Qualitative Research Methods in Public Relations and Marketing Communications*,.Routledge, London.

Finnegan, R. (1971), *Oral Literature in Africa*, Oxford University Press. Oxford.

Hamad, A.K. (1982), *Fasihi Simulizi ni nini? Msingi wa Nadharia ya Fasihi.* Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar.

Herman, L. (2011), "Dhima ya Mwingilianomatini kwenye Hadithi za Watoto katika Kiswahili,'' *katika Kioo cha Lugha*, Juz.9, kur.73-83.

Herman, L (2012), "Fantasia katika Fasihi ya Kiswahili kwa Watoto,*''katika Kioo cha Lugha*.Na. 1. TUKI, Dar es Salaam.

Hollow .L.(1997), *Basic Concepts for Qualitattive Research*. Black well Science.Oxford.

Hunt. P. (1994), *An introduction to Children's Literature.* Oxford University Press, Oxford.

Hunt. P. (1994), *An introduction to Children's Literature,* Oxford University Press, Oxford.

Kahigi. K. K. (1995), *Lugha katika Vitabu vya Watoto,'' katika Kioo cha Lugha*. Na.1. TUKI, Dar es Salaam.

Kirumbi, P .S. (1975), *Msingi wa Fasihi*, Shingwaya Publisher, Nairobi.

Kimani, N. (2006), *Fasihi Simulizi na Nadharia ya Fasihi ya Kiafrika' Katika Fasihi ya Kiswahili*, Twaweza communications, Nairobi.

Kitabuge.J.S.(2011),Athari Chanya na Hasi za maendeleo ya Sayansi na Teknolojia katika Fasihi Simulizi. *Tasnifu kwa Ajili ya Shahada ya Pili,* Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kitundu.A.M. (2011), Athari za Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia Kwenye Fasihi Simulizi Nyimbo za Ibada ya Kikiristo Tanzania. *Tasnifu kwa Ajili ya Shahada ya Pili,* Chuo Kikuu cha Dodoma.

Konde, H. (1984), Press *Freedom in Tanzania*, Eastern African Publication, Arusha.

Kothari, C.R. (1990), *Research Methods: Methods and Techniques* Wiley Eastern Ltd. New Delhi.

Kothari, C. R. (1993), *Research Methodology; Methods and Techniques*: WileyEastern Ltd,,New Delhi.

Kothari, C. R (2004), *Research Methodology, Methods and Techniques, Second Edition*, New Age International (P) Ltd.Delhi.

Madumulla J. S. (2009*), Riwaya ya Kiswahili, Nadharia, Historia na Misingi ya Uchanganuzi.* Mture Educational Publisher Ltd. Dar es Salaam.

Matteru, M. D (1983), Fasihi *Simulizi na Uandishi wa Kiswahili; Katika Fasihi z aSemina ya Kimataifa Wa Kiswahili,* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

Mbiti, J. (1969),.*African Religions and Philosophy*. Heinemann Educational Books, London.

McGrew, P. (2008), *Globalization in Terms at the Massive Advances in Global*

*Communication, Transport and Informatics,* University of Strength Clyde. Southempton.

Mlacha, S. A. K. (1995), '*Fasihi Simulizi na Usuli wa Historia ya Pemba''Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili.TUKI*. Uk -16-26.Dar es Salaam.

Mlacha, S. A. K (2004), *Kiswahili na Vyombo vya Habari*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili,Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1989), *Tanzu za Fasihi Simulizi. Katika Mulika,* Na. 21. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, kur. 1-2, Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. (1983),*' Utafiti wa Fasihi Simulizi*'' *Makala ya za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili,* III Fasihi. TUKI, Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1996), *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Dar es Salaam.

Mutembei, A. K. (2006), *Mulika,* Vol. 27: 11 TUKI, Dar es Salaam.

Mwansoko, H. J. M. (1995), *Dhima ya Vyombo vya Habari katika Ukuzaji, Usanifishaji naUenezaji wa Istilahi, Ktk* Mlacha (mh) *Kiswahili na Vyombo vya Habari*. TUKI. Dar es Salaam.

Nandwa, J and Austin, B. (1983), *African Oral Literature for Schools*, Longman Nairobi.

Ndunguru, P. C. (2001), Lecture *on Research Methodology for Social Science*, Mzumbe University.

Ngugi, P.M. (2011), "Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto Katika Shule za Msingi Nchini Kenya," *katika Kioo cha Lugha,*Juz. 9, kur.84-94.

Patton, M. (2002), *Qualitative Research and Evaluation* (*3rd Edition*). Sage Publication. London.

Senkoro, F. E. (1987), .*Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam. Press And Publicity Centre.

Steven,Y.(2011), Athari za Maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Nyimbo za Watoto Waishio Mijini. Mijini Mbeya na Tukuyu. *Tasnifu kwa Ajili ya Shahada ya Pili,* Chuo Kikuu cha Dodoma.

Wamitila, K. W.(2011), *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Focus Publications LTD, Nairobi.

Wafula,M. N. (2011) *'Tradition' versus 'Modernity': Generational Conflict in Vuta N'kuvute, Kufa Kuzikana, Msimu wa Vipepeo and Tumaini*.http://www.ifeas.uni-mainz.de.SwaFo, Volume 18. html, 27/08/2012.

Wamitila, K. W. (2003), *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*, Kenya Focus Publication, Nairobi.

Wasamba, P. (2010), Indigenous *Knowledge and Intellectual Property Rights in the Age of Globalization* ,Internationals societies for Oral literature, Mombasa.

Wellek, R..(1961*), A history of Modern Criticism 175()-lY5 () Vol 3.* Cambridge university Press, Cambridge.

# VIAMBATISHO

**Kiambatanisho 1: Hojaji na Madodoso Yaliyotumika Kukusanyia Data za Utafiti Huu Kutoka kwa Wazazi, walimu, wafanyakazi wa Idara ya Habari na Wafanyabiashara.**

a) Mwongozo wa Hojaji kwa wanafunzi, wazazi, walezi,walimu na wafanyakazi wa wizara ya habari

b) watoto waishio Wilaya ya Micheweni Zanzibar.

1. Una umri wa miaka mingapi?
2. Je umepata kusikia sayansi na teknolojia? Kama ndivyo eleza unavyoifahamu.
3. Ni vitu/vyombo gani vya habari na mawasiliano vinaathiri sana hadithi za Watoto? Kwa namna gani?
4. Kuna uhusiano wowote baina ya maendeleo ya sayansi na teknolojia na habari na mawasiliano katika hadithi wasimuliwazo watoto?
5. Unafikiri ni kwa sababu gani watoto wanapenda kutumia muda wao mwingi katika matumizi ya vyombo vya habari na mawasiliano?
6. Je waweza kuelezaje mabadiliko ya tabia za watoto kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika jamii ?
7. Ni athari gani zitokanazo na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto waishio Wilaya ya Micheweni?
8. Toa maoni yako ya jumla kuhusu mwamko wa jamii ya Wilaya ya Micheweni kuhusiana na athari za sayansi na teknolojian katika hadithi za watoto. hususan kwa kuangalia mifano ya hadithi za ngano.

Asante kwa ushirikiano wako

**Kiambatanisho 2: Dodoso kwa Watoto Waishio Wilaya ya Micheweni Katika Mkoa wa Kaskazini Pemba**

Tarehe ya kufanya dodoso…………………………

Mahala pa Utafiti. Wilaya ya Micheweni Zanzibar.

Tunafanya utafiti kuhusu athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto, kwa kuangalia mifano ya hadithi za ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Zanzibar.

Tafadhali tunaomba ushirikiano wako katika kujibu maswali ya utafiti yafuatayo.

Weka alama ya vema katika mabano ( ) na toa maelezo mafuti katika sehemu zilizoachwa wazi…………

1 Unasoma darasa la ngapi?..................................................

Kwanza ( ) Pili ( ) Tatu ( ) Nne ( ) Tano ( ) Sita ( ) Saba ( )

2 Taja vyombo unavyovifahamu ambavyo hutumika katika kutoa habari na burudani kwa mfano hadithi za watoto.

i………….......................ii……………………………..iii…………………

iv………………………….

3 Andika jina la msanii pamoja na jina la kipindi chake cha hadithi za watoto katika kituo cha televisheni kimojwapo hapa Tanzania.

i………………………………..

ii………………………………..

4. Taja vituo vitatu vya redio na vitatu vya televisheni unavyovifahamu ambavyo vinarusha matangazo yake na kufika vyema katika Wilaya ya Micheweni Zanzibar

i…………………………….ii………………………….iii………………

iv………………………….v……………………………vi……………

5. Taja hadithi yoyote ya watoto uliyoisikia katika redio au televisheni pamoja na ujumbe ulioupata kupitia hadithi hiyo.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

………

6a)Kuna madhara yoyote yale yatokanayo usimuliaji na uhifadhi wa hadithi za watoto, kwa mfano hadithi za ngano kupitia vyombo vya habari na mitandao kama vile televisheni na kompyuta.

Ndiyo ( ) Hapana ( )

b) Kama jibu ndiyo yataje madhara hayo yanayojitokeza kupitia njia hiyo ya usimuliaji na uhifadhi wa hadithi hizo za watoto.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

………

7. Taja vifaa vyingine ambavyo hutumika kuhifadhiwa hadithi za watoto. Kwa mfano hadithi za ngano.?

i………………………..

ii………………………..

iii……………………….

iv………………………

8. Toa maoni yako ya jumla kuhusu athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto. Kwa jamii ya Wilaya ya Micheweni Zanzibar. Kwa kuangalia mifano ya hadithi za ngano.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………..................

....................................................................................................................................

..........................

Asante kwa ushirikiano wako

**Kiambatanisho 3: Hojaji/ Usaili kwa wadau mbali mbali wa Fasihi Simulizi**

Katika swali 1, 4,5,6,7 na 8 jadili hoja za maswali hayo ukizingatia ufafanuzi wa pande mbili, yaani hadithi za watoto zilivyokuwa zama za kale kwa upande mmoja na hali ilivyo katika siku za leo za maendeleo ya sayansi na teknolojia.

1.Kwa mujibu wa ujio wa maendeleo ya sayansi na teknolojia ya siku za leo, ipi ni Fasihi Simulizi?

2. Upi ni mfumo bora zaidi ungependelea utumike katika suala zima la kustawisha na kuendeleza Fasihi Simulizi katika kipengele cha hadithi za watoto nchini Tanzania.Weka alama panapostahili.

A Fasihi simulizi ya kimapokeo pekee ( )

B. Fasihi Simulizi inayozingatia vifaa vya sayansi na teknolojia pekee. ( )

C .Fasihi simulizi ya kimapokeo yaani ya (jadi) pamoja na ile inayokwenda sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia ( )

3. Ni athari zipi hujitokeza wakati hadithi za watoto zinapohifadhiwa kwa kutegemea kumbukumbu za kichwa cha fanani pekee?

b. Ni athari zipi hujitokeza hadithi za watoto zikihifadhiwa kwa kutumia zana/media za kiteknolojia yaani;-

Runinga

CD/DVD/VCD

Kanda za kaseti/ Vidio

Maandishi

Redio

Tepurekoda

Kompyuta

Vinasa sauti

Makazi/ makumbusho

4. Maendeleo ya sayansi na teknolojia yanaleta athari zipi katika kipengele cha hadhira ya Fasihi Simulizi siku za leo.

5. Suala la uwasilishaji wa hadithi za watoto limeathirika vipi kutokana na ujio wa maendeleo ya sayansi na teknolojia katika zama za leo?

6. Dhana ya utendaji katika Fasihi Simulizi lina mabadiliko gani katika zama hizi za maendeleo ya sayansi na teknolojia.

7. Kuna athari zipi zinazojitokeza katika kipengele cha umuliki katika Fasihi Simulizi kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika zama za sasa.

8 Ni kwa namna gani teknolojia ya habari na mawasiliano (teknohama) imekuwa chachu na kichocheo kikuu katika kuathiri hadithi za watoto kwa jamii ya Tanzania, hususan Wilaya ya Micheweni Zanzibar?

Ahsante kwa ushirikiano wako.

**Kiambatanisho 4: Picha Mbalimbali za Utafiti**




Kiambatisho namba 1: Picha ya mtafiti akiwa pamoja na wanafunzi wa darasa la sita katika Skuli ya Msingi Tumbe akirekodi jinsi watoto hao wanavyotamba hadithi za ngano (Utafiti, 2015).



Kiambatisho namba 2. Mtafiti akisikiliza hadithi kutoka kwa mwanafunzi wa Skuli ya Msingi Tumbe (Utafiti, 2015).




Kiambatisho namba 3.  Picha ya mtafiti akifanya mahojiano na mwalimu wa somo la Kiswahili wa Skuli ya Msingi Wingwi kuhusiana na athari za sayansi na teknolojia (Utafiti, 2015).



Kiambatisho namba 4. Picha ya mtafiti akifanya mahojiano na mwalimu mkuu wa Skuli ya Msingi Tumbe (Utafiti, 2015).



Kiambatisho namba 5. Mtafiti akisikiliza na kurekodi hadithi za watoto kutoka kwa wanafunzi wa Skuli ya Msingi Micheweni (Utafiti,2015).



Kiambatisho namba 6. Mtafiti akisikiliza hadithi kutoka kwa wanafunzi wa Skuli ya Msingi Micheweni (Utafiti,2015).



Kiambatisho namba 7. Mtafiti akifanya mahojiano na mfanyabiashara wa CD, DVD na VCD katika mji wa Tumbe Wilaya ya Micheweni (Utafiti,2015).